ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
55.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
58. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
62.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
63.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
65.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
67.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
68.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
69.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
72.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim **Katibu wa Baraza la Wawalishi**

Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 13 Julai, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 199

Ziara za Viongozi wa Wakuu Nchi za Nje

Mhe. Asha Bakari Makame (Kny: Mhe. Hija Hassan Hija) – Aliuliza:-

Namuuliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nawapongeza sana Viongozi Wakuu wa SMZ, Rais wa Zanzibar, Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais kwa uamuzi wao wa kutembelea nchi za nje mara baada ya Uchaguzi Mkuu.

Kwa hatua hii ya viongozi iliwapa wananchi matumaini ya kupata misaada, ambapo Mhe. Rais amewahi kwenda Uturuki, Makamu wa Kwanza wa Rais amewahi kwenda nchi za Falme za Kiarabu na Makamu wa Pili naye pia amewahi kwenda nchini Iran. Naamani wote hawa ziara zao ziliwapatia mafanikio Wazanzibari.

(a) Je, ni mafanikio gani viongozi wetu walituletea?

(b) Pamoja na ziara za viongozi wetu kuja na mafanikio, lakini upo udhaifu wa ufuatiliaji, Je, serikali imejipanga vipi kwa ziara za viongozi wetu kufuatilia zile ahadi walizopewa nchi za nje.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe, swali lake Nam. 199 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kwa niaba ya Viongozi wetu Wakuu naomba kupokea pongezi alizozitoa Mhe. Mjumbe kwa ziara zile wanazofanya viongozi wetu nchi za nje kwa manufaa ya kuitafutia mema Zanzibar.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Viongozi wetu hawa Wakuu mara baada ya kuingia madarakani walifanya ziara nchi za nje, kwa lengo la kutafuta misaada na mikopo kwa ajili ya kuisaidia Zanzibar.

Kwa hivyo, kama nilivyosema mara tu baada ya Serikali ya Awamu ya Saba kuingia Madarakani Viongozi hao Wakuu, akiwemo Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais walifanya ziara nchi za nje kwa nyakati tofauti.

Rais wa Zanzibar alifanya ziara katika nchi ya Turkey na Libya, wakati Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais alifanya ziara katika nchi za Uholanzi, Umoja wa Falme za Kiarabu na Omar. Aidha Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi alifanya ziara katika nchi za Seychelles, Iran na Umoja wa Falme za Kiarabu. Mhe. Spika, wakati wa ziara hizo Viongozi wetu hawa Wakuu walipata nafasi ya kuzungumza na Viongozi Wakuu wa nchi walizozitebelea.

(a) Mhe. Spika, ziara hizi za Viongozi Wakuu wa Serikali zilizofanywa katika nchi za Turkey, Uholanzi, Falme za Kiarabu, Oman, Seychelles na Iran, zimekuwa na mafanikio makubwa kwa upande wa Zanzibar.

Kwa mfano, ziara ya Mhe. Rais nchi Turkey makubaliano kadhaa yamefikiwa, ambapo Turkey itashirikiana na Zanzibar katika kuimarisha Sekta za Afya, Utalii, Elimu, Kilimo, Mawasiliano na Miundombinu.

Mhe. Spika, mashirikiano katika Sekta ya Afya yatajumuisha kupatia wataalamu wa afya kutoka Turkey, kwa ajili ya kufanya tathmini ya mahitaji katika Wizara ya Afya, kuongeza nafasi za masomo ya udaktari, madawa, ufundi, teknolojia ya habari na kupatiwa Wataalamu wa Matibabu ya Moyo na maradhi mengineyo. Aidha Turkey watatoa wataalamu watakaosaidia katika Vitengo vya *Orthopedic Surgeon, Cardiologist, Pediatrician and Physician*.

Katika utalii ujumbe kutoka Zanzibar utafanya ziara nchi Turkey hivi karibuni kwa ajili ya kuanzisha rasmi uhusiano katika sekta hii, hasa katika Miji ya *Anca* na *Antalia*. Vile vile jengo la Beit-el-Ajab litaimarishwa, Chuo cha Maendeleo ya Utalii Maruhubi nacho kitaimarishwa na watembezaji watalii Wazalendo watasaidiwa kwa kujengwe uwezo.

Aidha Shirika la Ndege la Turkey, yaani *Turkish Airline* linaangalia awezekano wa kuanzisha safari za moja kwa moja baina ya Zanzibar na Turkey.

Mhe. Spika, katika Sekta ya Elimu pia kuna makubaliano kadhaa ambayo tunategemea yataendelezwa.

Halikadhalika kama nilivyosema mafanikio mengine ni pamoja na kufanyiwa matengenezo Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Karume na kupanua Uwanja wa Ndege wa Pemba hadi kufikia kiwango cha kuweza kutua ndege kubwa kama vile *Boeing*. Mhe. Spika, tayari maelewano katika hatua za awali za MOU yameshaanzisha na mazungumzo bado yanaendelea.

Vile vile ziara ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais. Uholanzi imeyapokea maombi ya Zanzibar yanayohusiana na utunzaji wa mazingira, mapambano dhidi ya Madawa ya Kulevya, Kudhibiti janga la UKIWMI na huduma kwa Watu Wenye Ulemavu.

UAE imekubali mashirikiano na kuisaidia Zanzibar katika maeneo mbali mbali. Aidha Serikali ya Omani ilipokea maombi ya Zanzibar yenye lengo la kuboresha huduma za jamii na kiuchumi katika Sekta ya Afya, Elimu, Maji, Kilimo, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Miundombinu. Oman imeihakikishia Zanzibar katika maeneo inayoyahitajia.

Mhe. Spika, pia ziara ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi zilikuwa na mafanikio yafuatayo:-

(i) Kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo Zanzibar hususan katika Sekta za Uvuvi na Utalii;

(ii) Kuona miradi mbali mbali ya maendeleo na shughuli za kiuchumi, ili kujifunza namna zitakavyoendeshwa na

(iii) Wakati alipokuwa njiani kurudi nyumbani Mhe. Balozi Seid Ali Iddi katika nchi za Falme za Kiarabu alipata fursa ya kuzungumza na Uongozi wa Juu wa nchi ya Uarabuni, ambayo imeonesha nia ya kuwekeza Zanzibar katika maeneo yafuatayo:-

- Ujenzi wa Bandari pamoja na Kiwanda cha Kusindika Samaki;
- Huduma za Meli za Mizigo, Uchukuzi na Vifaa vya Mafuta;

- Kilimo, Usarifu wa Mazao ya Chakula na Utalii.

(b) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeandaa utaratibu mzuri wa kufuatilia ahadi wanazopewa viongozi wetu, wakati wanapotembelea nchi za nje kwa kuweka maafisa maalum wa kuratibu, kusimamia pamoja na kufuatilia ziara za kiserikali zinazofanywa na viongozi hawa pamoja na ahadi wanazopewa wakati wa ziara hizo.

Kwa kweli maafisa hao wanatekeleza majukumu yao chini ya uongozi wa Makatibu Wakuu wa (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Ahsante sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwanza nimpongeze kwa majibu ambayo ametupa kwa urefu pamoja na ufafanuzi mzuri. Lakini atakubaliana na mimi kwa kuwa viongozi wetu baada ya kurudi katika ziara, basi kidogo kuna kuwa na udhaifu wa ufuatiliaji. Vile vile kwa kuwa Wizara ya Afya ni kiungo muhimu kwa jamii.

Je, atakubaliana na mimi katika ziara hizo ni kwamba vyema hiki kiungo cha afya kikafuatiliwa, ili kuhakikisha kuweza kupata madaktari hao.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba sasa tumejipanga vizuri, kwamba baada ya ziara hizi za Viongozi wetu Wakuu, basi maafisa wale dhamana hasa Makatibu Wakuu wa zile sekta wanakuwa mstari wa mbele katika kufuatilia yale yote yaliyoagizwa.

Kwa hivyo, alivyozungumza kwenye upande wa afya, nakubaliana na yeye kweli tutilie mkazo na serikali yetu kwa kweli suala hili imelivalia njuka kulipa umuhimu wa namna yake mwaka huu. Kwa maana hiyo, nakubaliana na Mhe. Mjumbe. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuongezea kidogo, ili Wajumbe wa Baraza lako tukufu waweze kufahamu yanayojiri. Mhe. Spika, pamoja na kuwepo kwa Kamati ya Wataalamu Baraza la Mawaziri pia limeunda Kamati ya Mawaziri, ambayo itaongoza ufuatiliaji katika nchi mbali mbali.

Kwa mfano, kwa ziara za Makamu wa Kwanza wa Rais, Mwenyekiti wa Kamati ya Mawaziri ni Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa upande wa ziara za Makamu wa Pili wa Rais, Mwenyekiti wa kamati ya Mawaziri ni Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na kwa ziara za Mhe. Rais Mwenyekiti wa Kamati ni mimi mwenyewe Mhe. Omar Yussuf Mzee. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tunao mawaziri wa sekta mbali mbali. Kwa mfano, kwa upande wa Turkey ninao Mawaziri kama Mhe. Waziri wa Miundombinu, Mhe. Waziri wa Afya ni Mjumbe na hayo ni kwa upande wangu mimi.

Kwa upande wa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais mimi ni Mjumbe pamoja na mawaziri wengine ni wajumbe.

Mhe. Spika, nataka niongezee tu kwamba tumetia uzito wa ufuatiliaji katika masuala haya. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa vikalio vya skuli vimekuwa ni tatizo kubwa kwa muda mrefu na utanuzi wa elimu. Kwa kweli tatizo hili limekuwa ni nje ya uwezo wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na bajeti yake.

Je, ziara hizi za Viongozi Wakuu, zinatilia mkazo suala hili la limeshughulikiwa kwa kiwango gani, ili sasa tuondokane na wanafunzi wetu kugaragara katika ardhi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, ni kweli kutokana na ongezeko la vijana wetu kwenda maskulini, basi tumekuwa na matatizo ya vikalio. Kwa hivyo, serikali yetu inajitahidi kadri ya uwezo wake kulikwamua tatizo hilo kidogo kidogo, kwa sababu watoto ni wengi kadri wanavyokuja na *Alhamdulillah* ni neema ya Mwenyezi Mungu, lakini na serikali nayo imejidhatiti kwamba tusimuache mtoto, yaani wote waende maskulini.

Sasa ku-*cop* na hiyo *volume* ya watoto, basi serikali nayo inajitahidi kutafuta misaada pamoja na hayo mengine yaliyozungumzwa viongozi nalo hilo wamelipa *priority*. *(Makofi)*

Nam. 133

Ukosefu wa Mashine ya *DNA*

Mhe. Fatma Mbarouk Said – Aliuliza:-

Miongoni mwa ushahidi muhimu wa kesi za kupewa uja uzito wasichana ni kutokupatikana kwa kipimo cha *DNA*, kipimo ambacho kinahitaji gharama kubwa. Aidha kipimo hicho hakipo hapa Zanzibar. Kutokana na sababu hizo wazazi wa waathirika huvunjika moyo kufuatilia kesi za aina hiyo.

(a) Serikali ina mpango gani wa kupatikana kipimo hicho hapa nchini?

(b) Serikali haioni kuwa ukosefu wa kipimo hicho utawafanya wanaume waendelee kuwapa wasichana uja uzito, huku wakielewa hapatopatikana uthibitisho.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 133 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, serikali inao mpango wa kununua mashine ya *DNA* kutokana na umuhimu wake. Hatua zilizokwisha chukuliwa ni:-

- Kufanya upembuzi yakinifu kazi kwa kusaidiana na Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ya Muungano.

- Kutayarisha jengo la Mkemia Mkuu kwa ajili ya kuweka mashine hiyo.

(b) Mhe. Spika, mashine ya *DNA* ni mashine ya kupima uasilia pale panapotokea utata wa mtoto. Kipimo hicho hufanyika baada ya kuzaliwa mtoto na kuthibitisha nani baba.

Suala la kuwapa mamba wasichana ni ukosefu wa maadili na hakuna uhusiano na ukosefu wa mashine hiyo.

Nam. 106

Ongezeko la Migogoro ya Ardhi

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa – Aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko mengi ya migogoro ya ardhi katika Mkoa wa Kaskazini hasa Wilaya ya Kaskazini 'A'.

(a) Je, kuanzia mwaka 2005 hadi hivi sasa, kuna migogoro ya ardhi mingapi ambayo serikali imeweza kuitatua, mingapi bado haijapatiwa ufumbuzi na kwa nini hayatatuliwi.

(b) Je, serikali inaweza kutueleza ni kwa nini migogoro hii hivi sasa imekuwa mingi kuliko ilivyokuwa zamani.

(c) Je, serikali ina mpango gani wa kuweza kuwasaidia wananchi, ili kuondosha tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 106 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, migogoro iliyoweza kutatuliwa ni kumi na saba (17), ambayo haijatolewa hukumu ni sabiini na tatu (73) na hii ni kutokana na kuchelewa kuteuliwa kwa Mahakimu katika Mahakama za Mikoa.

(b) Ni kweli migogoro imeongezeka tafauti na zamani kwa sababu ardhi imekuwa na thamani na hii ni kutokana na uwekezaji, hivyo wananchi wengi wameelewa thamani ya ardhi kutokana na uwekezaji tafauti na zamani. Pia ongezeko la watu na kukua kwa shughuli mbali mbali za matumizi ya ardhi inachangia kuongezeka migogoro hiyo.

(c) Serikali imo mbioni kutoa elimu kwa wananchi, ili kuondoa matatizo mengi yanayotokana na matumizi ya ardhi.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Wakati alipokuwa akijibu amesema kwamba kuna migogoro ambayo bado haijatatuliwa, lakini tatizo kukosekana kwa Mahakimu wa Mambo ya Ardhi katika Mikoa.

(a) Mhe. Spika, nataka kujua ni lini serikali itapeleka Mahakimu hao kwa ajili ya kutatua migogoro hiyo?

(b) Nataka kujua mikakati ya wizara katika kuwaelimisha wananchi, ili waweze kujua huo utaratibu mzima wa matumizi yao ya ardhi, ili kuondosha hii migogoro iliyokuwepo. Kwa hivyo, ni mikakati gani wizara kama wizara imepanga, ili kuweza kuhakisha kwamba migogoro hii inatatuka kwa kuwapa elimu wananchi?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kuhusu uchelewaji wa Mahakimu, tayari suala hili tumeshazungumza na Mhe. Jaji Mkuu na wamesema wanafanya maandalizi na itakapokuwa tayari tu, basi watateuliwa Mahakimu hao ili kuyaondoa matatizo haya. Hilo moja.

Pili wizara yangu imo katika kuwaelimisha wananchi kwa kupitia vyombo vya habari kama vile *television* pamoja na *radio*.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Spika, hivi karibuni mimi mwenyewe nilimshuhudia Mhe. Waziri alitatua tatizo la wananchi wa Pwanimchangani na hati akafuta.

Sasa Mhe. Naibu Waziri ametoa kauli kwamba yumo katika utaratibu wa kuondoa na haya matatizo mengine ambayo yanaendelea siku hadi siku.

Je, ni lini Mhe. Waziri utaratibu huo au ataunda kamati kwa ajili ya kutatua migogoro hiyo ya wananchi?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ni kweli tulikaa na kuzungumza na alinishauri labda tuunde kamati, ushauri nimeupokea na tunauzingatia. Lakini bado hata tukiunda kamati kama viongozi mbali mbali hawatoachana na kuiongeza migogoro ya ardhi kwa kugawa ardhi pamoja na maeneo basi hiyo kamati haitofanyakazi.

Kwa hivyo, juhudi tunazozichukua mara tu baada ya kumaliza Baraza hili tutafanya semina moja kubwa na kuwaalika viongozi wote wa ngazi zote. Hivyo, tutazungumza nao katika suala zima la kuheshimu madaraka ya kumiliki ardhi pamoja na kutusaidia kuondosha migogoro hiyo, sasa

watakapofahamu ninahakika migogoro itapungua. Mhe. Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini kwa kuwa mgogoro wa ardhi katika Kisiwa hiki cha Zanzibar umekuwa sugu.

Je, atakubaliana na mimi Mhe. Waziri kwamba miongoni mwetu sisi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunawajibika katika majimbo au kwenye sehemu ambayo tunakaa, ili kuhakikisha na sisi tunaifanyakazi ya kudhibiti ardhi mule tunamokaa? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa upande mmoja na hii ni asilimia ndogo nakubaliana naye, lakini kwa upande wengine tena ni asilimia kubwa migogoro mingi ya ardhi tunaisababisha sisi wakubwa, tukiwemo Mawaziri, Wawakilishi, Wakuu wa Mikoa, Wilaya mpaka Mawidani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikasema nakubaliana naye kwa asilimia ndogo, lakini asilimia kubwa migogoro tunaisababisha sisi. Kwa hivyo, naomba kutoa wito hapa Barazani kwanza watuachie wizara tuitatue migogoro iliopo na tuizuie mingine isije, ikiwa kuna namna ya kutusadia kwa ajili ya kuitatua, basi watusaidie. *(Makofi)*

Nam. 129

Ukosefu wa Maji Shehia ya Chaani

Mhe. Viwe Khamis Abdalla (Kny: Mhe. Ussi Jecha Simai) – Aliuliza:-

Muda mrefu sasa wananchi wa Jimbo la Chaani katika Shehia ya Chaani Kubwa wanakabiliwa na ukosfu wa maji safi na yaliyo salama. Kwa sasa uchimbaji wa kisima umekamilika lakini tatizo ni *transformer* na *machine* ya kusukuma maji.

Je, Mhe. Waziri ni lini tatizo hilo litatatuliwa kwa wananchi wa Chaani Kubwa?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 129 kama ifuatavyo:-

Wizara yangu imeshakamilisha hatua za awali za uchimbaji wa kisima, ulazaji wa mabomba na ujenzi wa kituo. Kwa hivyo, hivi sasa ipo katika hatua za kuvuta umeme katika *transformer* iliyokaribu na kisima hicho pamoja na ununuzi wa *pump* na mara tu kazi hizo zitakapokamilika, wananchi wa Shehia ya Chaani Kubwa watafaidika na huduma ya maji safi na salama kupitia mradi huo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: ahsante sana Mhe. Spika, hivi Mhe. Waziri atakubaliana na mimi katika manunuzi ya *pump* inachuku muda mrefu sana hati kufika miezi mitatu. Je, ni sababu zipi zinazopelekea kukwama wananchi kupata *pump* hizo?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, ununuzi wa *pump* inategemea pale ambapo tutakapoziagizishia, kwa sababu zipo Dar-es-Salaam, lakini hizi haziko makini kwa sababu zinakuwa ni *used*. Kutokana na kuwa tunaziagizishia nje, basi mara nyingi sana zinakuwa zinachelewa.

Kwa hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi wastahamili, kwa sababu lengo letu ni kuwapatia wananchi maji safi na salama. Kwa maana hiyo, wastahamili na zitakapofika tu pump hizo basi tutajitahidi kuzifunga kwenye visima vyao. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Spika, katika swali la msingi alilouliza Mhe. Ussi Jecha Simai ni kwamba Chaani Kubwa imeshachimba kisima na mabomba yameshalazwa na kila kitu kipo, lakini tatizo kubwa ni *transformer*.

Je, Mhe. Spika, ni lini hasa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati itakuwa na *transformer* za *spare*, ili wakati kinapoharibika chombo au *transformer* iwe tayari inawekwa na wananchi waweze kufaidika na hayo maji. Kwa kweli kuharibika *transformer* na ikawa hakuna *transformer* ni tatizo. Sasa ni lini wizara yake itakuwa na *transformer* za akiba, ili pale linapotokea tatizo liweze kurekebisha kwa haraka?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza kuhusu kisima cha Chaani *transformer* ipo ambayo wanaitumia wananchi na inao uwezo wa kutumia wananchi pamoja na kisima hicho. Kwa hivyo, kwa sasa tutatoa line kutoka kwenye *transformer* hiyo iliyopokaribu na kisima hicho, ili wananchi wafaidike na maji safi na salama. *(Makofi)*

Kuhusu *transformer* za akiba hili nalo shirika langu kwa kweli linajitahidi kutafuta *transformer* hizo na si kwa matumizi ya visima vya maji mpaka katika matumizi ya kawaida. Kwa hivyo, tutajitahidi na Mwenyezi Mungu akitujaalia na tutakapopata uwezo, basi tutatafuta *transformer* za akiba, ili pale popote linapotokea tatizo basi tuweze kudhibiti hali hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna shehia ambazo zina visima vinne vya maji, lakini *pump* moja tu ndiyo inayosukuma maji. Je, Mhe. Waziri kuna jitihada gani za kuwasaidia wananchi hao kwa visima vyengine, ili inapoharibika *pump* hiyo nyengine iwepo?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, ni kweli kuna baadhi ya sehemu kuna visima vinne, lakini kila kisima kina pump moja. Sasa utaratibu wetu wa Mamlaka ya Maji, basi pale inapoharibika *pump* huwa tunafuatilia wenyewe na tunaitoa *pump* hiyo kisimani kwa kuifanyia matengenezo na kama itashindikana katika matengenezo basi tunafunga pamp mpya, kwa sababu kama nilivyozungumza kwamba nia ya Wizara yangu na serikali kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama.

Nam. 141

Skuli ya Sizini Kujengwa Eneo la Raia

Mhe. Rufai Said Rufai - Aliuliza:

Skuli ya Sizini ambayo ilifunguliwa mwaka 1993 imejengwa katika shamba ambalo sio eneo la Serikali. Tokea mwaka huo hadi hivi sasa wamiliki wa eneo hilo wanafuatilia angala kupata fidia ya shamba lao kutoka Serikalini.

(a) Je, Wizara yako inalifahamu tatizo hilo.

(b) Kama inalifahamu ina mpango gani wa kuwalipa fidia wamiliki hao.

(c) Kwa kuwa muda umekuwa mrefu sana huoni kwamba huko ni kuwakatisha tama wenye shamba hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 141 lenye sehemu (a) na (b na (c) kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:

Ni kweli kuwa Skuli ya Sizini ilifunguliwa mwaka 1993 na imejengwa kwa pamoja na wananchi wa Seriklai ya Mapinduzi ya Zanzibar katika eneo ambalo halikuwa eneo la Serikali. Eneo hilo lilitolewa familia mbili tofauti kwa madhumuni ya kujengwa skuli. Mmoja wa mwananchi alietoa shamba hilo hivi sasa ameshafariki na baada ya kufariki kwake, mrithi wake alileta madai ya kulipwa fidia. Jambo ambalo halikuwepo hapo mwanzo kwa vile eneo hili lilitolewa na wananchi wenyewe mmoja wa waenyeji wa eneo hilo alijitolea kulipa fidia ya ardhi, femilia ya wanaodai kwa kuwapa eneo la ardhi sehemu ya Tumbe lakini wahusika hawakukubali kulipwa shamba katika eneo jengine

Baada ya maelezo hayo, naomba kujibu kama hivi ifuatavyo:-

a) Wizara inalifahamu tatizo hilo.

Wizara haina ardhi ya kuweza kulipa fidia ya wanaodai, hata hivyo Mhe. Spika, niko tayari kuyazingatia madai yao na itakaa pamoja kwa kutafuta njia ya kutatua tatizo hili, kama nilivyotangulia kusema Mhe. Spika, Wizara itakaa pamoja na wahusika na kutafuta njia ya kulitatua tatizo hilo.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, sikuridhika vizuri na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, nina suala moja la nyongeza lenye kifungu a, b na c.

a) Je, Wizara inayo hati yoyote ile iliyoonyesha kuwa mzee huyo alitoa shamba hiyo.

b) Ikiwa Wizara haina hati yoyote ile yenye kuonyesha kwamba imepewa shamba hilo, je huoni kwamba shamba hiyo imeporwa na wenyewe ndio wakaja juu.

c) Kwa kuwa haya yote sio je, huoni kuwa ipo haja baina ya mimi Muwakilishi wa eneo hilo na wizara pamoja na hao wazee kukaa pamoja kutatua tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, sitamjibu swali lake la moja kwa moja isipokuwa nitazungumza maneno ambayo ndani yake ndio limo hilo jibu la suala lake.

Mhe. Spika, napenda kuwaomba waheshimiwa Wawakilishi wote kijiji chochote kinapotaka kuanzisha skuli ni vizuri wanapopachagua mahala waelewane na yule mwenye shamba sehemu ile pale, na sio yeye tu lakini waandikiane kwa sababu watakapoandikiana baadae kuna warathi watakuja kudai kama inavyotokea sasa hivi Sizini, kwa sababu Wizara ya Elimu wanapokuwa wanakijiji wanataka kuanzisha skuli wao ndio huwa wanachukua hiyo *initiative* na kutafuta pahala na kuwaita maafisa wangu wakapime, bahati mbaya yule mzee anayekuwepo wakati ule anakuwa anakubali kutoa lakini wanawe wanakuja kudai urithi wao baadae na linatokea hili tatizo ambalo Mhe. Rufai ameliuliza kwamba hawakuandikiana kwa sababu walishakubaliana pale kijijini.

Kwa hivyo naweza kumjibu moja kwa moja kuwa hawakuandikiana hawa na hivyo itabidi sisi lazima tukae kitako tuzungumze sasa hivi na hii femilia tujue itachukua hatua gani baadae. Ahsante sana

Mhe. Salehe Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja dogo sana la nyongeza.

Kwa kuwa haki ikichelewa kutolewa ni sawa kwamba haikutolewa kabisa, na kwa kuwa sasa hivi kuna matatizo ya ardhi katika sehemu kadhaa zikiwemo za ukanda wa bahari na sasa hivi ndio tunakuja katika ardhi za makaazi. Je, kuendeleza ujenzi wa skuli hiyo bila ya kufanya makubaliano na wanaomiliki ardhi si kwenda kinyume na haki za binaadamu na utawala bora moja.

Pili kwa kuwa Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964 ilikuwa eka tatu tatu za ardhi kwa wananchi wanyonge, Je, kuendelea kumega ardhi ya wananchi kwa kujenga mambo ya shule na maandalizi mengine ya serikali si kwenda kinyume na dhamira halisi ya Mapinduzi ya mwaka 1964.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mheshimiwa anazungumzia suala la kwenda kinyume na haki za binaadamu, lakini pia tutizame ari na hamu za wananchi katika kijiji wanavyoitaka skuli ni sawa sawa na vile vile unapokitaka kituo cha afya, ukweli huwa wanataka skuli ijengewe haalan na wanapotaka skuli ijengwe halan huwa wao hawajakubaliana na yule mwenye shamba, lakini wakati ule wa makubaliano baina ya yule mzee na wanakijiji wameshaelewana vizuri pale na skuli inakuwa tayari kuanzishwa na chereko chereko zinakuwepo pale.

Kama hivi sasa tayari mimi nimeshapata maombi kuna skuli natakiwa nikaiezeke, sasa hapo ilipojengwa itabidi tuanze kuuliza mlikubaliana na huyu mwenye shamba kwa sababu skuli imeshajengwa na imeshafika katika kuezeka na tuntaka tukaezeke, sasa hili ndio tatizo hatwendi kinyume na haki za

binaadam lakini tunafuata hamu za wananchi wanapoitaka skuli kwa nguvu zote pale pahala.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nashukuru na mimi kupata kuuliza suala moja la nyongeza kama ifutavyo.

Kwanza nitoe shukurani kwa majibu mazuri kabisa ya kitaalam yaliyotolewa na Mhe. Waziri, lakini Mhe. Spika, kuna maeneo ni kweli unaweza kuzungumza na wanaohusika ile hali ya kujenga ikawa haina matatizo, lakini kuna sehemu lazima ipatikane kitu kama hicho cha skuli ambayo ni maendeleo ya lazima kwa nchi hii, kwa sababu bila ya elimu hakuna maendeleo bila ya elimu hakuna uongozi. Lakini kwa bahati mbaya hapakupatikana eneo la bure ambalo wazee wanaweza kujitolea ili kuweza kujengwa skuli hiyo.

Mhe. Waziri si ungefuata mpango kama ule wa zamani wa kukubaliana na wananchi wanaofika katika eneo lile kwa muhimu wa sekta yenyewe ya elimu na wakapewa malipo, pamoja na kupeana stakabadhi zinazohusika ili skuli iendelee kwa maslahi ya taifa hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nataka nikubaliane na yeye na hata hii skuli ya Sizini hatukuvamia wala hatukupora kama ambavyo tuliulizwa awali, tulikubaliana na wenyeji akiwemo Mwakilishi na Mbunge na wakatuambia kama tayari tumekubaliana kwamba tayari tumekubalina na wanakijiji kujengwa skuli hii.

Kwa hivyo, tumejenga tokea mwaka 1993 na wanafunzi wamo, hivi karibuni ndio yametokea haya matatizo. Kwa hiyo, popote pale ambapo tunahitaji kujenga Mhe. Spika, tunakubaliana na wenyewe kwanza wakiwemo Wawakilishi, Wabunge, Masheha wote tunakaa pamoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunajua kuwa ushahidi wa mali isiyohamishika basi ni kuwa na waraka. Sasa kwa kuwa waraka katika skuli hii hatuna, basi tutahakikisha kwamba tunakaa na wenye mali hii, kwa ajili ya kufanya suluhu pamoja na skuli nyengine yoyote ambayo itatokea matatizo kama haya. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

a) Lini tutegemee utafiti huo utafanywa.
b) Utamaduni wetu na dini yetu inatukataza pombe lakini kwa mshangao mkubwa hivi juzi katika tamasha la ZIFF mdhamini mkubwa ilikuwa kampuni ya pombe, sababu gani zilizotupelekea

kudhamini hivyo hujui kama hili ni jukumu letu mimi na wewe kupiga vita hili.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Kwa kweli tulisema kwamba haturuhusu taasisi zote ambazo zinahusiana na vileo au pombe kudhamini michezo yetu na tumetoa fursa hiyo kwa taasisi nyingi tu ili zijitokeze kudhamini michezo yetu zile ambazo hazihusiani na vileo, zaidi tulizuia kule uwanja wa Amaan waliomba na tukakataa tuliwaambia uzeni sehemu nyengine yoyote lakini Amani kwa sababu tumekuwa na utamaduni wa taasisi nyingi kuzikatalia.

Kwa hivyo mpaka sasa tumesema kwamba hatudhamini au hatutoi fursa kwa taasisi yoyote ambayo inahusiana na masuala ya ulevi kudhamini michezo yetu.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri suala moja la nyongeza.

Katika jibu lake la msingi alilokuwa akijibu yote aliyoyaeleza ukiwacha wazazi ni mambo ambayo yako katika wizara yake, magazeti ni mambo ya habari, utamaduni uko katika wizara yake, redio Tv na vyengine vyote na hivyo vyote ndio sababu ya mambo yote haya.

Je, serikali ina mpango gani wa kudhibiti mambo haya?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Ni kweli vyombo vyote vimo ndani ya taasisi yangu lakini kwa upande wetu tunajitahidi kuhakikisha kwamba Televisheni, Redio pamoja na Magazeti kuhakikisha kwamba vinajaribu kuelimisha jamii kuhusiana na suala zima la mila na utamaduni wa Mzanzibari, hatua ambazo tumezichukua kwa kweli hivi sasa tumejaribu katika kila kituo kuweka watu, vile vile kama vile Air port, Bandarini vile vile kwa ajili ya watalii ili watakapokuja waanze kutoa elimu na tunajaribu vile vile kuingiza katika *website* kuhakikisha kwamba wageni wanapokuja waelewe kwamba anatakiwa kuvaa vipi.

Lakini vile vile kwa upande wa magazeti tumejaribu kukaa na watu wetu wa magazeti ili kuwafahamisha jinsi ya kulinda utamaduni wetu na tutajitahidi kwa sababu hili ni suala zito kidogo na la muda mrefu lakini tutajitahidi kidogo kidogo na nina hakika baada ya muda mfupi basi mtaona mabadiliko katika magazeti, yale magazeti ambayo tunaona hayana maadili tutayazuia na vile vile vipindi tutahakikisha kwamba ni vipindi vya maadili, wasiweze kuonyesha filamu ambazo hazifai.

Kwa ufupi tunajitahidi na hilo suala naamini katika muda mfupi basi kutakuwa na mabadiliko makubwa sana. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kumuuliza Mhe. Waziri suali la nyongeza lenye vifungu a,b.

Imekuwa ni mazoea kwa mahoteli mbali mbali hapa Zanzibar kuweka siku maalum ya Swahili day hasa kwa kuonyesha wageni mbali mbali, siku hiyo chakula na hata burudani huwa za Kiswahili yaani za Kizanzibari, huchukuliwa watoto wa Kizanzibari hasa wanawake kuchezeshwa ngoma mbele ya wageni.

a) Je, huu ni utaratibu wa Kizanzibari?
b) Leo wametualika siku ya utamaduni wa ndugu zetu wa Oman Zaznibar inategemea kujifunza nini ?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Kama nilivyotangaza jana kwamba leo tutakuwa na tamasha la ndugu zetu wa Oman na lengo na madhumini ni kuja kujifunza, sababu tukitaka tusitake tunalingana kiutamaduni na Oman. Kwa hivyo imani yangu kwamba tutajifunza mengi na katika hao vile vile wamo wanawake na wao watacheza, kwa hivyo utamaduni haujamkataza kwamba manamke asicheze isipokuwa acheze katika hali ya kujistiri, asicheze uchi kwa sababu utamaduni unaweza kuonyesha ata kivazi hata wa kucheza na wao wataonyesha wa kucheza vile vile lakini watakuwa wamevaa vizuri tu.

Kwa hivyo isiwe ni *issue* kubwa itachezwa lakini kwa maadili michezo ambayo ni ya heshima, kwa hivyo nawahakikishia waheshimiwa wajumbe wote kwamba leo saa 8.00 tutakuwa na tamasha la Oman na tumechanganya Oman na Zanzibar, wakimaliza Oman tunaingia Zanzibar halafu mtaangalia namna gani tunavyotunza maadili na utamaduni wetu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2011
Wizara ya Miundo Mbinu na Mawasiliano

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe majadiliano yanaendelea nina maombi thalathini (30) hivi sasa wote hawa wana nia nzuri ya kutaka kumsaidia Mhe. Waziri, ndio anavyoomba hivi na mimi niwaombe munisaidie, tupange *point* zetu vizuri twende kwenye hoja moja kwa moja ili tutumie muda mfupi kuweza kuruhusu waheshimiwa wengi zaidi walioomba kuwapa nafasi ya kumsaidia

Mhe. Waziri, naomba sana waheshimiwa wajumbe ili tuweze kufanikisha shughuli zetu nyinyi ndio wa kunisaidia mimi na wenzangu wanaonisaidia kuendesha kikao hiki.

Nawashukuru sana waheshimiwa wajumbe.

Mhe. Mbarouk Mussa Wadi: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya mwanzo kabisa kuwa mchangiaji wa mwanzo katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri na timu yake ya watendaji yote katika Wizara yake kwa kutayarisha hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2011/2012 yenye muono mpana kabisa na maslahi kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi nianze mchango wangu kwenye ukurasa wa 11 hapa kwenye Idara ya Uendeshaji na Uatumishi, katika kitabu hiki Wizara ya Miundombinu inasema kupitia muongozo wa serikali inakusudia kujenga jengo jipya la Afisi katika kiwanja kilichopo Mazizini, Wizara hii hii kwenye bajeti ya mwaka 2009/2010 iliomba pesa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Afisi kuu ya Wizara eneo la Mtoni na waliomba Shs. 100,000,000 wakapewa Shs. 49.1 milioni kwa ajili ya ujenzi ule, sasa na leo anaomba ujenzi mwengine huu Mazizini sijui ule wa mwanzo umefikia wapi. Ningemuomba Mhe. Waziri aje atupe maelezo ya pesa zile alizoomba mwaka ule amejenga amefikia wapi kiasi cha kusema anajenga jengo jengine hili litakuwa la pili la Makao makuu ya Wizara, sasa hili la mwanzo aje kutwambia amefikia wapi ujenzi wake ndipo anaomba hili la pili kama lile lilikuwa dogo kama nimemfahamu vizuri lile ni dogo na anataka kujenga kubwa zaidi la pili. Sasa aje kutupa maelezo kwanza kuhusiana na hili la mwanzo kabla ya kuomba hili la pili la Mazizini.

Kwa hivyo Mhe. Waziri utakapokuja hapa hebu tupe maelezo yanayokidhi haja ili tuweze kukuidhinishia matumizi ya pesa hizi nyengine unazoziomba, hatuwezi tukakupa pesa nyengine bila ya hizi kwanza kuzijua matumizi yake na umefikia wapi, kwa sababu ulituomba unajenga makao makuu ya Wizara.

Nikitoka hapo kama ulivyotuahidi Mhe. Spika, twende kwenye *point* haraka haraka ili tuweze kuenea wote, sasa ninakwenda kwenye ukurasa wa 12 tu hapo kwenye Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara, Mhe. Waziri hapa katika kitabu chake ametuonyesha mambo mazuri kabisa ya barabara zinazojengwa, zilizokwisha kujengwa na zinazotarajiwa kujengwa. Mimi nilikuwa na mbili tatu hapa kidogo niziulizie, kuna barabara hii Mahonda, Kinyasini, Mkokotoni sijaisikia hapa na barabara ile kwa kweli imeshachoka kwa sababu hata ujenzi wake ulikuwa haukukamilika hapo ilipojengwa na hao wafadhili iliachwe,

ilijengwa kwenye leya moja tu haikuendelezwa tena. Ndio maana kila baada ya miezi miwili au mitatu barabara ile inakuwa mashimo matupu.

Mhe. Waziri kama sasa hivi atapita huko barabara hii ataiona namna gani ilivyokuwa imejaa mashimo kwa hivyo hata wale watengenezaji wa barabara wale ambao wanafukia fukia mashimo, kila siku wanakuwa kazini wakifika mwisho mwanzo kumeshatoboka sasa hemu namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze kidogo juu ya ujenzi wa barabara hii vipi ujenzi wake utakuwa kwa sababu sikuusikia lakini ni baarabara moja kubwa sana sikuisikia hii.

Sasa moende kwenye barabara ya Amani Mtoni kaitaja humu Mhe. Waziri lakini hakuiombea pesa humu sijui ujenzi wake humu unakwenda je pesa zake ziko wapi na itakamilika lini nilikuwa nataka kujua hilo.

Baada ya hapo nisogee barabara za ndani za jimbo langu la Mkwajuni *fidel road* niliwahi kuuliza suali langu la msingi hapa nikapata jawabu zuri tu kwa Mhe. Naibu Waziri, na akaniahidi kuja kutembelea barabara hizi na kwa kweli nimpongeze Mhe. Naibu Waziri alikuja kweli kwenye jimbo langu akatembelea barabara hizi yeye na wataalam wake tukazikagua zote, akaniahidi kwamba wanarudi kwenda kulishughulikia suala hili. Lakini bado sijapata majibu kwenye suala hili, kwa sababu walinambia wanafanya tasmini sasa sijui hiyo tasmini imefikia wapi. Naomba Mhe. Waziori utakapokuja uniambie tathmini uliyofanya mmefikia wapi juu ya barabara hizi za Mkwajuni na uwezekano wa kuzisaidia angalau japo kifusi tu uko je. Naomba hilo uje kunieleza.

Mhe. Spika, jengine nije kwenye utanuzi wa uwanja wa mpira wa timu yangu ya Banyamulenge ya Potowa pale ilipokuwa inajengwa barabara ya Mkwajuni/Nungwi ilipita katika uwanja huu, wizara ilikubaliana na timu ya mpira pale kwamba tunapitisha barabara lakini nyinyi tunakupitisheni pembeni kweli Wizara ilifanya jitihada hizo ilinunua eneo hilo la pembembeni kusogeza wale, lakini makubaliano hayakufikiwa ili kutengeneza uwanja wa kuchezewa pale. Lakini mlikubalina kutengeneza kwa kupiga *bulldozer* ili uweze kuwa uwanja wa mpira na uweze kuchezewa, lakini hadi hii leo haujatengenezwa ule Uwanja wa Mpira, kwa hivyo vijana wale wanakosa eneo la kuchezea mpira.

Mhe. Spika, suala hili nimeshalifuatilia nimekuja wizarani kwako nimeshaonana na Mhe. Waziri, nimeonana na Katibu Mkuu mara nyingi lakini bado napigwa dane dane kwenye suala hili, kwa hivyo Mhe. Waziri hoja yangu hii kama hukuniletea majibu mazuri fungu lako hili la Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa barabara nina azma ya kulizuia hapa mpaka unipe maelezo ya kuridhisha juu ya utanuzi wa uwanja huo. Nisogee tena kidogo nije mjini sasa hapa.

Mhe. Spika, kama unavyofahamu kuna njia pale ya Forodhani kwenye jengo lililokuwa la kulelea watoto yatima zamani, sasa hivi halilei tena. Njia ile imezibwa chini ya nyumba, zamani tukipitia upande wa pili ili mtu utokezee Forodhani , njia ile imefungwa. Mwanzo tulifikiri labda imefungwa kwa ujenzi wa Forodhani, lakini naona mpaka hii leo ndio haijafunguliwa tena. Matokeo yake sasa kuna viti pale watu wanapata murdi kidogo kidogo. Njia hii inaleta usumbufu mkubwa sana kwa wananchi.

Mhe. Waziri hebu tueleze maudhui ya kuifunga njia ile. Maana nahisi kama umemtengenezea mtu mmoja labda mwenye ile *Restaurant* ili aweze kutoa viti vyake nje. Lakini unatuudhi wengi ambao tunataka kupita pale. Hii serikali ni ya wananchi, wanalalamika juu ya tatizo lile. Tunaomba tueleze kiini hasa cha kufungwa njia ile hasa ni nini. Kiasi cha kwamba inafika wakati gari zinapishana kupenya katika lile tundu na hasiwezi kupenya mbili mnakaa pale zaidi ya dakika 10 au 20 madereva wanabishana tu, huyu hataki kurudi nyuma na huyu hataki kurudi nyuma.

Mhe. Spika, niondoke hapo nisogee kidogo kwenye Idara ya Usafiri na Leseni kwenye ukurasa wa 21. Idara hii ukiitizama unaiyona ndogo sana lakini kwa kweli ina mchango mkubwa sana katika taifa letu. Idara hii ndio inayoruhusu madereva kuendesha gari katika nchi yetu. Lakini kumekuwa na matatizo mengi na malalamiko mengi kwa wananchi hasa juu ya madereva wa daladala, ni kero kubwa sana kwa madereva wengine na wananchi kwa ujumla.

Mhe. Spika, naomba utakapokuja hapa Mhe. Waziri hebu atueleze mkakati wake hasa wa kuwarekebisha tabia kuanzia madereva mpaka makonda. Maana inakuwa ni kero kwa watu wazima wanaopanda gari hizi na kwa vijana wetu wanaosoma skuli ni tatizo kubwa, wanawasumbua mno. Utaratibu unapangwa lakini kuufuata ni vigumu.

Idara yako hii inaendelea kuwapa leseni watu ambao hawana tabia nzuri. Ningeomba kukawa na utaratibu mzuri wa kuhakikisha utoaji wako wa lesseni unazingatia utaratibu mzuri na hasa kuangalia mila na desturi zetu. Unamkuta dereva au utingo hata nguo hana mle kwenye gari anawapakia watu. Nidhamu pia hana. Hebu tuambieni ni hatua gani mnazochukua za watu wa aina hii. Naomba utakapokuja kutoa majumuisho yako utupe tathmini au tupe takwimu ya wale ambao uliwachukulia hatua kwa tabia kama hizi hasa hawa wa daladala. Kwa kweli imekuwa kelele mno kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, nende kwenye Sekta ya Usafiri wa Anga ukurasa wa 23 nasogea mbele kidogo ukurasa namba 24 kuna Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Tuliwahi kufika na Kamati ya PAC tukakutana na uwongozi, tukazungumza mengi na tukakagua maeneo mengi. Moja katika maeneo ambayo tulizunguka

ni ujenzi wa uzio wa Uwanja wa Ndege. Tulipokuwa tunakaguzwa na Mkurugenzi wa Idara hii pamoja na Meneja wake au sijui Msaidizi Meneja wa Uwanja, tulifika mahala hapajajengwe halafu huku mbele pameendelea kujengwa. Tukauliza mbona hapa pameachwa na ng'ombe hawa wamo ndani ya uwanja. Tukaambiwa kwamba mtu mwenye nyumba hii hapa ni mtu wa asili pale, lakini hajalipwa fidia. Ndio maana wajenzi wameshindwa kujenga kwa sababu hatuwezi kumvunjia. Na ndio maana hata ng'ombe wake anafunga hapa kwa sababu anasema kwamba hili eneo ni la kwake. Mpaka hapo atakapolipwa fidia eneo lile ndio litakuwa limetoka kwenye milki yake ataruhusu mambo yale yaendelee na ujenzi.

Chakushangaza, tulikuja na suala la msingi hapa tukauliza kwenye jambo hili. Majibu tuliyopewa na Mhe. Naibu Waziri hapa ni kwamba hakuna mtu ambaye anadai fidia pale au hakuna pahala ambapo pamezuiwa kujengwa kwa sababu mtu hajalipwa fidia. Mhe. Spika, kitendo hiki mimi naona hatujui ukweli ni upi kati ya Mhe. Naibu Waziri au Mkurugenzi wa Anga na Wasaidizi wake ambao walitukaguza pale. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja atupe ufafanuzi juu ya suala hili. Nani ametwambia uongo katika hili. Maana huyu anasema hajalipwa lakini Mhe. Naibu Waziri anasema hakuna mtu ambaye hajalipwa. Tunaomba utueleze nani ambaye anasema ukweli katika hili.

Tulivyotoka hapo tukazunguka zunguka tukakuta kuna jenereta kubwa sana limenunuliwa kwa ajili ya matumizi ya Uwanja wa Ndege. Tulipoulizia tukaambiwa jenereta lile lina zaidi ya miezi 9 tangu kuwekwa pale lakini halijaunganishwa. Jenereta lile limeletwa na Wizara ya Fedha. Tumewauliza nyinyi mna matatizo wakati mwengine ya mambo ya umeme na jenereta lipo lina mwezi wa 9, limeletwa pale jipya na gerentii yake ni mwaka mmoja. Kwa maelezo ambayo tumepewa pale gerentii yake inamalizika miezi mitatu itakayokuja mbele. Kwa sasa hivi nafikiri imebakia labda mwezi mmoja.

Sasa tukataka kujua hili jenereta mpaka hii leo halijaungwa gerentii inamalizika keshokutwa, litakapokuja kuungwa kama halifai pesa hizi ambazo zimenunulia jenereta si itakuwa zimekwenda ovyo. Tumepata shaka hizi pesa za wananchi zimeshanunuliwa hili jenereta hawa watu wa anga hawajaweza kulifunga tatizo ni kitu gani. Wakatueleza hapa tatizo sio sisi, hili walilolileta ni Wizara ya Fedha na ufungaji wa hili jambo linakaribia milioni 20 sijui sina uhakika vizuri. Lakini walikuwa wanawalalamikia watu wa Wizara ya Fedha kwamba wao ndio wenye wajibu wa kulifunga lile. Wameshawaomba sana fedha kwa ajili ya ufungaji wa lile jenereta na wameshapeleka mpaka tathmini yao.
Mhe. Waziri wa Fedha, nafikiri mweyewe yupo hapa atakuwa na majibu mazuri katika hili ili kumsaidia Waziri wa Miundombinu atuambie lini jenereta lile watalifunga kwa sababu gerentii yake sifikirii kama imebakia basi labda mwezi mmoja. Litakapofungwa halafu likawa halifanyi kazi hatuwezi

kulirejesha kwa yule aliyetuuzia kwa sababu gerentii imeshaisha. Kila kitu kinavyouzwa kinauzwa kwa utaratibu maalum. Sasa litakapokuwa halikufaa pesa hizi zilizotolewa zaidi ya milioni 300 kununua jenereta lile, si itakuwa pesa zimetumika ovyo tu. Watu wamekaa wanazitizama zinakufa. Mtu kama chake angelikubali.

Mhe. Spika, mimi nahisi ni uzembe huu wa hali ya juu. Hana uchungu mtu kabisa na ile mali ya serikali, anaona kama ni mali ya mjinga tu hivi. Maana kama pesa ile ni yak wake asingekubali mtu kuacha kitu namna kama ile kikaa tu kinaharibika. Hili Mhe. Waziri utakapokuja hebu kaa na Waziri wa Fedha mlizungumze ili mje mtuletee jawali lililokuwa linaridhisha kabisa. Vyenginevyo na mimi hapa kwenye Idara yako ya Anga naanzia hapa.

Tukazunguka zunguka kwenye uwanja ule ule, tukakuta kuna jengo la *Pharmacy* limejengwa ndani ya eneo la Uwanja wa Ndege. Tukauliza mbona mmempa ardhi hii ya uwanja wa ndege huyu mtu humu. Jawabu lake sikulipata vizuri. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri utakapokuja hetu tupe sababu za msingi za kuijenga ile Pharmacy mkampa eneo la Uwanja wa Ndege maana kavuja ukuta kabisa, uzio wa Uwanja wa Ndege umevunjwa kwa ajili ya kuweka *pharmacy*. Sijui umuhimu wake ni upi sana kiasi kwamba *pharmacy* ile ijengwe pale, badala ya kumtafutia eneo kama walivyowakatia wengine mle ndani. Maana mle ndani ukiingia mmekatwa vikataa mle utafikiri mtu anataka kurithisha. Kila mtu anapewa nafasi, madhali wewe hivi, unapewa.

Mhe. Spika, mimi nauliza jamani huu Uwanja wa Ndege, hapa katika kueleza Mhe. Waziri kwenye kitabu chake anasema kumekuwepo na ongezeko la idadi ya ndege na abiria. Yaani wanaongezeka abiria kila siku. Lakini utakuta nafasi ni chache ya wale abiria wenyewe wanaokusudiwa kwenye ule uwanja kukaa. Matokeo yake nafasi zote wanapewa watu kufanya biashara mle ndani. Mimi nataka kujiuliza imekuwa ndio Juakali au vipi. Pale kilichokusudiwa ni abiria wanaosafiri zaidi ndio wanaochukua muda kukaa pale kulika wanaoteremka.

Mhe. Spika, sasa lile eneo la kukaa abiria lote limekatwa patisheni wamepewa watu kufanyia biashara. Maana pale mtu wa mwisho, mtalii kaja na pesa yake imebakia ananunua kizawadi pale anaimalizia ile pesa anaondoka. Lakini huyu anauza vinyago, huyu hapa na yeye anauza vinyago, huyu anauza chai, huyu hapa na yeye anauza chai. Aiterm moja zina maduka manne au matatu yote ya kazi gani haya. Ukiuliza hakuna jawabu zuri. Sasa nakuomba sana Mhe. Waziri hebu utakapokuja tupe maelekezo mazuri juu ya suala hili. Maana tunajaribu kulikemea lakini inaonekana wakubwa wa kiwanja pale wazito kutekeleza maagizo ya Kamati hasa kamati zinapokwenda. Mhe. Waziri utakapokuja hapa ili tukusaidie haya matumizi yako katika Idara hiyo hebu tupe maelezo ya kutosha kidogo.

Mhe. Spika, nije kwenye shirika la Bandari. Mhe. Waziri ameeleza hapa kwenye kitabu chake juu ya matengenezo ya Meli ya LCT Jitihada. Kwenye ukurasa wa 31 hakuwa ameeleza gharama za matengenezo yale labda, Kampuni iliyotengeneza, hakueleza humu. Nilikuwa naomba atakapokuja atupe maelezo ya gharama zilizotumika hizi za matengenezo ya meli hii na Kampuni iliyopewa kazi ile ya matengenezo. Kwenye magazeti tunasikia sijui 2.6 bilion. Sina uhakika, sasa naomba Mhe. Waziri atakapokuja atupe la uhakika kidogo.

Halafu nije kwenye ununuzi wa Tishali la kuegesha vyombo vya abiria. Nalo vile vile limeelezwa lakini halina maelezo mazuri ya kuwa limenunuliwa wapi, gerentii yake miaka mingapi, kiasi gani cha fedha kimetumika. Mhe. Waziri utakapokuja hebu tueleze.

Mhe. Spika, nimalizie kwenye sekta ya usafiri ya watu binafsi alisema kuna sekta binafsi zinasaidia katika usafiri. Mimi nakubaliana na yeye Mhe. Waziri, lakini kumekuwa kuna tatizo. Wasafirishaji pale wamekuwa kama ndio wenye mamlaka katika bandari ile. Kwanza unaweza ukaambiwa mtasafiri saa 9:30 jioni mnatakiwa mfike saa 9:00, lakini mtafika saa 10:45 hamjaondoka pale na huna wa kumuuliza. Ukiwauliza wakali kama moto. Lakini wakati huo huo mnaondoka hapa mnaambiwa mtachukua masaa mawili matokeo yake mnachukua zaidi ya masaa matatu. Maana yake kuonesha zile meli nyengine zimechoka sasa.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri hizi meli wanazikagua, na wewe mwenyewe Mhe. Waziri umewahi kusafiri na meli hizi. Maana nyengine vile vyoo vyake haviendeki. Huwezi ukawachukua abiria pale vyoo vichafu kabisa. Hawa wakaguzi wenu wa shirika au wa Idara yako hii wako wapi, wanafanya kazi gani. Tunasafiri na meli zikiwa chafu.

Mhe. Spika, pia kuna kadhia ya watu waowasumbua pale bandarini. Tiketi imeandikwa mwisho kuchukua kilo 45 lakini ukienda na kiboksi cha kilo 10 anataka ukilipie. Anakwambia kwamba mzigo wa kilo 45 wa mkononi na hichi kiboksi cha kilo 10 nabeba mkononi, kwa nini nikilipie? Wanadai lazima ulipe. Mimi mwenyewe nimeshafanyiwa hayo na ushahidi ninao. Nililalamika na nikawambia mimi silipi kwa sababu mmesema kila 45 tiketi yako hii ndivyo inavyosema. Akasema hii tulikusudia begi. Sasa kama hivyo hukuandika humu kama ni begi. Kwa hivyo hata kama nakuja na boksi likiwa halijatimia kilo 45, maana yake nichukue tu. Ingawa hawazipimi wanakisia tu. Hili nalo ni tatizo. Naomba Mhe. Waziri utusaidie hili ili kuondosha usumbufu unaopatikana pale.

Mhe. Spika, nije kwenye jengo la kuondokea abiria. Jengo kwa kweli ni dogo halitoshi. Abiria wanaosafiri pale ni wengi mno. Ningekuomba sana Mhe.

Waziri mkafanya marekebisho kukawa na jengo la kuondokea abiria. Pia pawe na jengo la VIP kama bandari nyengine. Ukenda Dar-es-Salaam lipo eneo la VIP pale wanapita Waheshimiwa wanakwenda kupumzika halafu wakati wa safari wanaondoka. Hebu ukija Mhe. Waziri utueleze lini utaondosha kadhia hii ya kuwa na jengo la VIP katika bandari yako ya Unguja.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, mimi bajeti hii kwanza siiyungi mkono naweka asilimia 50. nyengine 50 nakaa nazo mfukono mpaka atakapokuwa Mhe. Waziri amenipa majibu ya kuridhisha katika hoja zangu hizi, naweza nikazirejesha. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Naomba kwanza nitoe muongozo kuhusu wageni. Kwa kawaida na tunapenda tuwe tunapata wageni mbali mbali kuja kuona shughuli zetu tunavyoziendesha. Lakini nadhani ingekuwa inafaa tukapata taarifa hizi mapema na wale wageni wakahakikisha kwamba wapo pale juu saa 3:00 ili mara baada ya anaeendesha kikao hiki kukalia kitu basi kazi ya kwanza pengine aifanye kazi hiyo.

Inapokuja taarifa ya wageni wakati tupo kwenye mtiririko wa michango kwa kweli haileti utaratibu mzuri katika kuendelea na ile michango yenyewe. Kwa hivyo iwaombe wote wageni wetu wanaotaka kuja hapa watoe taarifa mapema na kitengo chetu cha uhusiano iwape taarifa mapema kwamba wafike mapema ili waweze kutambuliwa mapema na kusalimiana na Wajumbe kabla hatujaanza shughuli nyengine. Ili tupate mtiririko wa moja kwa moja wa shughuli zetu.

Leo Waheshimiwa Wajumbe tumepokea wageni ambao ni kundi la wanafunzi kutoka Chuo cha Chukwani ambao juzi tulipata kundi moja na leo ni kundi la pili. Naomba niwatambulishe vijana wetu wamekuja hapa kuona shughuli zetu ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Chukwani. Naomba wasimame. (*Makofi*).

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai na uzima na kutuwezesha kwa mara nyengine tena kushiriki vikao vyako vya Baraza lako tukufu na kutoa mchango huo kwa ajili ya kusaidia kuiendeleza nchi yetu na watu wake.

Mhe. Spika, pili nikushukuru na wewe kwa kunipatia nafasi hii, kuichangia bajeti hii ya Wizara muhimu ya Miundombinu na Mawasiliano. Na kwa sababu ya muda naomba niseme kwa ufupi tu kwamba nampongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri, fupi lakini imejielekeza katika yale mambo ambayo tulikuwa tunayahitaji. Bila shaka kuna maeneo ambayo yana mapungufu, tunahitaji maelezo zaidi.

Mhe. Spika, naomba nianze kwanza kwenye ukurasa wa 9-10 wa kitachu hichi cha hotuba ya Mhe. Waziri anapozungumzia Mpango Mkuu wa Taifa wa Usafiri wa Zanzibar *(Zanzibar Transport Master Plan)* pia Sera ya Taifa ya Usafiri.

Mhe. Spika, naamini kutokana na upya watu wa Barazani sijapata kuiyona hii, lakini naamini itakuwa inashughulikia kwa ujumla wake masuala ya usafiri wa aina zote katika Zanzibar. Nukta yangu hasa inanipeleka katika suala ambalo Mhe. Mtando ameligusia hapa nalo ni suala zima la usafiri wa nchi kavu yaani usafiri wa barabarani.

Mhe. Spika, Zanzibar tumetoka mbali, tulizowea kutumia magari yale yanayotupeleka kwetu mimi na wewe kule Makunduchi ambazo huku mjini tunaziita mbavu za mbwa. Halafu tulipokuja kupata daladala katika miaka ya 80 wakafuata shepu ile ile. Nadhani kutoka mwaka 1984 -85 serikali iliporuhusu sekta binafsi kuingia katika kusaidia usafiri katika maeneo ya miji mpaka leo ni miaka mingi sana sasa.

Kwa jamii au nchi ambayo inapiga hatua za maendeleo tulipaswa tuonekane tumetoka kule. Mimi nilikuwa nasema kuzungumzia madereva wa daladala na makondakta na hali ya gari zetu zilivyo. Tumefika wakati katika suala hili la mpango mkuu tuelezwe hivi Wizara hii haina mpango wa kutuletea usafiri wa kisasa hasa katika maeneo ya mji.

Mhe. Spika, tunakenda katika miji ya watu hasa kunapokuwa na msongamano kama hivi sasa tunaouona Zanzibar. Madaladala yamekithiri, hakuna nidhamu, yamekuwa yanaweza kusimama popote tu. Madereva wake kile yule ambaye kafeli katika maeneo mengi ndio anakabidhiwa daladala kuendesha. Maajali yanazidi katika miji yetu na katika maeneo yetu mbali mbali. Kwa kifupi katika sekta hii ya *public transport* kwa maeneo ya mjini kuna total cause. Nilikuwa nadhani katika huu mpango uteueleze kabla hatujafikia pahala pabaya zaidi kuliko hapa tulivyo sasa. Hebu tueleze serikali haina mpango wa kuona kwamba tupate kampuni mfano Mhe. Spika, ukenda pale London pana *Public transport* kuna yale mabasi makubwa. Ukiwa na usafiri kama kwanza unapunguza idadi ya magari. Kama daladala ilikuwa ina uwezo wa kuchukua watu kidogo ile ina uwezo wa kuchukua watu wengi zaidi. Ule wingi wa magari katika barabara unapungua.

Pili tunaona kwa wenzetu yale hata kama una leseni inabidi kukafanye *practice* maalum ya vipi kupatia abiria. Wewe dhamana yako ni zaidi ya kwamba unajiendesha wewe binafsi na familia yako. Sasa hapa kwetu sisi madereva ambao wamefeli kabisa ndio tunaowakabidhi daladala. Udhibiti au *regulation* katika suala hili ni mbovu sana. kiasi ambacho sisi kama ndio watumiaji wa

huduma hizi na wananchi kwamba wanakata tamaa kwamba. huwezi tena uka *repair* eneo hili kiasi ambacho ukapata huduma zinazostahiki.

Mimi nadhani ili wizara tuisaidie hebu kama tunavyosaidia kuwaalika sekta binafsi katika maeneo mengi na hapa tuone mabasi mekundu, au ya rangi ya kijani tunayoipenda yoyote. Ambayo yawe yanatembea katika mitaa yetu, ilimradi Mhe. Spika, tutoe huduma ambazo zinakwenda na hali ya kisasa.

Zanzibar tunajenga uchumi ambao ume *base* sana katika utalii. Wanapokuja pengine ile kuona mbavu za mbwa ni sehemu ya kivutio, lakini bora tuache ziende kule kwetu. Katika maeneo ya mji kudhibiti lile suala la *traffic* na suala zima la usala barabarani nadhani wakati umefika tunahitaji kuwa na kitu kama hicho Mhe. Spika. Nilikuwa naomba Mhe. Waziri akija anisaidie katika hili.

Nadhani hilo litasaidiana pengine na linalosemwa kwamba kunasudiwa kuanzishwa Mamlaka ya Barabara katika ukurasa wa 10 wa kitabu chake. Mhe. Spika, naomba kidogo anipe maelezo zaidi juu ya sheria hii ya Uanzishwaji wa Mamlaka ya Barabara. Je, itatusaidia kutupeleka huko tunakotaka kwenye huduma bora zaidi au ndio itakuwa tunaongeza Mamlaka tu kama Kawaida yetu lakini bado hai *reflect* katika huduma ambazo kuwa ni bora zaidi katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nimefurahishwa sana katika ukurasa wa 10 katika Idara hii ya Mipango, Mawasiliano na Utafiti kuna mambo mawili yamenifurahisha sana. Moja ni suala la kuja na mpango wa kuanzisha Sera ya Teknolojia ya habari na mawasiliano (TECNOHAMA). Ni vizuri maeneo mengi masuala haya yakawa na Sera tukawa tunajua muelekeo wa nchi yetu katika suala hili tunataka ku-*achieve* nini.

Mhe. Spika, hapa nilikuwa nina hoja moja. Mara nyingi katika Baraza hili tumepiga kelele sana kuhusu maadili, hata leo asubuhi. Mhe. Jaku alikuja na swali kuhusu maadili. Moja katika maeneo ambayo yanatupa shida sana na hili si kwa nchi yetu tu ambayo utamaduni wake umechangiwa na kuathiriwa sana na utamaduni wa Kiislamu. Lakini hata katika nchi za wenzetu zilizoendelea kunakuwa na udhibiti fulani kwa mfano wa matumizi ya *internet*.

Nilitaka kulizungumzia hapa kwamba siku hizi ndio biashara, ndio maendeleo tunavyoambiwa, kumekuwa na kuibuka kwa hizi *internet service (internet café)* kila pahala, pale ukenda hakuna udhibiti kuwa nani anatumia. Wakati mmoja nilikwenda katika kibanda kimoja natumia *internet* pembeni yangu kakaa kijana mdogo kabisa wa *primary school* anatizama picha za ngono.

Mhe. Waziri je, hatuoni kama kuna haja na mimi ninavyoambiwa katika teknolojia inawezekana kabisa kuzifunga baadhi ya *sites* zisionekane katika nchi fulani. Na zipo baadhi ya nchi zimefanya hivyo. Sasa katika kulinda haya maadili yetu tunayoyazungumza, hatuoni kama kuna haja ya vitu kama hivi katika Sera hii kuvitizama upya.

Mhe. Spika, pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa hii *idea* iliyokuwemo katika hotuba yake ukurasa wa 10 juu ya mpango wa kuanzisha *Zanzibar Civil Aviation Academy na Zanzibar Maritime Training Institute*. Hii ni hatua nzuri sana ya kupigiwa mfano. Kwa muda mrefu vijana wetu wanasumbuka sana mambo haya ya mafunzo na mambo yanayohusu usafiri wa anga. Gharama zake ni kubwa sana, Mhe. Spika. Vijana wetu wengi wanaopenda kuingia katika fani hiyo, wanagharamika wao na familia zao kupoteza fedha nyingi sana. Itaishia kwamba labda ni huduma ambayo itakwenda kwa wale wanaojiweza. Lakini watoto wengi wa kimasikini pengine wanao uwezo kiakili lakini watashindwa kupata huduma kama hizo.

Kitendo cha kuanzisha *Civil Aviation Academy* nakipongeza sana tunategemea kwa vyote viwili hichi na hichi cha *Maritime Training Institute* basi tuwe wabunifu zaidi Mhe. Spika. Moja katika dunia ya leo tunapobuni taasisi kama hizi kuna kitu kinaitwa *training up* yaani kuzitafutia taasisi nyengine nje ukaziwekea mahusiano. Kwa hivyo mnapata kubalishana uzoefu na maarifa na pengine hata misaada mbali mbali, hawa wakati wa mwanzo wakati unazianzisha taasisi kama hizi.

Mhe. Spika, nataka kusema wizara inapojipanga kuzianzisha ilione hilo. Ni kiasi gani inaweza ikapata mahusiano na taasisi za nje tena zenye *international reputation* ili hadhi ya Zanzibar tunayotaka kuijenga tuiyone kupitia katika taasisi kama hizi.

Mhe. Spika, jengine nimeligusia kidogo pale mwanzo nilipokuwa nikigusia Sera ya Usafiri ukurasa wa 12-22 ya hotuba hii inazungumzia sana secta ya usafiri wa nchi kavu. Mbali ya kwamba nimependekeza tuanze kuangaliwa kuwa na *public transport* inayoeleweka. Lakini kwa hivi sasa tunaishi na hii ambayo tunayo, sasa kama tunaishi na hii ambayo tunayo nilikuwa naomba Mhe. Waziri atusaidie. Wanapanga utaratibu gani kama alivyozungumza ndugu yangu Mhe. Mtando wa kuona kwamba hawa wanaobeba maisha yetu. Maana ukipakiwa ndani ya daladala inabidi usome Ayatul-Qursiyu tokea pale unapotoka mpaka pale unapofika Mwenyezi Mungu akihifadhi. Kutokana na vile tivu ambavyo unaviona mle ndani.

Nilikuwa nasema hebu atusaidia kuna mpango gani wa kuongeza udhibiti ya vitu hivi. Kwanza hizi gari zenyewe zinazotu mika katika shughuli hizi

zimefikia kiwango fulani. Madereva wake wanaoziendesha hizi daladala wamethibitishwa na wana viwango fulani pamoja na makondakta na vitu vyengine. Tuone, sheria kama hazina *sanction* Mhe. Spika, bahari nzuri wewe uliwahi kuwa hakimu unajua, zinakuwa hazina nguvu, watu ndio wanapoanza kuzidharau. Sasa tuone .hawa ambao wanakiuka wanachukuliwa hatua gani. Mhe. Spika, pia kuna malalamiko makubwa ya wananchi kwamba na askari wetu wa usalama barabarani wanachangia kutokana na kukithiri kwa rushwa, mtu anakamatwa lakini baadae akishatoa chochote anaachiwa. Hii inapelekea uzembe mkubwa sana katika suala zima la matumizi ya barabara na hasa matumizi haya ya usafiri huu ambao kwa nchi yetu bado unabakia kuwa ndio *public transport* tunayoitegemea.

Mhe. Spika, hapo hapo katika suala la usafiri nataka niombe ombi maalum. Mhe. Waziri pale tunapoishi katika Jimbo la Mji Mkongwe lakini limepakana na Jimbo la Kikwajuni la Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa kuna hii barabara inayopita baina ya jumba namba saba na namba nane. Mhe. Spika, njia hii karibu nayo itakuwa inaitwa machinjioni *road* kwa sababu ajali zimekuwa zinaongezeka sana pale. Kwa hivyo, tunaomba lile suala la kuwekwa tuta na wakati fulani tuliwahi kuomba tukaambiwa kwamba barabara hii imo katika hizo zitakazowekwa matuta. Lakini mimi nikajiuliza mbona hii barabara ya hapa Mafunzo na Uhamiaji yako matuta. Mhe. Spika, naomba hili Mhe. Waziri atusaidie sana pale kwa sababu pameshatokea ajili nyingi na zimeshauwa katika eneo lile. Naomba hili alitazame.

Mhe. Spika, vile vile naomba nije katika zile barabara ambazo amezitaja katika maeneo mbali mbali ya hotuba yake ukurasa wa 12-22. Kwanza ametaja hii barabara ya Maeneo Huru *Fumba Ring Road*, hii amesema ilikuwepo haikujengwa na bado inaahirishwa mpaka 2012 na 2013. Mhe. Spika, naomba maelezo kwa sababu tunasema tunataka maeneo haya yaendelezwe, lakini hatuyaekei miundombinu na hii ndio Wizara ya Miundombinu hata ule mradi mdogo tu wa barabara ya Maeneo huru nao tunauondoa tunauhairisha. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ni kweli tutavutia wawekezaji wakenda kuekeza kule hata kama huduma ya msingi yakuweza kupata barabara tunaanza kuliahirisha.

Mhe. Spika, hapo hapo nigusie kidogo huu mradi wa upembuzi yakinifu wa barabara zinazoingia Mjini Zanzibar. Vile vile nataka kupongeza zila barabara zote zilizotajwa zitasaidia kuboresha mandhari ya Mji wetu na kuimarisha huduma za kiuchumi. Lakini nilikuwa naomba najua Mhe. Spika, hili liko nje ya wizara hii ni shughuli hasa ilipaswa ifanywe na Mamlaka ya Mji Mkongwe pengine na Baraza la Manispaa. Lakini hizi barabara zetu za ndani za Mji Mkongwe kuna eneo hili la Darajani na Mchangani, kuna hizi barabara za Mkunazini ukishafika pale iliwahi kukufikisha ndani mpaka kwenye Sunni Madressa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kama Manispaa hizi zimewashinda

tunaomba Wizara ya Mawasiliano katika hii miradi yao wazijumuishe ili tuone nazo huu Mji Mkongwe unaotupatia fedha nyingi sana katika Sekta ya Utalii, biashara na mambo mengine basi pia huduma zake ziweze kukumbukwa.

Mhe. Spika, hapo hapo mimi nimepata wasi wasi kidogo katika mradi huu wa upembuzi yakinifu umetajwa barabara ya Mtoni, Amani, Kiembesamaki zimetajwa kilomita 8.5. Kwa hivyo, kidogo imenipa shida hapa imeorodheshwa lakini pia kuna mradi *specifically* ukurasa wa 19 ambao umeitaja barabara hii *specifically* ya Mtoni-Amani. Mhe. Spika, nasema mbona barabara hii moja inajumuishwa katika miradi miwili tofauti, kuna Mtoni-Amani halafu kuna Mtoni-Amani-Kiembesamaki. Mimi naomba maelezo katika hilo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, katika hilo hilo nimuombe kwenye ile miradi ya barabara pia kwa sababu amesha-*cover* maeneo mengi ya barabara hizi za Mjini basi pia asisahau barabara ya Chukwani-Buyu. Kwa sababu Mhe. Spika, hii ilitajwa katika kitabu cha bajeti kilichopitwa inaonekana haijatengenezwa na Mhe. Rais Karume mstaafu aliahidi kuijenga kwa kiwango cha lami, hebu pia tunaomba hii ijumuishwe katika huu mradi.

Mhe. Spika, naomba na mimi niungane hapo hapo katika suala alilozungumza Mhe. Mtando la ile njia ya Forodhani. Mhe. Spika, mimi ndiye Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe, lakini Mji Mkongwe unatumiwa sio na wananchi wa Mji Mkongwe, lakini hata wananchi wengine wote wanapata huduma zao pale. Kile kitendo cha kuifunga kile kipande kidogo pale mbali ya mambo mengine hakileti sura nzuri katika nchi yetu. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hebu kile kipande tukifungue, kwanza kitapunguza huu mgongano wa *traffic* kupitia hii *archway* ambayo iko chini ya ile *Muslim Academy* ya zamani pale. Pia kama kulikuwa na hitilafu zote mbaya tutaziondoa Mhe. Spika, kwa hiyo nilikuwa naomba hiki kipande Mhe. Waziri awaombe watu wake wakifungue ili tuweze kupata *traffic* iwe na *flow* vizuri sana.

Mhe. Spika, ukurasa wa 21 hotuba ya Mhe. Waziri ametaja Karakana Kuu Chumbuni. Hii naikumbuka tangu mimi mwanafunzi tukisikiliza hotuba za bajeti tunaisikia inatajwa na huko nyuma ilikuwa ndio pahala ambapo gari zote za serikali zilikuwa zikitengenezwa pale, lakini siku hizi mara nyengine kunatajwa sana kwamba magari ya serikali yanatengenezwa katika magereji ya mitaani. Kwa hivyo, hebu tuambiwe kwa sababu huku kunaweza kukawa kuna upotevu wa mapato, tulitegemea kama serikali ina Karakana Kuu yake basi gari zote za serikali ziwe zinakwenda kutengenezwa pale. Mhe. Spika, kwa nini hazitengenezwi pale kuna ukosefu gani katika Karakana Kuu na kama kuna ukosefu huo kwa nini haziwekwi hizi huduma zake ili gari zote za serikali zikawa zinatengenezwa pale kupunguza uvujaji wa mapato serikali kupitia hizi gereji za mitaani.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye ukurasa wa 22 Mhe. Waziri amezungumzia suala la uuzaji wa bendera, mimi nilikuwa nikijiuliza nimemchokoza rafiki yangu Mhe. Naibu Waziri kwamba Wizara ya Mawasiliano na bendera vyereje? Lakini sasa nikasema sawa pengine utaratibu wa kiserikali. Mhe. Spika, hoja yangu haiko kwamba wauze au wasiuze, kama wao wanauza mtengenezaji ni nani ndio hoja yangu. Na hoja yangu Mhe. Spika, ni kwamba sifa ya bendera zetu zinapauka haraka sana. Tulitengeneza bendera ya Zanzibar tukaipitisha katika Baraza hili kwa hamasa kubwa kwamba ni alama nyengine ya utambulisho wa kuwepo kwa nchi ya Zanzibar.

Kwa hivyo, basi hata ile hadhi yake pia ilingane na ile hamasa tuliyokuwa nayo, mimi nilikuwa naomba katika hili tulitizame. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ukitizama mara nyingi katika maofisi ya serikali kunapepea Bendera ya Muungano na kunapepea na bendera ya Zanzibar, unaikuta ya Muungano bado iko katika hali nzuri lakini baada ya muda mfupi bendera ya Zanzibar imepauka. Kwa hivyo, nilikuwa nasema hebu tuangalie *quality* ya hizi bendera. Mhe. Spika, nije ukurasa wa 24 kuna Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar hapa naomba nipate maelezo Mhe. Waziri kuna fununu nyingi mitaani anisaidie kwamba kuna uvujaji wa mapato hapa hasa katika ndege zinazotua pale, wasafiri wanaopita pale na mambo mengine. Mhe. Spika, kuna maneno mitaani nasema anisaidie yeye labda amefanya uchunguzi wa kiasi gani kwamba mara nyengine hufika pahala hata ile idadi ya ndege zilizotua zikarushwa yale mapato yanayoingia pale yakawa yanaingia katika mfuko mwengine. Mhe. Spika, naomba maelezo katika hilo kama Mhe. Waziri alijue hili na kama halipo atuhakikishie hapa.

Mhe. Spika, hapo hapo pia naomba maelezo katika eneo hili amegusia ukurasa wa 25 kwamba kumepungua idadi ya mizigo na ndege za mizigo zinazohudumiwa hapo *air port*. Ni sababu gani zilizopelekea suala hili naomba maelezo kwa sababu tunategemea sisi viwanja vyetu ili viongeze huduma ili mapato yaweze kuongezeka katika nchi sasa kama imeshuka kwa nini imeshuka?

Mhe. Spika, ukurasa wa 26 naomba haya niyaache kwa sababu Mhe. Mtando ameshayaelezea ilikuwa ni suala la uzio, kulikuwa na suala la *new terminal building* naomba pia maelezo hasa katika kava ya kitabu chake kuna maelezo hapa kwamba *the high mast apron broadlights and ground lights are out of our project scope.* Nilikuwa naomba maelezo kama hizi hazimo lile suala la *apron* na *taxiways* limekuwa kama ni pahala pengine lakini haya mambo ya *broadlights* na vitu vyengine je wana mpango wakuona kwamba na hivi pia vinajumuishwa katika miradi mengine yakuimarisha mradi wetu.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 27 kuna huo mradi wa kujenga *apron* na *taxiways*, lakini katika hotuba tumepewa vitabu haikuwemo lakini Mhe. Waziri alitaja kwamba kuna mradi hapa ambao wa Benki ya Dunia watatoa mkopo wa dola milioni 57. Kwa hivyo, nilikuwa naona kama aliwahi kuzungumza Mhe. Hija hazikuombewa ridhaa Baraza la Wawakilishi humu, kwa hiyo Mhe. Spika, tunategemea kwamba fedha hizi zote hata kama zinatoka nje ikiwa ni mikopo au misaada bado zikija ni za Zanzibar na wenye mamlaka ya kuidhinisha mapato ni Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hilo pia tuelezwe kwa nini hizi hazikuombewa bajeti.

Mhe. Spika, sasa naomba nije katika sekta ya usafiri baharini ukurasa wa 29 na kwa haraka haraka niseme tu kwamba mheshimiwa hapa tunaona kidogo kuna jitihada za kuimarisha huduma, lakini hizi huduma inavyoonekana kama vile hazikufanyiwa utafiti mzuri. Kwa sababu badala ya kuimarisha upande mmoja zimeimarishwa lakini upande zinaathiri. Kwa mfano, kujengwa kwa ile bandari inayohudumia abiria kwa hizi boti zetu zinazokwenda Dar es Salaam na Pemba kumepelekea kuwa na msongamano mkubwa sana wa magari katika barabara.

Mhe. Spika, bado shirika au idara na bahati nzuri mambo haya yote yako chini ya wizara hii hii moja hatuonekani kama kuna ufumbuzi wa suala hili. Naona hili halijakaa sawa tunaenda kuongezewa na kujengewa *landing craft* pale kwa ajili ya meli za mizigo. Mhe. Spika, hii haitoongeza msongamano zaidi na kuletea usumbufu sio kwa watu wa Mji Mkongwe lakini kwa watu wote wanaoutumia barabara zile, Mji Mkongwe unahudumia watu wengi sio watu wa Mji Mkongwe peke yake.

Mhe. Spika, hapo hapo kwenye ukurasa wa 30 amesema shirika hili pia linashughulikia utoaji leseni. Mimi nilikuwa nataka kumuuliza Mhe. Waziri katika ile mipango yake mingi mizuri ya kisasa ya kujenga nchi yetu hafikirii kwamba Zanzibar imefika pahala kujenga utaratibu wa kuwa na *flag of convenience*, na kama kunahitajika kuwa na sheria juu ya suala hili nchi nyingi zinafaidika kwa kutumia bendera yake kuruhusu kupeperushwa katika meli ikapata mapato. Kwa hivyo, sisi hatufikirii kuwa na utaratibu wa kuwa na *flag of convenience* ili na sisi tuweze kupata mapato katika eneo hili.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa mawili kwa ufupi tu katika ukurasa wa 40 Mhe. Waziri amezungumzia kuhusu *Zantel*. Hapa Mhe. Spika, wananchi wa Zanzibar wana kilio kikubwa sana. Kwanza *Zantel* kuhamishwa Zanzibar ukiwaambia wenyewe lugha hii hawaipendi, lakini ukweli imehamishwa. Pale Amani ipo lakini ipo ipo tu, lakini ukenda ukitizama ile Makao Makuu ilioko Dar es Salaam pale Msasani unajua hasa kama pale ndio Makao Makuu sio kama ilivyokuwa mwanzo, na imeondoka hata ile kubeba ujumbe wa Zanzibar.

Mhe. Spika, tulipoanza na *Zantel* hata zile kadi zake tulikuwa tunaziita za marhaba zilikuwa zinaonesha utamaduni wa Zanzibar, picha za Zanzibar, kalenda walizokuwa wakizitoa ziimarisha utamaduni wa Zanzibar yote yale Mhe. Spika, yameondoka kabisa. Nafikiri karibu tutaletewa twiga na zebra na vitu vyengine kama hivyo katika mambo yao.

Mhe. Spika, kuhusu hili kwa shirika ambalo serikali ina hisa asilimia 18 haipendezi, hili ni shirika la Wazanzibari na ni kampuni ya Wazanzibari. Mhe. Spika, hatujaathirika hapo tu kwani mapato haya tangu hapo, hapo lilipokuwepo Zanzibar tulikuwa tunaambiwa kwa sababu yakura utaratibu wa Muungano tuliwahi kuambiwa kuwa dola milioni 3,200,000 kwa mwaka ambazo zinalipwa hizi zinaishia *TCRA* hatujui sisi Zanzibar tunafaidika kiasi katika kuja *Zantel*, seuze sasa hivi tumelihamisha tumelipeleka kule kabisa. Lakini sio kama tumehamishiwa kule hapa Zanzibar ofisi yake ukenda, nenda hata pale ofisi yao inayotoa huduma wale waliokuwepo wafanyakazi wa kawaida ndio utakuta wafanyakazi wa Zanzibar, lakini ukipanda ngazi kidogo tu kuingia katika ngazi ya *management* tayari unakuta ndugu zetu wa damu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tulitegemea kwamba hizi kampuni ambazo Zanzibar zimeekeza basi ziwafaidishe Wazanzibari kwanza na nchi kama yetu Mhe. Spika, ambayo inatakiwa kujenga uchumi wa kisasa basi suala la kulea *middle class* ambao ni hawa vijana wetu waliomaliza masomo na wao wakapata kazi ili waweze kunyanyua uzoefu wao, lakini sasa hawa hawapati kazi. Mhe. Spika, huko Bara katika Taasisi za Muungano tunapiga kelele hawapewi na hizi zilizoko Zanzibar pia tunazichukua tunawapa ndugu zetu. Utaratibu kama huo Mhe. Spika, utakwisha lini hebu Mhe. Waziri unipe maelezo ya kina kuhusu suala la *Zantel* ili niridhike kwamba kweli *Zantel* ni ya Wazanzibari na itatunufaisha. Mhe. Waziri alisema asilimia 80 mapato ya *Zantel* yanatoka Zanzibar ndugu Moyo amekiri siku ile pale alipokuwa anatupa semina na akasema anaweza ku- *afford* yeye kwamba hata *Zantel* isipofanya kazi Bara itajiendesha kwa mapato yatakayotoka Zanzibar. Mhe. Spika, halafu unakuta huduma zote zimepelekwa Bara sasa faida yake nini Wazanzibari sisi tunachangia kazi yetu kumchumia mjomba tu.

Mhe. Spika, pia naomba kutoka kwa Mhe. Waziri juu ya mapato ambayo sisi Zanzibar tunayapata kutokana na haya mashirika na kampuni ambazo ni za Muungano kwa upande wa huduma kwa Zanzibar. Tuna hii *TCRA*, tuna *TTCL* na tuna *TPC* naomba nipate maelezo katika hilo. Na la mwisho kabisa niliombwa kwamba kuna wafanyakazi hawa wanajiita wa *group* "C" katika Shirika la Bandari wanasema wamesaidia sana hata hii M.V Jitihada wameitengeneza wao na mambo mengi sana, lakini hawakumbukwi katika maslahi kwa vyovyote namuomba Mhe. Waziri akija na hili anipe maelezo kuhusu wafanyakazi wa *group* "C" pale bandarini anawafikiria nini katika

maslahi yao. Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja lakini nitaunga mkono zaidi baada ya kupata maelezo juu ya yale ambayo nimeyatoa, nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia uzima, salama na uhai na kuweza kufika hapa kuendelea na mambo ambayo yanatulazimu ili kuweza kuendeleza nchi yetu. Pili nachukua fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Spika, kutokana na unavyoendesha shughuli zako kwa ufanisi na kwa umahiri mkubwa.

Vile vile napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Naibu Waziri na timu yake yote kutokana na kazi nzuri ambayo wameifanya kuhakikisha kwamba hotuba hii inakuwa safi na makini kabisa.

Mhe. Spika, kwa kuanza mimi ilikuwa nianze na ukurasa wa 11 ibara ya 23 katika suala la Idara ya Utumishi, lakini kwa sababu nilishindwa kupata vielelezo vya uhakika sehemu hii nitaiwacha hapo baadae nitakuja kuifuatilia ili tuweze kupata uhakika wake. Ilikuwa inahusu masuala ya uajiri.

Mhe. Spika, sehem ya pili ambayo nilitaka kuchangia ni eneo la ujenzi wa barabara. Mhe. Spika, katika maeneo yetu ya Jimbo la Kikwajuni sisi tunafarijika zaidi kuona zile barabara zetu za ndani zinafanyiwa marekebisho na kuweza kuwa katika *level* ambayo watu wengi wanaitarajia. Kwa bahati mbaya nilikuwa naangalia sana hapa katika kitabu hiki ili niweze kuona maeneo ambayo tutaneemeka, lakini baada ya maelekezo mazuri ambayo tulikwishakupata kwa Mhe. Naibu Waziri katika vikao vyetu vilivyokuwa vinaendelea hapa, kwamba tutapata neema ya kutengenezewa barabara zetu mbili ndani ya Jimbo la Kikwajuni badala ya kuangalia nyuma nimekuta kuna barabara moja tu ndio ambayo tutakuja kukutana nayo.

Lakini nilipokuwa nakwenda zaidi katika utafiti wa barabara za ndani ambazo zitakuwa zinatengenezwa nimekuta kwamba kuna asilimia kama 43 ndio barabara za ndani ambazo zitakuwa zinatengenezwa kwa upande wa Zanzibar, na asilimia 57 barabara za ndani ambazo zitakuwa zinatengenezwa kwa upande wa Pemba. Kwa hivyo, barabara nyingi za ndani ambazo tulikuwa tunaulizia tunaambiwa kwamba hili suala linahusu zaidi na Baraza la Mji la Zanzibar kwa ajili ya hizi barabara za ndani. Sijui kwa huku upande wa Pemba ambapo tumepata asilimia 57 kuna Baraza la Mji ambalo litakuwa liko makini likaweza kufanya masuala haya na kufikia katika *level* hii. Nitamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupe maelezo ya ziada.

Mhe. Spika, suala la pili ambalo nilikuwa napenda kuchangia wakati umefika sasa katika suala la leseni, leseni zetu za Zanzibar zinashughulikiwa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, lakini wapasishaji wa masuala haya wanakuwa ni ndugu zetu wa polisi. Mimi naona kwamba wakati umefika sasa ili ndugu zetu wa polisi kwa sababu wao ndio wenye dhamana ya vyombo na barabarani wao wawe ndio wapasishaji na watoaji wa hizi leseni. Pia hawa ndugu zetu wa mawasiliano wawe wanaratibu shughuli zote za kuweza kuhakikisha kwamba mapato ya serikali yanapatikana na yanakwenda katika utaratibu ambao unatakikana.

Mhe. Spika, jengine nilikuwa nataka nizungumzie ukurasa wa 24 ibara ya 60 ambapo kuna suala la ulinzi na usalama katika maeneo ya *air port*. Mhe. Spika, juzi nilifanya matembezi katika maeneo yale ambapo wanashukia abiria wa kawaida pamoja na mizigo yao. Nilipata fursa yakuweza kuonana na baadhi ya watendaji ambao wapo pale *air port* na wanafanya shughuli zao mbali mbali.

Mhe. Spika, kitu ambacho kilinishtua na kunishangaza zaidi ni pale nilipoonana na askari wa Jeshi la Polisi na wao wakawa wanasikitika kuona kwamba wanashindwa kufanya majukumu yao kama ambavyo kazi zao zimewasabisha waweko pale. Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inagharamika kusomesha watu wake katika fani mbali mbali, na baadae kuwachukua watu wale kuwapeleka katika maeneo ya *air port* kwa ajili ya kulinda ulinzi na usalama katika nchi yetu, ikiwa ni pamoja na kudhibiti madawa ya kulevya.

Kwa hivyo, utaratibu wa kuwa uangalizi wa mizigo katika *air port* yetu ya kimataifa ya Zanzibar, mimi naona kwamba una matatizo kwa namna fulani. *Air port* ile wanaoshughulika na upekuzi wa mizigo ni watu wa mawasiliano na uchukuzi, watu ambao kwa imani yangu kabisa nina amini kwamba hawana taaluma na ujuzi wa kuweza kutambua watu gani wanafanya nini na kwa sababu gani. Mhe. Spika, ningeliomba katika kitengo cha upekuzi wa mizigo wale watu ambao wanapewa majukumu yale ndio wawe wahusika kamili na wanafanya taratibu zile kwa mujibu wa sheria inavyotuongoza.

Mhe. Spika, jengine katika kitabu hiki cha bajeti ya mara hii kuna maeneo hapa niliona kwamba kuna uboreshaji wa maboya na kuna maboya ya *solar* ambaya yanataka kuwekwa. Tayari katika uchangiaji wa maswali na majibu hapa ambao ulikuwa unaendelea katika kipindi cha nyuma kidogo tuliona kwamba kuna mmoja kati ya wajumbe wetu aliulizia suala la maboya na akaambiwa kwamba kuna maboya matatu tu ndio ambayo yana matatizo.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa kwa mara nyengine tena atuelezee hasa kuna maboya mangapi ambayo hayafanyi kazi na wamejipanga vipi kuhakikisha kwamba maboya hayo yanafanya kazi na kuweza kuzisaidia

meli zinazoingia na kutoka katika nchi yetu ziende kwa usalama na kuweza kunusurisha ajali ambazo tunahisi kwamba tuna uwezo wa kuziepuka.

Mhe. Spika, vile vile kuhusu utengenezaji wa MV Jitihada. Mhe. Spika, maelekezo ambayo tulikuwa tumepata majuzi tu hapa tuliambiwa kwamba meli hii imekwishakutengenezwa na sasa iko tayari inatafuta watu wakuweza kukodi ili kuweza kuendelea na masuala yake yakutoa huduma kwa wale ambao watakuja kukodi. Mhe. Spika, katika kitabu hiki tulitarajia kuona gharama halisi za matengenezo ya meli ile ili tuweze kwenda sambamba na kuweza kutoa maoni yetu juu ya suala lile. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa aweze kutufahamisha meli hii imetengenezwa katika kiwango gani na kwa thamani gani.

Mhe. Spika, jengine ni suala la ununuzi wa tishari katika maelekezo ya kitabu hiki tumeona kwamba kuna tishari ambalo linataka kununuliwa. Tungelimuomba Mhe. Waziri pale tayari naona tishari dogo limekaa je, tishari hilo ndio lile lilokuwa linataka kununuliwa au kuna jengine ambalo litanunuliwa baadae. Tunaomab maelekezo yakina katika hili.

Mhe. Spika, nikiendelea katika kitabu cha bajeti cha mwaka uliopita tuliona katika nafasi ya malengo kwamba kulikuwa kuna ujenzi wa jengo la abiria katika bandari ya Zanzibar, lakini katika kitabu hiki kipya eneo hilo hatukuliona na wala hakuna sababu ambazo zimeelekeza kwa nini ikawa hamna eneo hilo. Jengine katika kitabu hiki hiki cha bajeti iliyopita kulikuwa kuna ununuzi wa vifaa vya *air port* ikiwemo matrekta na mambo mengine. Lakini katika kitabu hiki kipya ambacho kimekuja mara hii hatukuona eneo hilo na wala hatukujua kwamba yale matrekta ambayo yalikuwa yanatakiwa kununuliwa na serikali ikawa imeidhinisha pesa ilikuwa ni suala la kufuatilia tu Wizara ya Fedha na Uchumi hatukujua kwamba matrekta yale yamenunuliwa au vipi. Atakapokuja Mhe. Waziri hapa tunaomba atusaidie zaidi fedha hizo zinahusiana na *MDRA*, tunaomba maelezo kuhusiana na suala hilo.

Mhe. Spika, baada ya maelekezo hayo mwisho nimalizie katika kitengo cha Mashirika ya Simu. Mara nyingi hapa Zanzibar tumekuwa tukizungumzia suala la simu hizi za *Zantel*, lakini ndani ya Zanzibar kuna mashirika mengine ambayo yapo hapa. Kuna *Vodacom*, kuna *Zain*, kuna *Tigo* na mengineyo. Mashirika haya Mhe. Spika, hatuelewi hasa nini faida ya Wazanzibari tunaipata kutokana na mashirika haya kuwepo kwao hapa Zanzibar. Mhe. Waziri atakapokuja hapa tunaomba atuelezee japo kwa muhtasari serikali inapata asilimia gani ya mapato kwa mashirika haya mengine ambayo yako hapa Zanzibar na kuendeleza shughuli zao kama ambavyo *Zantel* inafanya.

Mhe. Spika, baada ya maelekezo hayo kwa kuokoa muda wako kwa heshima na taadhima na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni naunga mkono hoja kwa asilimia 99, ahsante sana.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nitakuomba radhi nitakaa kitako. Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kufika hapa na tukawa tuna afya njema ya kuzungumza. Nakupongeza na wewe Mhe. Spika, na nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza na mimi kidogo katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano. Vile vile nampongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote waliopo Unguja na Pemba katika sekta hii kwa kuweza kupanga shughuli zao vizuri na tukaweza kufika hapa tulipo. Pia nampongeza Waziri wetu aliyepita kipindi cha nyuma kwa kuweza kuyasimamia mambo haya kikamilifu na mpaka hivi leo ikawa Mhe. Waziri tuliyenaye anaweza kuyaendeleza kutimiza ahadi ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, mimi nataka nizungumze kidogo tu katika ukurasa wa 12 mpaka nafikiri nitafika ukurasa wa 17 kwa jumla. Mhe. Spika, hapa pana mradi wa barabara 3 za Pemba, barabara hizi ni muhimu sana na barabara hizi tulizizungumzia wakati tulipokuwa katika Baraza la Kikwajuni. Mhe. Spika, barabara inayotoka Ole-Kengeja na barabara ya Kipangani-Kangagani. Mhe. Spika, barabara hizi ni za siku nyingi sana na barabara hizi wananchi wetu wanamahitaji sana ya barabara hizi kwa sababu ni barabara ambazo kwamba zina watu wanatumia kutoka kule kuja Mjini.

Mhe. Spika, hata ukamwambia dereva kule apeleke gari huwa wanakataa basi wakati wa mvua barabara hizi zina matatizo sana. Barabara ya kutoka Kojani basi mheshimiwa kukinyesha mvua huwezi ukenda na gari, barabara imekatika vibaya sana. Tunasikia barabara hii imeshakua kwenye matengenezo, lakini bado hiki kipindi cha nyuma nataka kuja huku mimi nimeshakwenda na bado sijaona matengenezo yoyote juu ya ile barabara. Kwa hivyo, tunakuomba Mhe. Waziri ikiwa mradi huu wa barabara tayari waweze kuwafikiria wananchi wale kuweza kuwafanyia matengenezo ya barabara ile ili kupata mahitaji yao na wao bila ya kuwa na usumbufu.

Mhe. Spika, vile vile pana barabara ndogo ya Mchangamdogo kuingia Hindi naona sijakiona humu na barabara ile ni mbovu sana yakutokea Mzambarauni. Sijui wenzetu wale wao wanafikiriwa vipi Mhe. Waziri tunakuomba aweze kuiona ile barabara wenzetu wa *TASAF* walikwenda pale kuweka kifusi lakini mheshimiwa unachukua dawa unaiweka juu ya kigaga haikai, barabara ni ya zamani ina majiwe kwani haikukwangurwa. Mhe. Spika, hivi karibuni mimi nimekwenda kule ni kuwa barabara hiyo haipitiki na ni mbovu sana.

Mhe. Spika, pia barabara yetu hii ya kutoka Kipangani kwenda Kangagani namuomba Mhe. Waziri wakati barabara hii sio ya leo tunaizungumzia kila siku ajitahidi iwezekanavyo barabara hii ipate matengenezo yake tena kwa lami kwa sababu Mhe. Rais ndivyo alivyoahidi kuwa itajengwa kwa lami. Vile vile barabara inayotoka Ole kwenda Kengeja mheshimiwa tunasikia barabara hii imeshaanza huko katika mradi, lakini barabara hii tunaomba kwani ni barabara kubwa na barabara hii iko kati kati kila itakapopita inapita kati kati ya majumba. Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri awe makini sana kutujengea barabara hii kwa kuweka alama za barabarani na hata kuweka matuta kwa sababu madrasa lazima ukate njia ndio uingie upande mwengine na skuli ni vile vile ukate upande huu uingie upande mwengine. Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri barabara hizi atakapozijenga hizi awe muhitaji sana wakuzitizama hata kuziwekea matuta wala asituwekee matuta yale ya *foundation*, aweke matuta hasa yale makubwa.

Mhe. Spika, kwa sababu alipotujenge *COGEFAR* hatukuwa makini pale Kianga mheshimiwa tuna tatizo sana kwa gari zinavyokwenda mbio na kila siku pale panagongwa watu. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri atakapozijenga barabara hizi awe muangalifu na umakini kweli kweli.

Mhe. Spika, nikitoka hapo kidogo nitaingia katika usafiri huu wa bandarini na nitaanzia katika bandari ya Mkoani. Mhe. Spika, usafiri wa bandarini una matatizo makubwa sana kwanza ya msongomano wa watu tutakapokwenda katika meli, pale hapana utaratibu, upande huu unapita magari na upande huu wanapita wananchi huwa msongamano ilimradi tuna matatizo. Mhe. Spika, halafu pale gatini magari yanayoingia ni mengi sana na gati ile tuna wasi wasi nayo kuwa ni mbovu, gati ile inatuwama maji hayajuulikani yanapotokea na pale pana msongomano mkubwa wa watu na magari yanayopakia mizigo na mambo mengine. Mhe. Spika, isijekuwa tena pakawa na hadithi likachawanyika ikaja ikawa ni mtihani, tunamuomba Mhe. Waziri awe makini sana katika bandari ile ya Mkoani.

Halafu hata usafiri una matatizo Mhe. Spika, kwa sababu msongamano wa watu unaokuwepo pale, basi watu wa jinsia nyengine kusafiri ni tabu. Ukienda pale pana watu wanaosafiri waliokuwa hawajiwezi ni mtihani mkubwa sana, watu wanasukumana na eneo lile tunaliona lilivyo ni kama vile.

Jengine Mhe. Waziri nije kwenye gati yetu iliyopo Malindi. Gati hii inayojengwa hivi sasa ina matatizo kidogo, kwa sababu hapa tunapoteremka gari kuteremka bondeni kule kwa watu waliokuwa hawajiwezi na msongamano wa watu uliopo njia ni finyu, basi Mheshimiwa pale ni mtihani. Kwa sababu mimi nimeshawahi kufika pale kigari cha kwendea bondeni hakipo na mimi naumwa natoka hospitali sijiwezi ikabidi nichukuliwe mmoja akamate na

mwengine huku kupelekwa kwenye meli. Kwa hivyo, nikakata usafiri ule ikabidi sasa mimi nisafiri kwenye usafiri wa anga. Pale pana matatizo, hata mgonjwa akitolewa katika meli Mhe. Spika, nimemuona kwa macho yangu mgonjwa anatolewa pale kwa godoro, tunaomba pawe na vifaa ili mgonjwa atakapoteremswa kwenye meli asitolewe kwa kigodoro atiwe kwenye machera aletwe juu kwenye kitanga aje aingizwe kwenye gari. Tunamuomba Mhe. Waziri asimamie kwa umakini mambo hayo ili kuondoa usumbufu wa wananchi na kuweka Zanzibar yetu kuwa katika hali ya usalama na ikapata sifa katika mafao yake.

Halafu Mhe. Spika, katika viwanja vyetu vya ndege. Mimi nashukuru sana katika viwanja hivyo, nasafiri sana katika viwanja hivyo, lakini tatizo nililoliona katika sehemu hizo ni siku za mvua maji ni mengi sana ambayo kuwa labda uvue viatu, maji mengi sana viwanja vyote viwili, kiwanja kilichopo Pemba na cha Unguja. Mhe. Waziri pale afanye utaratibu wa maji yale kuweza kuyaondoa na yasituame pale. Mvua ikiwa kubwa tukisafiri tuliokuwa hatujiwezi tunapata tabu sana kwa viwanja vya ndege vyetu kwa kutuama maji.

Mimi ninawashukuru sana watu wa Uwanja wa Ndege ninaposafiri sina kadhia sana, lakini wenzangu wanapata shida. Kwa sababu ujione wewe lakini pia uwaone na wenzako. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ajitahidi sana katika maeneo haya kwa sababu ni maeneo ambayo yanapita watu wa aina mbali mbali.

Mhe. Spika, katika ujenzi wetu wa gati au ujenzi wa vikalio mule manamokaa watu tunamuomba Mhe. Waziri katika mabanda yale yatakapojengwa pawe na sehemu ya kupita watu waliokuwa hawajiwezi na vigari vyao, isiwe tena watu wakitaka kupita tena wale waliopo pale wanyanyuke kumsaidia mtu aliyekuwa hajiwezi kumuweka kwenye bao kukaa kitako.

Hata vyoo, vile vyoo vilivyoko pale patengwe choo kimoja kilichokuwa walemavu wataweza kujisaidia. Mlemavu anakwenda pale apande vidaraja, ateremke ni mtihani Mhe. Spika, tunaomba Mhe. Waziri hili nalo alione ili kuondoa usumbufu kwa wananchi wote, kwa sababu sote tuna haki za kusafiri na kurudi majumbani kwetu.

Halafu Mhe. Spika, nizungumzie katika majumba yatakayojengwa au yanayojengwa. Kwa sababu juzi sikupata fursa ya kuzungumza lakini hapa pia yanahusika nitazungumza. Mhe. Waziri barabara iwe na vielelezo vya kuweza kusimama magari watu kupata njiani. Kwa sababu tunapita watu wa aina mbali mbali na majengo yanayojengwa basi yajengwe yale majengo yanayokidhi haja kwa watu wa sasa. Kwa sababu wengine hatujiwezi, tukifika pale pana vigazi sita uteremke kwenye kigari chako huna mtu wa kukupandisha upande kwa

miguu ni mtihani, upande kwa mikono na mafuti ni mtihani. Tunawaomba waheshimiwa watakapojenga katika maofisi na sehemu nyengine wajue kuna watu wengine waliokuwa hawajiwezi waweze kuwawekea sehemu zao na waweze kujisaidia.

Mhe. Spika, hata kwenye hayo maofisi katika kujenga vyoo viwemo vya watu waliokuwa hawajiwezi, wengine hawawezi kutembea kwa miguu lazima aingie na kigari chake kile akifika pale pawe na choo cha kisasa aweze kukaa na kupata mahitaji yake. Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri atakapotufanyia majumuisho hapa aweze kutueleza majengo yaliyojengwa tuliyoyapigia kelele toka mwaka 2005 ni jengo gani na gani lililotimiza ahadi yake na mimi nilikuwa nikizungumza kila siku mpaka skuli kwa watu waliokuwa hawajiwezi tulijue ili na sisi tuweze kufika katika majumba yale kwa urahisi.

Halafu Mhe. Spika, sitakuwa mwingi wa fadhila mimi nampongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kutuona watu wenye ulemavu, kila sekta unayokwenda watu wenye ulemavu wako wanapewa kipaumbele. Tunaomba katika Baraza la Wawakilishi tuweze kupewa kipaumbele nisiingie mimi peke yangu, nafasi moja ya watu wenye ulemavu hatuna mbunge, hatuna chochote isipokuwa mimi peke yangu. Naomba vyama vyengine vyovyote waweze kutoa watu kugombania uwakilishi ili kuja hapa kutetea haki zetu za wanawake na makundi maalum.

Mhe. Spika, baada ya hapo mimi nakushukuru sana na ninamshukuru Mhe. Waziri na watendaji wake na ninaunga mkono hoja.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii kutoa mchango wangu ili kumsaidia Mhe. Waziri kama ulivyotuelekeza kwa lengo la kufikia ufanisi kwenye maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi naomba nitoe pongezi maalum kwa Rais wa Zanzibar kwa kuamua kumchagua Wenzangu wanamwita Magufuli lakini mimi nasema Mhe. Hamad Masoud, kuwa waziri wa wizara hii na msaadizi wake Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) kuwa naibu waziri. Kwa kweli ukiwaangalia tu picha zao ni kuwa hawa wanaelekea kuwa mawaziri wa wizara hii, sasa uhalisia itategemea matendo yao ambayo watatufanyia Wazanzibari.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba lazima nipongeze kwamba kabla ya Rais wa Zanzibar aliyestaafu Dkt. Amani Abeid Karume alikuwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, na kwa kweli alituwekea mtandao mzuri wa miundombinu hasa barabara Unguja na Pemba. Lazima nimpongeze kwa hilo na kama kweli wenzangu hawa watafuata nyayo zile, basi watakuwa wanaenzi

sio tu Dkt. Karume aliyestaafu, lakini hata Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Mhe. Spika, mara nyingi ninapozungumzia barabara baadhi ya watendaji wa wizara hii husema sina shukurani, lakini kama shukurani ni kunyamaza kimya basi na nizikose maisha, lakini nitasema pale ambapo barabara haziendi vyema hasa ndani ya jimbo langu.

Mhe. Spika, *UUB* wametuomba shilingi 1.004 bilioni kwa kazi za kawaida, mishahara na *other charges*, lakini wao wenyewe wanakusanya shilingi milioni tano. Wametuomba tuwaidhinishie shilingi bilioni moja, lakini wao mchango wao serikalini ni shilingi milioni tano, ni asilimia ndogo sana ambayo wanakusanya. Kwa hivyo, hili ni jukumu la serikali waangalie njia gani watawawezesha wenzetu kukusanya pesa nyingi.

Mhe. Spika, jengine niwapongeze wizara hii kwamba wamebuni na kujenga hoja barabara mpya zenye urefu wa kilomita 108.7, hizo wamezibuni. Mimi nashukuru sana kwamba wamekaa, wamehangaika na kutafuta wafadhili kwamba kumbe wana uwezo wa kubuni na kutafuta wafadhili kwa barabara zenye urefu wa kilomita 108.7 hizi peke yake ni zile za *Zanzibar Urban Entry Roots* na nyengine kilomita 25 zile za barabara tatu za Unguja. Jumla ni barabara ambazo zinaifikia karibu kilomita mia moja na kidogo.

Lakini wenzangu hawa Mhe. Spika, wameshindwa kwa mara nyengine kubuni na kutafuta mfadhili kwa barabara kongwe ya miaka 20 nyuma ya Mgagadu/Kiwani ya kilomita 7.6. Barabara mpya wamebuni na fedha wamezipata, lakini barabara kongwe ya tangu Karume Mkongwe wameshindwa kubuni na kuipatia fedha barabara hii na habari yake wanatuletea hadithi ambazo hazina maana yoyote.

Mhe. Spika, mimi kazi yangu hapa ni kuidhinisha fedha kwa ajili ya maendeleo ya nchi, sina jukumu la kuidhinisha fedha kwa ajili ya watu kuharibu. Mhe. Spika, nataka Mhe. Waziri anambie kitabu cha mwaka jana waliandika kwamba barabara ya Mgagadu/Kiwani urefu wa kilomita 7.6 imetengenezwa kwa kilomita 3 kifusi, kitabu cha leo barabara hiyo hiyo wanatwambia kifusi wametia kilomita 0.5. Je, zile kilomita 2.5 zimebururwa na maji? Huu ni uongo usio taa.

Mhe. Spika, si maandishi yangu ni maandishi yao wenyewe vitabu viwili. Mwaka jana walitwambia wamejenga mpaka nukta tatu kamili kwa kifusi.

Mhe. Spika: Mheshimiwa jaribu kutumia lugha iliyo nzuri, unaweza ukasema sio kweli.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakubali, sio kweli hata kidogo kwamba barabara ya mwaka jana wametwambia wenyewe kwamba wamejenga kilomita 3 kwa njia ya kifusi kwa kutumia gharama ya shilingi mia tatu na hamsini, mara hii wanatwambia wamejenga kilomita 0.5 kwa kifusi, hizi kilomita 2.5 zimekwenda wapi? Bahati mbaya barabara ile haina chemchem kwamba kimebururwa, wanatutania kiasi hiki.

Mhe. Spika, sisi kazi yetu hapa kuja tukitoa hadithi tu na kutumia, lakini ripoti ya *CAG* anatwambia barabara hii hawakuziona fedha matumizi yake shilingi milioni mia tatu, *supporting document* pia hazipo. Mwaka juzi barabara hii hii ilitumiwa shilingi 40 milioni kwa teknolojia ya *RO-MIX*.

Mhe. Spika, tusifanyeni masihara, masihara hayafai kwenye mali ya watu, Mhe. Waziri lazima anambie kwa nini vitabu hivi vinatofautiana. Aliyeandika alikuwa likizo, kipofu haoni au anakusudia kutuchezea.

Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano haina nia ya kujenga barabara ya Mgagadu/Kiwani na mimi siko tayari kuwaidhinishia pesa wakenda wakaponda. Kwa mujibu wa maelezo yao na kwa mujibu wa maelezo ya *CAG* pesa hapa zinaharibiwa, hatuwezi kila siku kuona hadithi.

Juzi ndugu yangu Naibu Waziri alikwenda Kiwani akawaambia watu wa Kiwani nitakaa na Mhe. Hija Hassan tujenge barabara kwa kifusi. Hivyo mimi huo mshahara ninaopewa nijenge barabara? Kwa hivyo, ikiwa mmeshindwa kutujengea barabara yetu kwa miaka 15 hamna haja ya kutuomba fedha. Lazima Wizara ya Mawasiliano kupitia idara hii Pemba wana matatizo watwambie kuna matatizo gani? Haiwezekani Mhe. Spika.

Mimi nimekwenda mwenyewe kwa *engineer* amenambia barabara ile ili imalizike ni 1.2 bilioni, sasa wewe ndiye *engineer* mtaalamu leo unatutilia shilingi milioni mia tatu! Wakati umeshafika wa kutuchezea kiasi hiki halafu unawaambia wananchi barabara hii itajengwa na nani? Malaika Mhe. Spika? Mhe. Spika, wasichezee udhamini mwengine, kama hamna uwezo wa kujenga barabara hizi tafadhalini zitoweni, itoweni ili Wazanzibari wa Kiwani waone kwamba serikali hii imeshindwa kujenga barabara ya Mgagadu/Kiwani, miaka 15!

Mhe. Spika, barabara hii kwa mtazamo wangu na kwa ushahidi wa *CAG* na vitabu ni mtaji wa watu maalum na mimi siko hapa kuidhinishia watu mtaji, kwamba watu wapate barabara hii wanufaike, wanenepe, wacheze na magari mazuri, mimi siye mwakilishi wa kazi hiyo. Mimi nitaidhinisha fedha kwa ajili ya watu walionichagua.

Mhe. Spika, kwa hapa Mhe. Waziri hana jibu la kunambia, ama anambie fedha itaongezwa vipi na lini kazi itaanza ya lami, vyenginevyo namuomba Pemba watendaji awaondoshe hawafai. Mhe. Spika, nadhani ujumbe wangu umefika kwamba sina jibu la msingi hapa nitakalopewa nikaliamini kwa sababu maandishi yenyewe yanagongana hawana ukweli katika vitabu. Ni dhahiri kwamba barabara ile ni mtaji wa watu ambao wanafaidika.

Jengine ni kwa barabara sita za Kusini Pemba. Mimi nashukuru nimejengewa barabara moja ya Mtambile/Mwambe kilomita 9.4, ingawa nina haki ya kujengewa kwa sababu barabara ya Kusini Pemba hujengi mpaka uje Mwambe. Kwa hivyo, hii si hidaya wala si zawadi ni haki yangu. Lakini nimekuwa nikisema kwamba barabara hizi hazina viwango vizuri na haya maelezo sio yangu mimi wataalamu wenyewe wanasema hivyo.

Kwa mfano, kila barabara ilipangiwe ipitie hatua nne, kuna hatua ya *sub grade ten centimeter*, kuna hatua ya *sub base ten centimeter*, *base ten centimeter* na hatua ya *asphalt 0.1 four centimeter*. Mhe. Waziri anambie barabara ipi imetimia kiwango hicho na kila hatua Mhe. Spika, mna fedha iliyotengwa, sasa ikiwa barabara haikufikia kiwango hicho maana yake huo ni wizi. Sasa mama watu wanatujengea barabara chini ya kiwango na baadae waziri wamekaa na wizara yake sisi tuhesabu nini.

Mhe. Spika, kwa kweli tuna masikitiko makubwa, unyonge wetu isiwe sababu ya kutuonea. Pemba barabara hakuna, Norway wametufadhili kwa huruma leo watu wanatuchezea?

Mhe. Spika, mbali na hilo nina tetesi kwamba barara hizi kuna wizi unafanyika na hili Mhe. Waziri nimemwambia akakiri kwamba kuna mtindo wa wizi unafanyika, naomba nijue kuna hatua gani iliyochukuliwa. Mhe. Spika, hizi ni pesa za walipa kodi, wanyonge wako hali mbaya sana, kwa hivyo hatuwezi kuchezea maslahi ya watu kwa watu wachache. Mhe. Spika, hizi barabara ni mbovu sana kwa kweli kuzikataa hatuwezi lakini hazina kiwango na wenzetu wanatuchezea.

Mhe. Spika, niende kwenye Shirika la Meli na niwaambie serikali kwamba wanasahau kwamba Zanzibar hatuna meli? Wazanzibari wa Unguja na Pemba wanasafiri kwa meli na hatuna meli na mmekuwa na uzito kiasi gani kwamba kila siku meli, meli, meli hii inaundwa wapi? Mhe. Spika, meli hiyo hata kama ingekuwa inaundwa mbinguni ingekwishafika chini hapa, lakini serikali hamna nia ya kuunda meli mpya kwa ajili ya Wazanzibari. Leo Mhe. Spika, waziri anambie miaka mitatu MV. Maendeleo imetengenezwa kwa shilingi ngapi na iko wapi, kila mwaka wanapeleka Kenya matengenezo baadae anambie faida shilingi ngapi imeingiza.

Mimi nampongeza sana Mhe. Ali Mzee ni Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Meli, kama si msaada wake na busara hii meli ingekuwa haipo hapa, lakini ni mwenyekiti wa bodi aseme nini, anashauri kitaalamu na kihalisia lakini serikali haikubali. Sasa meli hii ya MV. Maendeleo nayo iuzwe, imeuzwa MV. Mapinduzi tushanyamaza kimya mmeshachukuwa pesa zenu hakuna tatizo na hii uzeni mchukue pesa zenu msiweke mzigo mbovu, bora wayauze Mhe. Spika, yawe hayapo baadae sisi tushukuru Mungu.

Mhe. Spika, Pemba wamejenga jengo la Shirika la Meli Mkoani linavuja, amepewa mkandarasi *runs* jengo linavuja, maana yake kama vile fedha ya watu haina uchungu wowote watu wanatumia tu, ponda uje kufa kwaja. Mimi nasema kwamba, lazima wawe makini sana katika kusimamia fedha za umma.

Lakini jengine Mhe. Spika, meli za watu binafsi zina mtihani, naomba nisome mkataba wa *Seagull Sea Transport*. Mkataba huu unasema, "kwa heshima naomba uhusike na mada ya hapo juu, kutokana na hali tuliyonayo sasa hivi tunakuomba kukufahamisha kuwa, Kampuni yetu haina pesa za kukulipa mshahara. Hata hivyo, kampuni inakupa ruhusa kama utaendelea kufanya kazi bila ya malipo kwa kujitolea".

Mhe. Spika, hii ndio meli? Wazanzibari wanapewa meli hawana mkataba na bado meli hii inaambiwa salama. Mimi nasikitika sana kwamba mrajisi wa meli anaruhusu meli kuendesha bila ya mikataba ya wafanyakazi, leo Wazanzibari wanafukuzwa ovyo kwa sababu hawana mkataba, anakuajiri siku tatu halafu anakwambia nenda zako, hana mkataba ikitokezea ajali aende wapi.

Mhe. Spika, *Seagull* mwaka jana iliungua jenereta Pemba kama watu wangekufa kepteni angekuwa na jukumu la kujibu hoja hana mkataba. Mhe. Spika, mimi nasikitika sana kuona kwamba wizara hii ambayo Dkt. Karume aliiasisi watu wanaichezea. Mhe. Spika, naomba kauli ya waziri kuanzia leo lini atatuletea mkataba wa *Seagull* kwa ajili ya Wazanzibari vyenginevyo hii meli izuiliwe, kama ile haina mkataba wa wafanyakazi ina maana hii meli haifai kuendeshwa baharini. Kwa hivyo, atuletee mkataba hii leo au vyenginevyo meli hii izuiliwe kuchukua abiria na kufanya kazi Wazanzibari wetu.

Mhe. Spika, mwisho kabisa niseme kwamba, matengenezo ya MV. Jitihada 2.6 bilioni kwa mujibu wa magazeti si pesa kidogo. Hivi asubuhi nimekwenda pale bandarini kuiona ile meli kwa sababu nilikuwa sijaijuwa vizuri, nimeikagua kidogo na nimeona kweli imetengenezwa, lakini 2.6 bilioni kwa kutengeneza Meli ya MV. Jitihada ingawa ni ya nchi mtihani mkubwa. Mhe. Spika, lazima watwambie fedha hizi zimetengenezewa kwa viwango hivi na kwa madini gani, shaba, dhahabu au almasi.

Mhe. Spika, nasema kwamba mwisho kabisa wizara hii imeamua kuhamisha meli za mizigo Forodha Mchanga, pia nimekwenda hivi asubuhi nimekagua. Ni wazo zuri lakini pale wanapojenga hivi sasa wasi wasi wangu kuwa wataongeza msongamano wa abiria na watu.

Mimi Mhe. Spika, kabla ya kuwa mwakilishi niliwahi kuwa nahodha wa jahazi najua upepo wa kaskazi unapokuja lazima kunakuwa na mawimbi, pale ambapokuwa mmeweka ni sehemu mpya ya kuweka meli za mizigo basi pale mtasababisha ajali baina ya maboti ya watu binafsi na meli za mizigo hiyo. Naomba kujua nani atakuwa dhamana wa fidia ile ikitokea janga hilo.

Mhe. Spika, mimi naomba niseme kwamba, asubuhi niliwapigia simu watu wa Kiwani wakanambia kwamba sina ruhusa ya kuunga mkono bajeti hii na wasidhani watu wa mawasiliano kwamba sisi tunapopoa tu, sisi tunajua mengi sana ya mawasiliano. Kwa hivyo, wasitulazimishe kusema mengi kwa barabara moja. Tafadhalini nitoshelezeni barabara yangu vyenginevyo mnanipa mwanya niseme mengi kwa wizara hii.

Mhe. Spika, baada ya hayo siungi mkono hoja mpaka nipate maamuzi ya waziri.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu na wewe pia kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia na zaidi hasa Mheshimiwa ukaniachia nimalize dakika zote za mwisho.

Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na Naibu wake na Katibu na Wakurugenzi wake kwa utendaji wao mzuri sana. Mhe. Spika, unaweza ukavaa koti lakini kuna sehemu ndogo tu ikawa imejikunja isiwe kosa, lakini ni sehemu kubwa ya wizara hii matendaji yake tunayaona, wenye macho tunaona na wenye mapungufu ya macho wanaona, mimi sijamsikia mtu hata siku moja akaingia kwenye kidimbwi akajikwaa. Sasa hiyo niseme hivyo.
Lakini kwa kuendelea nimshukuru sana Mhe. Waziri katika ukurasa wa tatu na mimi kunikumbuka kwa kuniandika humu Mwenyekiti Makame Mshimba Mbarouk, hii ni moja ya shukurani kubwa sana tena kaniweka katika ukurasa wa tatu. Ni lazima nimsifu, vitanbu vingi sijaona hii kwa hivyo, lazima nichukue fursa hii ya kuweza kumsifu Mhe. Waziri wangu.

Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Zanzibar siku zote husema hakosei akichagua kitu, anachagua kitu kwa uhakika. Mhe. Waziri ana *experience* katika utendaji wake wa kazi akisaidiwa na kijana mdogo kabisa, mbichi, msimamizi wa kazi zake. Mhe. Spika, natoa hongera sana kwa Mhe. Rais kwa kumchagua Mhe. Waziri

wa Miundombinu na Mawasiliano kwa kutuletea humu Barazani, mambo mengi amebuni.

Mhe. Spika, nikiingia katika ukurasa wa 12 katika utekelezaji wa barabara. Kwanza niishukuru sana hii Kampuni ya *MECCO*, inafanya kazi kwa uadilifu mzuri sana na imo katika kuleta barabara zenye viwango na ndio maana utakuta waheshimiwa wengine wanapiga kelele katika maeneo yao kusema jamani ee, mnafanya matuta makubwa, lile sio tuta jamani lile ni moja katika kuufanya umahiri wa ile sehemu yenyewe ya barabara. Sasa kwa hivyo, Mhe. Spika, *MECCO* anafanya kazi kwa jitihada kubwa Pemba na Unguja tena kwa wakati.

Hivi sasa Mheshimiwa jinsi ilivyofanywa ile barabara utasema bora isitiwe lima hiki hiki kifusi kilichopo. Kwa sababu kile kifusi chake kinakuwa imara je ukimwaga lami itakuwaje? Sasa kwa hivyo, lazima nao tuwasifu sana hasa katika hiki kitengo cha mwenyewe Mkurugenzi Msimamizi wa Barabara.

Mkurugenzi huyu ana sifa mbili, sifa ya kwanza ni mtu ambaye anakupokea kwa ghuba na furaha kabisa na unaridhika ukienda katika ofisi yake, hii ni moja katika utendaji mzuri kiongozi kama huyu. Sifa ya pili ni mtendaji na msimamizi katika ufuatiliaji wake, ukimwambia kuna matatizo pahala fulani hataki kukujua wewe ni nani, anaheshimu madaraka yako anakwenda katika sehemu husika tena hachagui kama *feder roads*, *main road*, yeye yumo tu popote ukimwambia tu, twende zetu barabara yangu ya ndani ina hitilafu anakuja mbio, maporini tunampeleka.

Sasa hii ni moja katika sifa nzuri Mhe. Spika, na ndio maana ikawa barabara hizi zimo katika hali ya umadhubuti. Kwa hivyo, nimpongeze sana Mkurugenzi naye katika sifa zake hizo na Mwenyezi Mungu ambariki ampe na jengine zuri zaidi kuliko hili katika utekelezaji wake.

Mhe. Spika, tunapiga kelele sana humu waheshimiwa wenzangu, lakini wapi pa kugonga nyinyi hampaoni niulizeni mimi sasa nitakwambieni. Wizara hupata fungu kutumia katika Serikali Kuu, inapanga bajeti yake kwa mujibu wa sheria zake jinsi ambavyo malengo yake katika utekelezaji, lakini tuulize anapata asilimia kubwa? Hafiki asilimia kubwa na ndio maana kila siku tunagomba, tutawagomba mawaziri kila siku, lakini nani wa kumgomba tumkamate Mhe. Waziri wa Fedha. Zile bajeti ambazo wanazipanga wale mawizara basi ndio zile zile tuwatafutie tuwape, lakini hatimaye hawafiki tutawagomba kila siku jamani hawa na ndio maana Mheshimiwa aliyekaa kaonesha vitabu viwili anauliza lipi tulifuate kwa sababu gani? Ndio, anayekuja ana *plan* yake nyengine, lakini hamalizi lile kero la nyuma kwa sababu fedha yake aliyopewa ni asilimia ndogo na huyu atatekuja sasa hivi nae fedha yake ni ndogo kabisa. Sasa na sisi tunaangalia Mhe. Spika.

Nikiendelea katika jitihada za kuendelea kumsimu Mhe. Waziri katika kitabu chake, lakini kuna mambo mengine nitatoa ushauri. Idara ya Leseni na Usafiri ukurasa wa 21 hapa mimi siku zote husema kuwa makontena tuwawekee muda maalum wa kusafirisha, yanaleta hitilafu kubwa sana. Kwa sababu msongamano na yule dereva anakuwa chizi pale anaendesha mbio anavyotaka mwenyewe, anapita na kontena la 45 ni hatari. Hili mimi nimeshalisema, Mheshimiwa wangu hili naomba kabisa ushauri wangu tuwawekee muda maalum wa kuweza kusafirisha yale makontena ili kusitokezee matatizo ya kupatisha ajali. Ilitokezea kwa wenzetu Dar es Salaam hakutoka mtu hata mmoja baada ya kontena kuanguka. Kwa hivyo, tutahadhari kabla ya athari.

Mhe. Spika, nizungumzie ukurasa wa 31 Shirika la Bandari. Mhe. Spika, sifa yake lazima tumpeni. Katika watendaji wa Afrika Mashariki wanaopakua makontena ni mmoja katika *standard* akiwemo Mkurugenzi wa Bandari Zanzibar. Mhe. Spika, Zanzibar tunajichukulia sifa nyingi tu kwa mkurugenzi huyu, yakija pale makontena anamaliza anaondoka. Lakini tusikitike sana kuwa mkurugenzi huyu hana zana za kileo, ingekuwa ana zana za kileo basi nafikiri sifa zake zingezidi kuenea. Tunapata biashara sasa hivi kutokana na wepesi wetu wa kupakua makontena kutoka kwenye meli na kuweka juu. Mhe. Spika, nimpe hongera sana mkurugenzi huyu azidi kuendelea.

Mhe. Spika, zaidi pale watendaji wake makontena yakifika pahala fulani kila mtu anaambiwa chake kitu chukua. Mhe. Spika, msema kweli ni mpenzi wa Mungu, jitihada ya mkurugenzi wetu tunaiona ana asilimia 118 katika mambo ya upakuaji makontena.

Mhe. Spika, nizungumzie ukurasa wa 33 nikiendelea kumpa sifa Mkurugenzi wa Shirika la Bandari, tuna mainjinia wazuri sana katika sehemu yetu hapa Zanzibar. Mhe. Spika, niwapongeze sana vijana wetu wameanza tangu mkuku, maana yake wameanzia *frame* imetiwa pale na vijana wetu wadogo wazuri. Lakini tuone kuna mambo mengine hawa viongozi wetu wa shirika wanakuwa na mbinu za kutafuta mambo mengineyo ya kuweza kusaidia jambo lake liwe zuri. Sasa watu wanapiga kelele bilioni na nini, mkiona undani wake alichonunua mle ni mashine tu hakuna kitu chengine. Mashine nzuri kabisa *caterpillar* mimi sijapata kuziona. Nimekwenda China *NGN home* nimeangalia.

Mhe. Spika, mambo mengine huku anadai anaambiwa leo mzee hatukupi pesa lakini sema tukupe nini, wakati mimi nina tatizo nitasema. Kwa hivyo, huku anapata hichi na kule anapata hichi ndivyo tunavyokwenda hivyo. Leo tazameni ile pale MV Jitihada ni nzuri kabisa *Alhamdulillah,* tukitaka tusitake watoto wetu wa Kizanzibar ndio waliofanya kazi ile.

Mhe. Spika, suala la chelezo la ile gati ya *land craft.* Mhe. Spika, nimpongeze sana Meneja wa Shirika la Bandari kwa sababu kafanya kitu cha uchungu kwa kuifanya ile *land craft* ikakae pale hakukosea. Mhe. Spika, kuna mambo mengine wazungu wanaweka mambo *special* kwa kazi yake, akipita mtaalam akaona tunaharibu jambo tunakwenda kufanya pahala ambapo hapahusiki na kuweka gati. Wewe umeona wapi forodha mchanga na gati hebu nambieni. Mhe. Spika, ile ni stone town bwana ina haiba yake, tena Mhe. Ismail Jussa Ladhu usikubali unaharibiwa mandhari yako. Lakini leo tunakwenda kuifanya stone town pale vurugu mechi hajulikani nani mchukuzi.

Mhe. Spika, nampongeza sana Meneja wa Shirika la Bandari. Watu wanasema pale pana msongamano si kweli, kaweka njia ya kuingia na njia ya kutoka. Mtoto *serious* yule bwana, hakupata kazi jana na leo pale, mimi namjua tangu alikuwa *pilot,* anaingia Shirika la Bandari ilikuwa chini juu. Kwa hivyo, hakuna hitilafu yoyote pale tunalaani tu kwa mambo yetu.

Mhe. Spika, ukiangalia watu wanakimbia ushuru hatulioni hili hatulisemi. Hata mimi kama mfanyabiashara wangu nitakuwa sisemi nitabana na ndio ukweli ulivyo wanapitisha magari mengine pale hawalipi ushuru. *Audhubillah min dhalika* mambo mengine yanaweza yakapitishwa pale pale sisi hatuoni, *security* hakuna pale halafu unaturuhusu tu haiwezekani hichi kitu. Ni lazima wawepo pale pale kwa sababu pale pana *security* wala hakuna purukushani yoyote. Mhe. Spika, mimi nasema kabisa siwazi.

Mhe. Spika, nikija Shirika la Meli kwanza nimsifu sana Mhe. Mwenyekiti wa Bodi, Mhe. Ali Mzee Ali jamadari, ahsante. Mhe. Spika, mimi siku moja nilisema suala lile la Mambo Msiige ilipoondoshwa kuna fedha zilitolewa shirika hili halikupewa na ni kweli. Hawakupewa pesa zao za kutengeneza ofisi yao. Sasa naomba Mhe. Waziri wa Fedha hayupo hapa awape pesa zao wametengeneza pesa hizi ndio mambo kama haya. Bajeti iliyokusudiwa inakuwa haitengenezeki inatengenezwa bajeti nyengine hatimae tunakuja tunasema hapa kumbe hatujui. Sisi tunakwenda kamati tunajua tuulizeni tukwambieni.

Sasa hiyo Mhe. Spika, kuwa MV Mapinduzi imeuzwa fedha hawajapewa mpaka leo. Kesho kutwa tunachuma karafuu utaipeleka wapi, haiwezekani kutiwa kwenye meli nyengine kwa sababu karafuu tunailinda ili isipotee. Kwa maana hiyo, naiomba serikali iwatafutie meli haraka sana kabla ya mavuno ya karafuu kuanza.

Mhe. Spika, fedha hizi wapewe wenyewe zile za MV Mapinduzi waliouza watie kwenye akaunti yao. Mhe. Spika, naamini bodi ilikubali suala hilo, lazima itakuwa bodi walikubali wanapopata zile fedha wazitie kwenye akaunti

ya Shirika la Meli, sidhani kama mpaka leo fedha hizo zimo. Mhe. Spika, naomba kuwa hizi fedha waingiziwe wao wenyewe waweze kununua meli kwa kuweza kubeba karafuu zetu zisije zikapotea. Hizi fedha za Mambo Msiige walizopewa pale wapewe wenyewe ili waweze kufanya shughuli zao.

Mhe. Spika, mimi leo sitokuwa na mchango mkubwa, lakini kuna kitu kimoja kwa idhini yako kwa makusudi naomba hicho kitu nikieleze si dhambi hata kidogo. Mhe. Spika, jana katika kupitisha hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuna kitu nilikaa nyumbani nikaangalia sana kwenye buku la makisio sikukiona. Najua si utaratibu lakini kwa idhini yako ni jambo zuri tu na watu wengi watalipongeza suala hilo sio baya. Sikuliona fungu la Shirika la Umeme kwenye buku kuu sijaliona sasa sijui fungu lile limekwenda wapi.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo atakapokuja kuchangia wizara hii anieleze hili suala la fungu la Shirika la Umeme liko wapi, mbona kwenye buku kuu halimo.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nimpongeze tena wala si dhambi mheshimiwa wangu kwa jina jengine Magufuli. Mhe. Spika, nimemwita Magufuli kwa sababu ni mtu ambaye anakijua kitu kabla, wewe ukianza swali tu ameshakijua zamani anakujibu. Kwa sababu yule waziri wa kule Mhe. John Magufuli ana *experience* ya kazi yake na huyu wetu wa Zanzibar ana *experience* ya kazi yake.

Mhe. Spika, kwa hayo machache nawaomba wajumbe wenzangu tuichangie hii bajeti kwa vizuri. Ametuaidhi Mhe. Spika, twende katika pointi na tuseme kile kitu kisichokuwa na dhana. Kwa sababu hii ni hatari baadae mtu kapigwa buti utafute ushahidi huna ushahidi, bora ya jitihada imekwenda kwa utaratibu inavyotakiwa. Mhe. Spika, naunga mkono hotuba ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia kwa mia pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa fursa hii ya kuweza kuichangia hotuba ya Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye leo ametuwezesha kuja hapa tukiwa na afya njema na uzima na kuweza kusimama hapa tukalitumikia taifa letu.

Mhe. Spika, sina budi kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutuletea hotuba nzuri ambayo ina muelekeo mzuri, naamini kwamba

muelekeo wa hotuba hii utatupeleka pale ambapo tumekusudia na pale ambapo tutakuwa tunawatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi nitaanzia ukurasa wa 14 kwenye Mradi wa Barabara Kuu ya Zanzibar. Mhe. Spika, mimi ni mwananchi ambaye naishi Mwera na sasa hivi kuna ujenzi wa barabara ya Dunga/Amani. Barabara hii sasa hivi imeshakuwa ni kipindi kirefu sana iko katika ujenzi. Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwa sababu barabara hii ujenzi wake unakwenda kwa kasi, lakini kipindi kirefu sana ilikuwa ni kero kwa wananchi, ndio maana wakati mwengine huwa nachelewa. Kwa kweli mara nyingi unasimamishwa njiani ili angalau wa upande mwengine waweze kupita halafu upite wewe.

Lakini Mhe. Spika, barabara hii mimi naamini kwamba itakuwa bora kwa sababu unaona hasa mara kwa mara hata ukifikiria tayari imemalizika kumbe haijamalizika, linaletwa fusi jengine unakuja utaalam mwengine. Mhe. Spika, nawashukuru sana wamezingatia suala zima la maji kwa sababu mara nyingi sana barabara zetu zinaathirika kwa maji. Lakini nimeona hata pembeni ya hizi barabara tayari wameanza kuchimba misingi na kutia mapaipu makubwa ambapo maji yale yatajikusanya yatakwenda kwenye mabonde yanayolimwa mipunga.

Mhe. Spika, ingawa nasikitika na nawaonea huruma wananchi ambao wamejenga katika mabonde kwa sababu naamini kwamba wakati mvua zitakaponyesha maji yale yote yaliyokusanywa kutoka kwenye barabara yatakwenda kwenye mabonde na yataathiri nyumba zao. Sasa sijui Wizara italifikiria vipi suala hilo.

Mhe. Spika, kuna suala la usalama wa raia ambalo nimeona ni muhimu sana kulizungumzia. Mhe. Spika, barabara hii inapita gari nyingi sana zikiwemo gari za abiria za kwenda shamba mbali mbali kama vile Chwaka, Dole, Uroa, Kiboje na nyenginezo. Lakini hii barabara sasa hivi imekuwa inatumika sana, halafu iko katika eneo ambalo wanaishi watu wengi na kuna watoto wengi ambao wanakwenda skuli wakirudi. Mhe. Spika, nina wasi wasi barabara hii itakuja kuleta maafa mengi.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri ahakikishe kwamba anachukua jitihada ya makusudi ili barabara hii iwe ni barabara ya salama. Kwa sababu tunajua gari zetu hasa za abiria namna zinavyokwenda mbio, hivi sasa ninavyokwambia juu ya kwamba kunafanywa ukarabati lakini gari za abiria zinakwenda mbio, zinatifua vumbi na nakuhakikishia kwamba baada ya muda wa miaka fulani pale tutakuja kupata wagonjwa wengi sana wa vifua kwa sababu vumbi limekuwa jingi.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri aitazame tena barabara hii kuhakikisha kuwa vituo vya daladala vinawekwa, sijaona kama kuna mpango wowote ambao utahakikisha kwamba kuna vituo vya daladala na usimamizi wa gari zile ovyo ovyo unasababisha ajali. Mara nyingi sana barabara zetu tunazijenga lakini tunasahau ujenzi wa vituo vya daladala. Vituo ni moja katika mbinu ya kuhakikisha kwamba kuna usalama wa magari yanayopita kwenye njia zile. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kama kutakuwa na mradi mwengine basi mradi wa kujenga vituo katika barabara zetu kuu vituo vya daladala uwepo.

Mhe. Spika, pia nizungumzie suala la Uwanja wa Ndege. Mhe. Spika, nimefurahi sana kwamba sasa hivi serikali imeona umuhimu wa kujenga katika sehemu ya *terminal*. Sasa mimi nimeona kwamba itajenga terminal, nimeona kuna picha huku nyuma ambayo inaonesha kwamba terminal yetu itakuwa nzuri kiasi kutegemea na uwezo wetu, hatuwezi kujifananisha na nchi nyengine ambazo wao wana uwezo mkubwa sana wa kiuchumi.

Mhe. Spika, hata hivyo, mimi nilitarajia Mhe. Waziri pamoja na kwamba ametuonesha hii picha lakini angalau angetuletea picha nyengine tukaona ile *interior design* ya hili jengo. Kwa sababu tunataka na sisi tujue tutoe mchango gani katika kuhakikisha hili jengo letu ambalo tunalitegemea kiuchumi kuwa ni *entry point* ya wageni wetu wengi wanaoingia hapa Zanzibar kwamba linatimiza vigezo vya kimataifa.

Mhe. Spika, mara nyingi sana tumekuwa tunakosea katika ujenzi wetu na makosa hayo yanajitokeza katika majengo mbali mbali. Mhe. Spika, pia tungepata kujua *capacity* ya jengo hili litachukua abiria wangapi ili tujue kwamba sio tu tunasema tunahesabu ndege ngapi zitakuja.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa nizungumzie Shirika la Bandari. Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk amelisifu sana shirika hili na mimi sina budi kuchukua nafasi hii kulisifu shirika hili. Kwa kweli linafanya kazi nzuri na hatuna budi kwa sababu mara nyingi unapoona mambo yanakwenda vizuri ujue kwamba ni kiongozi mzuri. Inapendeza kuwa shirika hili lina kiongozi mzuri pia lina wafanyakazi wazuri. Mhe. Spika, niwape pongezi wafanyakazi wa shirika hili kwa sababu wanafanya kazi nzuri na kwa nidhamu.

Mhe. Spika, kuna baadhi ya wafanyakazi wa Shirika la Bandari kwa kipindi kirefu sana wamekuwa ni waajiriwa wa kibarua *(daily paid).* Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri awatengenezee mpango maalum wafanyakazi hawa huku akishirikiana na Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hawa wafanyakazi wamekuwa pale kwa kipindi kirefu wengine zaidi ya miaka 10, kwa kweli kama raia wa Zanzibar tutakuwa hatuwatendei haki.

Sasa Mhe. Spika, ningeomba tuwatazame wale kwa jicho la huruma kwa sababu kuna haki zao wanazikosa. Mhe. Spika, namuomba Mkurugenzi wa Shirika la Bandari kwamba juu ya kuwa kazi zake anazifanya vizuri na wafanyakazi wake wanafanya kazi vizuri, basi awatazame kwa jicho la huruma wafanyakazi hao.

Mhe. Spika, jengine ni lile eneo ambalo meli au abiria wanaondoka kwa kusafiri kwenda Pemba au Tanzania Bara. Mhe. Spika, sijui uwezo wetu ulikuwa ni mdogo au sijui ni kigezo gani ambacho kimefanya lile jengo la watu wanaposubiri usafiri likawa dogo. Tufanyeni *extension* kwa sababu lile sio la zamani sana, tufanyeni research tujue ni meli ngapi zinaingia wakati gani na watu wangapi. Kwa sababu mara nyingi ukenda pale unakuta watu wamesongamana, wengine wamekaa njiani, panakuwa hapana *discipline,* lakini hiyo haisababishwi na wale abiria inasababishwa na mpango wetu uliokuwepo pale.

Mhe. Spika, ningeshauri kwamba ile sehemu iongezwe kama upo uwezo huo kwa sababu naweza kusema mimi lakini sijui kama uwezekano huo upo. Lakini mimi ningeshauri hata tutazame kwa baadae, inawezekana leo haupo lakini baadae ukawepo uwezo. Tuwe na mpango wa kupaongeza pale na kufanya sehemu ambayo inaweza ikatoa huduma zote, zikiwemo huduma za chakula, halafu pia tuwe na huduma za vyoo. Pale pana choo kimoja cha wanawake na kimoja cha wanaume, lakini ukenda unaweza ukakuta foleni ndefu sana. Nafikiri watu wa afya watakubaliana na mimi kwamba sio vizuri sehemu kama ile ambayo ina abiria wengi lakini choo kikawa kimoja. Kwa hivyo, naomba tuliangalie hilo kwamba kuna umuhimu pale wa kuwa na huduma za lazima.

Mhe. Spika, naomba tena nitoe pongezi zangu maalum kwa Mhe. Waziri kwa sababu amekuwa sio tu waziri lakini amekuwa ni mtu msikilizaji na mtatuzi wa matatizo ya watu wengi. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ukimwambia leo nina shida anakwambia nitakusaidia. Nampa hongera sana Mhe. Waziri, naomba aendelee hivyo hivyo na Mwenyezi Mungu atamjaalia yeye na Naibu wake kufanya kazi zao kwa ufanisi na ubora na kwa ajili ya taifa hili.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, naiunga mkono hotuba kwa niaba ya wanawake wa Unguja na Pemba asilimia mia moja. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, sina budi kumshukuru *Allah* kunijaalia na mimi kupata nafasi hii ya kuchangia kidogo katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, nitaanza katika ukurasa wa 16 kifungu cha 37. Mhe. Spika, kuna mradi wa barabara tatu Pemba. Kwanza sina budi na mimi kuipongeza wizara

kufungua macho yake yote mawili kuondosha tatizo hili la usafiri kwa barabara hizi pale Wete/Konde/Gando na nyengine. Mhe. Spika, hili limekuwa ni tatizo la muda mrefu usafiri wa kutoka Wete hadi Konde. Mhe. Spika, barabara hii ilikuwa ina hadhi kubwa hapo asubuhi lakini umeshakuwa ni muda mrefu hata zile gari za abiria zimekosekana katika barabara hii. Kwa hivyo, sina budi na mimi kuipongeza wizara kwa kuliona hili na umuhimu wake.

Mhe. Spika, katika umalizaji wa hii barabara kasi yake imekuwa ni ndogo sana na itachukua muda mrefu bado barabara hii haijafikia kile kiwango ambacho wamekusudia. Lakini pia tunahofia kwamba ule uwekaji wao wa kifusi kwa kweli kifusi kingi kinapotea barabarani na kinaanza kusambazwa na maji kupelekwa katika maeneo ya mashamba ya watu. Hili Mhe. Spika, kama wizara haitaliangalia barabara hii hata itakapomalizika basi tutapata uchafuzi mkubwa wa mazingira katika maeneo haya yanayochimbwa kifusi.

Mhe. Spika, kwa taarifa ya Mhe. Waziri anasema bado kama kilomita moja kukamilisha umwagaji wa kifusi katika barabara ile. Lakini pia kuna kilio cha wananchi kwamba wale ambao wamepitiwa na barabara baadhi yao malipo ya vipando vyao hawajapata na kwa kweli wananchi wetu wapo katika hali ngumu ya maisha. Pale wanapoambiwa watalipwa basi ile roho yake huleta tamaa nzuri kwamba leo kesho nitafaidika katika kipando changu kile. Lakini wanakata tamaa kwamba hadi hivi sasa hawajapata mafao yoyote baada ya kupitiwa na barabara hii.

Mhe. Spika, ukurasa wa 17 kuna mradi huu wa barabara vijijini Kaskazini Pemba. Pia nashukuru sana kwamba kuna barabara karibu tano hapa wizara kwa kupitia mfuko wa *MCC* kwa kweli umefanya jambo moja la maana sana katika barabara hizi za ndani ambazo ni usumbufu mkubwa wanaopata wananchi wetu kwa muda mrefu. Mhe. Spika, barabara hizi zina umuhimu wake kwani ni maeneo yanayozalisha uchumi wa Zanzibar, karafuu nyingi zinapatikana katika maeneo haya yatakayopita barabara.

Mhe. Spika, pia nimuombe Mhe. Waziri hii barabara inayotoka Pandani/Finya, pale Finya kuna barabara inayotoka Finya kuelekea Shumbaviamboni/Chimba kwa kuunganisha barabara ya Piki. Hii barabara mara nyingi inasemewa na viongozi mbali mbali, hata Mhe. Rais hivi karibuni alipokwenda kufungua jengo la hospitali pale Tumbe barabara hii pia aliisemea. Barabara hii ni miongoni mwa barabara zinazozalisha uchumi wa nchi yetu ya Zanzibar, lakini ni suala la muda mrefu barabara hii haijaangaliwa kwa jicho la rehema.

Mhe. Spika, kama mwaka huu imekosekana hii barabara kutengenezwa basi ningemuomba sana Mhe. Waziri ajaribu angalau kwa hatua za mwanzo

kumwaga fusi katika yale maeneo ambayo yanaleta usumbufu kwa wananchi wetu wanapochuma zao lao la karafuu kuweza kuzifikisha kule kunakohusika.

Mhe. Spika, pia katika barabara hizi zitakazojengwa kuna eneo la Mzambarauni Mapofu, hapo Mapofu pia pana njia inayoingia katika Jimbo la Tumbe na ndio kiunganishi kikubwa sana kufikia maeneo hayo ya Shumba Viamboni. Mara nyingi wenzetu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kila kipindi cha mvua hujaribu kuchukua kifusi kwenda kumwaga katika barabara hii kwa sababu wakubwa wengi wanapita.

Lakini Mhe. Spika, umwagaji huu wa kifusi mimi nahisi kwamba hauna maana yoyote kwa sababu fusi linapelekwa lakini hakuna chombo chochote kinachokwenda kukishindilia kile kifusi. Kwa hivyo, zikimalizika tu mvua basi na kifusi kile kimemalizika, inakuwa kodi ya wananchi pale inapotea ovyo kabisa.

Kwa hivyo, ningemshauri sana Mhe. Waziri tatizo hili aliangalie, kama kweli wamekusudia kuziba maeneo ambayo yanahatarisha vyombo vya moto, basi wahakikishe wanapeleka kile kifusi na kukishindilia. Tena namuomba sana Mhe. Waziri na kwa mara hii wakati hii barabara imo katika mpango wa mwaka 2012/2013, basi na barabara hizi angalau wazitupie macho ili ziondokane katika yale maeneo ambayo yanahatarisha vyombo vya mashine na wananchi wetu. Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri atuonee huruma katika maeneo haya.

Mhe. Spika, pia pale *COGEFAR* kuelekea Tumbe Bandarini. Tunashukuru kwamba serikali ya awamu hii ya saba ina mpango endelevu sasa unaendelea wa kujengewa soko la samaki pale Tumbe. Lakini Mhe. Spika, kutoka hapa COGEFAR kuelekea huko Tumbe kwenye soko ambako kutakuwa na kitega uchumi na watu wengi ndio wanakwenda huko, kuna usumbufu mkubwa wa kufikia katika maeneo hayo. Hakuna barabara, barabara ilioko ina mashimo makubwa kabisa. Kwa kweli uchumi huu tutakaouanzisha utakuwa na usumbufu kwa kiasi fulani.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri ili kufanya harakati za uchumi zikuwe haraka na samaki waweze kufikia katika maeneo ambayo wanahitaji kutumiwa, basi ni kuifanyia upembuzi hii barabara ili iweze kuleta tija haraka na yale maendeleo tuliyokusudia yaweze kupatikana kwa haraka iwezekanavyo.

Mhe. Spika, nimesema kwamba sitakuwa na mchango mkubwa, lakini nitazungumza kidogo katika sekta hii ya usafiri wa barabarani. Mhe. Spika, kwa kweli hili ni tatizo moja kubwa kabisa katika visiwa vyetu vya Zanzibar.

Usafiri hapana bwana. Usafiri uliopo ni mbovu kabisa. Kwanza wananchi wetu wanachukuliwa tu kama mizigo hakuna idadi maalum, ukiangalia sasa hivi vyombo vyote havisafiri tena mchana, meli zote zinafanya safari usiku, maana yake ni nini. Maana yake ni vibovu. Kwa hivyo, kumchukua mtu saa mbili za usiku hapa hata akifika Pemba kule anafika saa 12:00 za asububi kwa sababu ya vyombo vyenyewe havijiwezi.

Mhe. Spika, halafu watu wanaoingizwa humo kwenye meli ni wengi. Mwenyezi Mungu apitishe mbali, lakini ikijakutokea ajali inakuwa ni hatari ilioje Mhe. Spika. Kwa hivyo, tunaiomba sana wizara suala hili alihangaikie haraka, watu wamechoka kukaa kwenye bahari muda mrefu. Kwa hivyo, wanahitaji wafanyiwe usafiri ambao wataweza kufika katika maeneo yao bila ya kupata usumbufu mkubwa.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi naomba kuwa mara moja ufanye safari ya kwenda Pemba, upande hizi meli wanazopanda abiria wetu ndipo utakapofaidi hali halisi ya wananchi wetu wanaofikwa na matatizo makubwa. Watu hujaa hata pakuweka mguu inakuwa ni tatizo. Lakini ukiuliza kwenye wizara utaambiwa, tunachukua watu mia 300 au mia 400. lakini Mhe. Spika, sio kweli, watu wanaoingizwa ni wengi mno.

Mhe. Spika, ningemuomba sana Mhe. Waziri upatikanaji wa tiketi, suala hili lishughulikiwe. Tiketi haziuzwi tena katika shirika, tiketi zinauzwa vibandani. Kule kwenye ofisi zao zinauzwa tano na zilizobakia zinauzwa mikononi tu, sasa inakuwa ni tatizo mwananchi wetu kuweza kumiliki ile pesa utakayoambiwa pale kwenye zile za kuuzwa mikononi. Kwa hivyo, bado kama tuna malengo ya kuwaondoshea wananchi wetu matatizo basi na suala la kupatikana kwa tiketi lipatiwe ufumbuzi ili wananchi wetu wasipate matatizo kama haya.

Mhe. Spika, Mkoani pale Bandarini, Mhe. Raya hapa alisema. Mhe. Spika, pale pana matatizo sugu, nidhamu imepungua, hajulikani mkubwa wala mdogo. Kwa hivyo, hili ni tatizo. Hivi karibuni tu Mhe. Spika, kiliharibika kile kifaa cha kubebea mizigo kikasimama katika njia za kurejea magari yanayotoka kule bandarini. Chombo chenyewe kidogo, huwezo wa kusukumwa kikapakiwa pengine upo, lakini karibuni mwezi kimesimama njiani, abiria na magari ya kwenda na kurudi yote yanapita njia moja. Kwa kweli ile ni njia moja ya kuhatarisha maisha ya wananchi wetu. Kwa hivyo, masuala mengine madogo, lakini ufuatiliaji wake unakuwa ni tatizo watu wetu hawafanyikazi vizuri na wanawasababishia wananchi wetu kupata usumbufu wa hali ya juu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, hili pia ningeliomba sana kwamba wizara isimamie matatizo yake. Wenzangu wameisifu sana Wizara hii ya Miundombinu na

Mawasiliano. Ni kweli wanajituma lakini kuna mambo mengine madogo madogo, kwa sababu kila unapolidharau jambo dogo hatima yake ndio linakuwa kubwa. Kwa hivyo, ningewaomba sana ili kuweza kuyatatua matatizo basi tusiyadharau. Kwa sababu waswahili wanasema kila mdharau mwiba mguu huota tende.

Mhe. Spika, mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Tumbe, tunaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia fil mia na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu awape moyo wa kuweza kumaliza matatizo ya Zanzibar, ahsate sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa ya kuweza kutoa mchango wangu katika hoja ilioko mbele yetu. Awali ya yote Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu kuweza kumpongeza Mhe. Rais Dk. Ali Mohammed Shein kwa kuweza kutuchagulia vijana hawa, Mhe. Hamad Masoud kuwa Waziri na Mhe. Issa Haji Gavu kuwa Naibu Waziri wake.

Kwa kweli Mhe. Rais amesibu kuwateuwa vijana hawa. Mhe. Spika, naomba unipe dakika mbili nieleze wasifu wao hawa. Ukiwaangalia Mhe. Issa Haji Gavu na Mhe. Hamad Masoud utawaona ni wanasiasa wa kawaida tu kama hivi nilivyo mimi. Mhe. Spika, hawa vijana Mwenyezi Mungu kawajaalia vipaji vitatu vikubwa.

Kwanza wana ulimi wa fasaha wa kuweza kujibu hoja zetu humu ndani kama vile mwalimu anavyomsomesha mwanafunzi. Wasifu wa pili wana ubongo wa hekima wote wawili kwa pamoja wa kuweza kubuni miradi ya maendeleo katika wizara yao. Wasifu wa tatu Mhe. Spika, wana moyo wa kuweza kuhifadhi siri za serikali hii pamoja na wizara yao kama vile kaburi linavyohifadhi maiti.

Baada ya tanbihi hiyo Mhe. Spika, naomba sasa niende moja kwa moja kwenye hoja ilioko mbele yetu. Mhe. Spika, kwanza nianze na hii sekta ya usafiri wa nchi kavu. Kwa kweli Mhe. Spika, wizara hii imekuwa makini sana katika kusimamia usafiri wa nchi kavu kwa kuhakikisha kwamba miundombinu ikiwemo barabara na daraja hasa zile za vijijini, aidha zimo katika mipango au zinafanyiwa ukarabati wa hali ya juu, ili kurahisisha mawasiliano baina ya vijijini na mijini, hili nawapongeza sana.

Mhe. Spika, baada ya kukisoma kitabu hiki cha hotuba ya Mhe. Waziri. Sitaki niseme kadharau, lakini nafikiri wamesahau kidogo, kwa sababu katika Jimbo langu la Wawi kuna barabara muhimu sana ambazo sio tu kwamba zina changia maendeleo ya wale watu wa pale Wawi na Chake Chake, lakini hata kwa maendeleo ya Zanzibar nzima.

Mhe. Spika, kuna barabara hii inayotoka sehemu ya Vikunguni mpaka Matrekta Wawi pale ni kiunganishi baina ya Vikunguni na Matrekta. Vikunguni wanalima sana ndizi ni wakulima wazuri sana wa ndizi jamaa zangu wa Vikunguni, wapiga kura wangu na wanachangia asilimia sabini ya ndizi zinazopelekwa katika soko la Chake Chake na karibu asilimia 20 ya ndizi zinazoliwa hapa Unguja mjini. Lakini barabara yake ni mbovu sana na iliwekewa ahadi na Mhe. Rais wetu Mstaafu wa Zanzibar Mhe. Aman Abeid Karume, aliiwekea ahadi wakati akitowa zawadi kwa skuli bora ile ya Vikunguni, kwamba ataijenga kwa kiwango cha lami. Lakini Mhe. Spika, barabara ile kwa masikitiko makubwa haipitiki. Siku za mvua ni Vikunguni ni kisiwa hakupitiki, ndizi zinaiva kule wakati watu wa Unguja wanataka kuzila, wakati watu wa Chake Chake wanataka kutumia ndizi zile basi zinabakia Vikunguni kuoza.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri aiangalie hii barabara ilioanzia hii njia iliopo karibu na kituo cha kilimo karibu na Ole hadi kupitia Vikunguni mpaka Matrekta ni barabara muhimu sana kwa maendeleo ya nchi hii. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri barabara ile haizidi kilomita 2 na wakati Mhe. Rais keshaiwekea ahadi jamani, ile ahadi ya Rais imesibu, tuitekelezeni.

Jengine Mhe. Spika, kuna barabara moja inayounganisha kutoka Vikunguni kupitia Skuli ya Ng'ambwa hadi uwanja wa mpira wa Gombani. Barabara ile ni muhimu sana lakini humu sikuiona. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri ajitahidi sana kuitupia jicho ni barabara ambayo inawaunganisha sana watu wa Wawi barabara hii. Mhe. Spika, naomba barabara hii ya kutoka Vikunguni kupitia Skuli ya Ng'ambwa na kupitia Gombani ya Kati hadi uwanja wa mpira Gombani aiangalie sana.

Vile vile Mhe. Spika, kuna barabara ya kipande cha kilomita moja ambacho ni muhimu sana, kuanzia pale Dodeani hadi katika Mgodi wa Matofali. Kuna Mgodi wa Matofali kule Uwandani, ambapo Pemba nzima wanachukua matofali kutoka Uwandani. Siku za mvua watu hawapati kwenda kununua tofali kule. Kwa kweli Mhe. Waziri mgodi ule ni muhimu. Mimi napinga kwamba wanaochimba matofali eti wanaharibu mazingira. Hawaharibu mazingira, wale wanatunza mazingira. Wachimba matofali wa Uwandani wanahifadhi mazingira kabisa Mhe. Spika, naomba uniruhusu dakika moja tu nieleze. Kabla ya kuanza uchimbaji wa matofali Mhe. Spika, watu wa vijijini kule Pemba nzima walikuwa wakijenga kwa miti na nyumba moja inakula heka mbili za miti, nyumba moja tu kuijenga inakula heka mbili. Sasa ulipokuja mradi ule wa matofali, watu hawakati tena miti, wanajenga kwa matofali wale. Kwa hivyo, uhifadhi wa mazingira umepatikana.

Mhe. Spika, naomba kile kipande cha kutoka Dodeani mpaka katika Mgodi wa Matofali kule basi kijengwe kwa kiwango cha lami kusudi watu wa Jimbo la Ole, Jimbo la Chonga na Pemba nzima waweze kujengea matofali yale, katika hali ya kuhifadhi mazingira.

Mhe. Spika, sitaki niondoke katika sehemu hii. Nataka nizungumzie kuhusu hawa jamaa zangu wa UUB wanavyochukua vifusi jinsi wanavyoathiri mazingira. Mhe. Spika, jamaa hawa wa ujenzi wa barabara wanachukua kifusi sana kutoka Makaani Vitongoji kule, wanachimba mashimo makubwa mno, mengine yameshazua chumvi sasa hivi, wametengeneza bahari kule watu wa UUB. Kila mradi kwa mujibu wa taarifa niliyonayo ni kwamba mradi wowote wa barabara unatakiwa uchangie asilimia 10 ya mradi ule ili uweze kuhifadhi mazingira. Lakini miradi yote inayokuja Pemba, kifusi kinachukuliwa Vitongoji, wanachimba mashimo hatujaona hizo asilimia 10, asilimia 10 hizo zikowapi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri katika maelezo yake aje aniambie yale mashimo yalioko Liko la Vumba, yalioko Liko la Mjini na yalioko Liko la Makoba ambayo yamesababishwa na uchimbaji wa kifusi katika kuleta maendeleo ya barabara, sasa asilimia 10 zile hazikutolewa au zinamezwa pahala hizi. Naomba anieleze Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, sasa niende katika suala zima la Idara ya Usafiri na Leseni. Mhe. Spika, hapa napenda kwanza niwapongeze wanajitahidi sana, lakini nina mambo madogo tu. Ili upate leseni ni lazima uwende katika skuli ya udereva. Sasa Mhe. Spika, mimi nimefanya utafiti wa kina. Naona hisi skuli za udereva zinamilikiwa na watu binafsi tu na wengi wao ni wafanyakazi wa hapa hapa mawasiliano je, kuna siri gani hapa, napata wasi wasi. Hasa nikiona vitoto vidogo sasa hivi wa umri wa miaka 15, 18 au 20 vinatuendesha mule barabarani.

Nataka anieleze Mhe. Waziri je, wizara yake imeamua kutukia skuli hizi kwa kuwapa wafanyakazi wao tu au kila mtu anaweza kuanzisha. Halafu nataka nijuwe vile vile wanapowataini hawa wanafunzi wa udereva mitihani yao kila skuli inatoa mtihani wake au wizara yake ina *monitor* ya kufuatilia usaili. Kwa sababu huyu anaweza akasaili hivi na huyu akasaili hivi na matokeo yake tukawa na tofauti za viwango vya madereva, jambo ambalo linaweza kutusababishia ajali. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri hizi skuli za madereva ziwe-*centralize*, yaani hiyo mitihani yao iwe-*centralize.* Ikiwa kila mtu anaruhusiwa kufanya yake, basi unaweza kuambiwa usome miezi sita ukishakupeleka Shs. 40,000/= ukapewa cheti pale ukenda kuchukua leseni, jambo ambalo ni tatizo. Kwa hivyo, tunaomba mu-*centralize* hii *system* ya usomeshaji. Hilo ni jengine Mhe. Spika.

Mhe. Spika, sasa niende moja kwa moja katika usafiri wa baharini. Mhe. Spika, Unguja na Pemba ni visiwa, ni visiwa na kwa kiasi kikubwa vinatumia usafiri wa bahari. Napenda niwapongeze viongozi wetu wa awamu ya kwanza na awamu ya pili, wametuachia Shirika la Meli likiwa madhubuti mno. Mzee Karume kafariki hapa katuachia meli ya Jamhuri na Afrika na zilitosha kabisa kwa wakati ule kuhudumia wananchi. Alipokwishafariki Mzee Karume, akaja Mhe. Abdu Jumbe akatumiminia Meli ya Mapinduzi na Meli ya Maendeleo, MT Uhuru na MT Ukombozi. Kwa kweli meli mbili hizi zimetusaidia katika kipindi kirefu sana. Hivyo napenda niwapongeze waasisi wa awamu ya kwanza na awamu ya pili kwa kujali maisha yetu.

Mhe. Spika, ilipoingia awamu ya tatu sasa, meli moja baada ya nyengine ikaanza kuuzwa. Ikaanza kuuzwa Afrika, ikaja Jamhuri na sasa sijui imeshauzwa Mapinduzi, tunaambiwa eti ipo Maendeleo iko wapi, mbona haiji Pemba. Mimi nataka waziri aniambie hii Maendeleo iko wapi na tumeinunua kwa pesa za walipa kodi. Tunaambiwa ipo. Mara iletwe Nura, viboti uchwara uchwara tu, wakati meli ya serikali ipo. Mara Buraki I, Buraki II. Zisekeseke unakuja Unguja kwanza zipige tanga. Jamani mtaendelea kutuuwa. Ikiwa meli yetu ipo ya Maendeleo tunataka itowe huduma baina ya Unguja na Pemba, baina ya Unguja na Dar es Salaam, baina ya Pemba na Tanga, tunataka huduma hiyo.

Mhe. Spika, kwa kweli katika shirika ambalo sasa hivi linaendeshwa kienyeji ni Shirika hili la Meli. Usafiriwa baharini hauna uangalizi. Hawa ni mahodari kwa kusimamia usafiri wa barabarani tu, ukipita *traffic* hapa atakusimamisha, pale akusimamishe tena, hujatembea hata kilomita mbili utasimamishwa tena. Lakini mameli yanasekaseka baharini usiku na mchana wala hayasimamishwi wakaambiwa tutakunyang'anya leseni meli yako ni mbovu, hawasimamishwi kuna siri gani hapa.

Mhe. Spika, walipa kodi wa nchi hii wana matatizo sana na usafiri wa baharini. Kila mwaka sisi Wapemba tunakufa pale, tukisafiri kwenda Tanga na Pemba kila mwaka tunakufa. Hivi sasa upepo umeshaanza basi tumeshaanza wasi wasi. Mhe. Spika, tunaomba utuokowe ajira hazipo, Wapemba wanatoka Pemba wanakwenda kununua nyanya kule Tanga na Viazi wanafanya biasha na kuweza kuishi. Lakini leo hawana usafiri na kwa bahati mbaya shirika hili haliwezi ku-*monitor* mwendo wa vyombo vya bahari. Mhe. Spika, tunataka Shirika la Meli liwe sayantific.

Mhe. Spika, mwaka jana ilizama boti, wale walioko ndani ya boti wanasema jamani sisi tunazama, wanapiga siku jamani watu wanakufa. Wakafa watu hivi hivi tu, wakati uwezekano wa kuwaokoa watu wale upo. Mimi nadhani Mhe. Spika, kuna haja ya kuanzisha kitengo maalum ndani ya Shirika la Meli, kama

walivyokua *traffic* kule barabarani wawe na *speed boat* ambazo nita-*monitor* usafiri wa bahari. Ikiwa hawawezi hii kazi sisi *backbenchers* tupo watuazime kidogo. Haiwezekani kuna gharama gani kuweka *speed boat* baina ya Tanga na Pemba, kuweka *speed boat* baina ya Pemba na Unguja. *Speed boat* tatu tu zikawa zina-*monitor* angalau likitokea tatizo tu watu wasife hivi kienyeji tu.

Mhe. Spika, Shirika la Meli wanatupa aibu sana. Kuna nchi wanajali raia wao, inaonekana sisi hatujaliwi hapa. Meli inazama pale baina ya Pemba na Tanga wanashindwa kutoa *speed boat* kwenda kuokolewa watu wanakufa wote. Mhe. Spika, niwape mfano mmoja jinsi wenzetu wanavyojali watu wao.

Mhe. Spika, pale Gwantanamo na Miami wanatumia hizi *boat* ndogo ndogo za *speed boat*. Mwaka 1998 ilizama *boat* pale. Akazama mwanamke mmoja wa Kikyuba ambaye aliolewa na Mmarekani, basi yule mwanamke alikufa lakini mtoto akapona wa miaka sita. Basi nchi mbili hizi zilikuwa zinamuwania raia yule na kupeleka ma-*boat* kumuokoa Mkyuba anasema ni wake na Mmarekani anasema ni wake, mpaka Mahakama ilipotoa uamuzi kama yule mtoto ni Mkyuba ndio ikabidi apelekwe Kyuba kwa mtoto wa bunduki. Sasa sisi tunakufa watu chungu nzima pale mnachuachia hivi hivi tu, wakati wenzetu mtoto wa miaka sita tu walimuania mataifa mawili, sisi tunakufa bure hivi hivi hamtujali jamani. Mtatumaliza sana.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe bado dakika tatu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, sasa niende moja kwa moja katika sehemu ya bandari ambapo tunaambiwa kwamba kuna zile meli pale zinahamishwa kutoka forodha mchanga zinaletwa hapa kuja kusiginiana na maboti. Mmeshafanya nyinyi uchunguzi wa kina kweli, *scientific analysis* mmefanya. Sasa mimi nashauri wale wanaomiliki meli kubwa kwamba Shirika la Bandari ni lazima liwe na captain wake waweze kufungisha wao meli pale, kwa sababu ikijakukwaruza meli ya Bakharesa hatokubali nawaambia. *Boat* ya Bakharesa ikikwaruzwa au *boat* ya mtu mwengine basi ni mapesa mengi, yale mameli makubwa yatakwaruza meli za watu pale. Miaka yote ilikuwa yanakaa pale wala hapana tatizo. Hebu tuelezeni msingi hasa wa kuziondosha pale na kutuletea zogo kule, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kabla ya yote na mimi nichukuwe nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuichangia wizara ambayo ni nyeti kabisa katika visiwa vyetu hivi viwili. Kwanza nichukuwe nafasi hii nitowe pongezi maalum kwa Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote ambao wamemsaidia katika kuweka vyema kitabu hiki. Nasema kwamba namuomba Mhe. Waziri wa Fedha, pale ambapo patakuwa panahitaji fedha kwa dharura basi Mhe. Waziri huyu uweze kumpatia.

Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kumteuwa Waziri wa Mawasiliano Mhe. Hamad Masoud Hamad, hakukosea na kweli ni moja katika fani yake.

Mhe. Spika, mengi yamezungumzwa lakini mimi kwanza nichukuwe nafasi hii niwapongeze sana wafanyabiashara wa vyombo vya usafiri. Kwa kweli tukitaka tusitake wamesaidia sana. Wenzetu hawa ambao wameleta usafiri baina ya Zanzibar Dar es Salaam, nakusudia Unguja Dar es Salaam na Unguja Pemba. Ni lazima tuwape sifa zao na kama sio wao basi sasa hivi usafiri wa baharini ungekuwa unatuletea usumbufu. Sasa mtu akifanya vyema mpe sifa yake. Mimi nawapongeza sana na waendelee.

Pia niwapongeze kwa sababu ni Baraza hili hili ambalo lilikuwa linatatua matatizo mbali mbali ya vipoza baridi kule katika maboti. Kwa kweli niwapongeze sasa hivi wamejitahidi kuyatengeneza baadhi ya maboti na kwa kweli hakuna usumbufu huo. Sasa nija katika shughuli ya bandari Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi kwanza niungane na wenzangu kulipa pongezi sana Shirika la Bandari, lakini penye mema na maovu hayakosi. Nasema tu kwamba kwa kweli kuna haja ya kutizama Mhe. Waziri pale wanapofikia abiria, tusimuache ndugu yetu Bakharesa amenufaisha Tanzania Bara pale Bandarini sisi tukambeza beza, kwa sababu huyu ni wetu wenyewe na taarifa nilizonazo kwamba yuko tayari kusaidia, lakini sisi bado tunampiga chenga huku na huku. Naomba sana pale pawe katika mandhari nzuri na hasa ukiangalia watalii pia wanafikia sehemu ile. Sasa ukikitizama hicho kibanda cha Uhamiaji pale, kwa kweli ni aibu kwa “Zanzibar Njema Atakaye Aje”. Kwa hivyo, namuomba sana wizara hii kupitia kwako Mhe. Spika, ihakikishe kwamba na sisi tunapata pahala pa kupumzikia pazuri na wenzangu wameeleza sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia nizungumzie kuhusu suala la uegeshaji wa magari, mbona kuna matatizo pale. Kwa hivyo, nadhani ni vyema Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atueleze ni sababu zipi wakati abiria wakitaka kusafiri, yaani wengine wanateremka na wengine wanaingia, magari na kupelekea balaa na usumbufu moja kwa moja. Sasa ni vizuri Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, akatueleza kuna tatizo gani ambalo linasababisha watu kupata shida wakati wanapotaka kusafiri. *(Makofi)*

Vile vile suala jengine na sisi tunasema kwenye utalii kuna mapapasi. Lakini na kwenye vyombo vyetu vya usafiri wako mapapasi wa tiketi, mimi nawaita mapapasi, kwa sababu kuna season maalum kama hivi sasa. kwa mfano, unapotaka kusafiri basi ukenda utaambiwa tiketi zitauzwa kesho asubuhi na

ukifika pale unaambiwa hakuna tiketi, lakini ukikaa kidogo watu wanakuja na tiketi mkono na kukuuzia kwa shilingi 40,000/= mpaka 50,000/=. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba kumuuliza Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba kuna sababu zipi ambazo zinazowafanya watu wetu wengine masikini wa Mungu hawawezi na tena wanao watoto ambao tayari wameshafikia umri wa kulipiwa tiketi. Kwa maana hiyo, naomba suala hili Mhe. Waziri wakati atakapokufa kufanya majumuisho aje atufafanulie.

Mhe. Spika, sasa nizungumzie kuhusu suala la barabara. Naomba nichukue nafasi hii Mhe. Spika, mimi pamoja na familia yangu ambayo inatoka Mtambwe. Kwanza nimpongeze Rais Mstaafu aliyepita kwa kuhakikisha hakujali kwamba Makamu wa Kwanza wa Rais anatoka Mtambwe na alikuwa ni mpizani katika vyama viwili hivi, lakini alihakikisha anapeleka maji pamoja na umeme. Kwa hivyo, lazima nimpongeze sana pamoja na kumshukuru Mhe. Rais Mstaafu Amani Abeid Karume. *(Makofi)*

Lakini ni Baraza hili wakati bado hatujahamia hapa, ilikuwa ni mimi miongoni mwa Wajumbe waliokuwa wakisimama kuhusu barabara ya Mtambwe. Kwa mfano, kuna siku Mhe. Rais Mstaafu alikuwa kulihotubia Baraza na kusema kwamba njia ya Mtambwe itajengwa na kama haikujengwa kwa fedha za serikali basi tutatafuta mfadhili, yaani mawili yatafanyika, itajengwa kwa fedha za serikali au tutatafuta mfadhili ambaye ataweza kujenga.

Kwa hivyo, nasema ninampongeza sana Mhe. Rais Mstaafu pamoja na Mhe. Rais ambaye ametawala hivi sasa, basi niwapongeze sana kwa kuwa na mpango mzuri wa kuweka njia katika Shehia ya Mtambwe. Mhe. Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba Mhe. Waziri atahakikisha njia hii, kwa sababu ilikuwa ya miaka mingi kama imeshatiwa katika mpango, basi iendelee ili na wananchi wa Shehia ile wapate kufaidika.

Mhe. Spika, sasa nije katika suala zima la utendaji katika wizara hii, kwa sababu wizara yangu ya mwanzo katika kuteuliwa mimi niliteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mawasiliano. Kwa hivyo, nichukue nafasi hii niwapongeze kwa kweli wizara hii inavyo vichwa, yaani inavyo vichwa ambavyo vitamsaidia sana Mhe. Waziri. Kutokana na hali hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, ashirikiane na vichwa hivi alivyonavyo, ili kuweza kuhakikisha mambo yetu yanakwenda sawia. *(Makofi)*

Mwisho niseme kwa niaba ya wanawake wa Tanzania hii, kwa sababu mimi nimechaguliwa na wanawake wote wa Tanzania. Kwa hivyo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kusimama tena hapa nikiwa mzima mwenye afya njema. Pili Mhe. Spika, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii kuweza kusimama hapa kwa ajili ya kuchangia machache katika wizara hii.

Mhe. Spika, asilimia ya bajeti hii nitakuja kuitoa baada ya majibu ya Mhe. Waziri, kwa sababu na mimi ni Mwakilishi wa Jimbo ninacho kilio changu nadhani Mhe. Waziri anakifahamu.

Katika Jimbo langu la Kwamtipura kuna barabara inayotokea pale kwenye Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara, maarufu kwa Abass Hussein inayopitia Mboriborini na kumalizikia pale Makao Makuu ya CUF ya Wilaya, maarufu Daraja Bovu.

Mhe. Spika, barabara hii kwa kweli wananchi wengi kwa Kwamtipura pamoja na majirani zao maeneo ya Chumbuni wanaitumia sana. Kwa kweli miongoni mwa majimbo ya mjini yenye umasikini mkubwa ni Jimbo la Kwamtipura, kwa hiyo wengi wao hawana usafiri wao wenyewe na hutumia daladala.

Sasa barabara ile Mhe. Spika, tumeiombea sana serikali tokea nilipoingia Barazani mwaka 2000 hadi leo 2011/2012 bado kilio changu serikali hakijasikilizwa. Mhe. Spika, nilifurahi zaidi na nilishukuru wakati ulipokuja ule mradi wa majaribio unaoitwa *RO-MIX*, ambapo ilikuwa ni *chemicals* zinachanganywa, ili baadaye zijengwe barabara.

Hivyo, kwa bahati nzuri katika *Pilot Project* barabara yangu ile ilikuwemo na ilikuwa pamoja na barabara ya Chumbuni ambayo inayotoka Karakana mpaka Saateni, barabara ya Kwa Kissassi pamoja na maeneo ya Fuoni na nyengine zilikuwa za Pemba.

Mhe. Spika, niliona Alhamdulillah Rabillalamina kile kilio changu cha barabara ile tayari kimeweza kupatiwa ufumbuzi, kwa sababu niliamini mradi ule kama ungelifanikiwa basi ungeendelea mpaka mwisho. Kwa hivyo, tulitiliwa hiyo *RO-MIX* kutoka pale Shaurimoyo chini ya kilima mpaka pale juu.

Sasa eneo lile Mhe. Spika kwa sababu kila mwaka wakati wa masika tunagharimika sana katika kutia kifusi kwenye eneo lile. Lakini kwa bahati mbaya kutokana na mteremko mkubwa, basi maji yanapita kwa kasi na kila tunapotia kifusi maji yana *flash out* na kile kifusi hakikai.

Kwa hivyo, hata huo mradi wa majaribio wa *RO-MIX*, inaonesha zile *chemicals* kwa mazingira ya Zanzibar hazikukubali, kwa sababu hivi sasa hiyo sehemu ambayo iliyotiwa hizo mchanganyiko wa *chemicals* tayari kimeshavurugika nyang'anyang'a, yaani hivi sasa kama mtu mjamzito anapitishwa akifika eneo lile basi nadhani anaweza kujifungua hapo.

Kutokana na hali hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwa sababu mwaka 2006 nilipokuwa namalizia wakati nilipokuwa nafungua Mradi wangu wa Chekechea Kwamtipura, tulimualika Mhe. Rais Mstaafu wa Zanzibar Dkt. Amani Abeid Karume alikuja na tulimuomba katika risala yetu. Kwa kweli alitukubalia na akasema basi atawaambia wataalamu wake waje waangalie na baadaye kuitengeneza barabara ile tena kwa kiwango cha lami, kwa bahati mbaya tunajua mambo yanakuwa mengi.

Lakini nilijitahidi tena katika kipindi cha mwisho mwaka 2010 nilijaribu kutuma barua kwa aliyekuwa Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi ambaye ni jirani yangu Mhe. Machano Othman Said na nakla nilituma kwa Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi kwa ajili ya kumkumbushia ahadi ya Mhe. Rais, pia nilipeleka Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara pamoja na Mfuko wa Barabara, ili kukumbusha kwamba kule Kwamtipura kuna ahadi ya Mhe. Rais.

Mhe. Spika, nashukuru rafiki yangu ambaye ni swahibu yangu, aliniahidi kwamba nisubiri kidogo tumalize hapa na pale tutakujengea. Lakini kwa bahati nzuri aliwahi kujenga ya kwake jirani pale Karakana, lakini ya kwangu mimi aliisahau. Sasa hakusahu barabara yangu, isipokuwa alisahau ahadi ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kilio changu hiki sikunyamaza kimya, wakati wa Kampeni nilimuona Mgombe wa Urais ambaye hivi sasa ndiye Rais wa Zanzibar na kilio kile cha barabara ile, tena nashukuru na kwa bahati nzuri Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kumbe anakujua vizuri, basi aliniuliza ile inayopita Mboriborini mpaka kwa Abass Hussein ah! ile barabara ya zamani naijua, basi usiwe na wasi wasi Assakheir Mwenyezi Mungu atajaalia.

Sasa Mhe. Spika, kwa kweli ni aibu Mwakilishi Hamza Hassan Juma yupo vipindi vitatu, yaani barabara ile kutoka pale mpaka kule isipite. Kwa hivyo, itakuwa siwatendei haki wananchi wa Kwamtipura ikiwa nitaikubali bajeti hii kama sijasikia kauli ya Mhe. Waziri. Kwa kweli nimejaribu kupekua sana kitabu hiki pia nimekwenda kwenye viambatanisho na wala sikuona kama kuna mwelekeo wa kujengwa barabara ile. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Spika, si hivyo tu hata kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka huu, ambapo naamini Mawaziri pamoja na Makatibu Wakuu wamepewa Ilani ya Uchaguzi ya CCM na barabara hiyo pia imetajwa. Sasa hiki kitabu inaonesha *priority* haikuangalia Ilani ya Uchaguzi na sijui *priority* hii ambayo imo humu kwenye kitabu hiki sijui inatoka wapi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hapa kidogo Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Naibu Waziri wasione tabu hii ndio ajira yenyewe. Kwa hivyo, nitakuwa mgumu kidogo kupitisha mpaka nipate maelezo ambayo labda hii ahadi ya Mhe. Rais Mstaafu itatekelezeka, kama itatekelezeka ni mwaka gani. Mhe. Spika, nimempelekea barua hata Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ajili ya kumkumbushia ahadi hii ya Mhe. Rais. *(Makofi)*

Nikiendelea na machango wangu kwamba tayari nimeshawatendea haki wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura na ninaamini hivi sasa wanasikiliza Mhe. Waziri atakuja kuleta jawabu gani katika barabara hii.

Mhe. Spika, nikiongoa hapo sasa nakuja ukurasa wa 8 wa kitabu kihi. Lakini samahani Mhe. Spika, katika kumbukumbu zilizoingizwa kwenye Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara katika kitabu hiki inaonesha wenzetu hawaweki kumbukumbu ya mambo wanayoyafanya. Kwa kweli kuna barabara ya Chumbuni haikutajwa kwenye kitabu hiki na imetengenezwa hatujui kama ni Mfuko wa Barabara au kwa fedha zao wenyewe ama ufadhili. *(Makofi)*

Sasa mimi naomba kuwakumbusha tu kwamba kazi nzuri wanayoyaifanya, lakini Mhe. Waziri hiki kitabu hakukitendea haki, kwa sababu kuna mambo mengi wanafanya na humu hayamo. Kwa hivyo, inawezekana masuala nikatayouliza mimi pengine wameshayafanya, lakini katika kitabu hiki hayamo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba mwakani Waheshimiwa Mawaziri wetu watuelezee, kwa sababu mimi sipendi kumsifu tu waziri, kwani Mhe. Waziri anatakiwa ajisifu mwenyewe kwenye kitabu chake kwa kazi alizozifanya. Kwa hiyo, mimi nimuangalie zile kasoro ambazo zimo kwenye wizara yake, ili mambo yawe sawa.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nije kwenye ukurasa wa 8 na Mhe. Waziri ameelezea kuhusu Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Mhe. Spika, moja kwa moja niende kwenye Uwanja wa Ndege au Mamlaka ya Anga hivi sasa. Kwa kweli hapa kuna kilio ambacho ni cha muda mrefu tena hiki ni cha wananchi.

Mhe. Spika, kwa kuwa hivi sasa nchi yetu tunasema kwamba tunakwenda katika Utawala Bora, tunashukuru hata wizara imezidi kuimarishwa, masuala

ya Utumishi wa Umma yameimarishwa. Lakini bado namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, ajaribu kuliangalia sana suala hili ambalo nitakalolizungumza na ninaamini na yeye analifahamu.

Mhe. Spika, kuna kampuni ambayo iliomba kazi ya kubeba mizigo pale Uwanja wa Ndege. Kwa kweli kampuni hii huyo mzalendo ambaye ameamua kuanzisha kampuni hii, alianzisha kwa sababu anayo *experience* ya ile kazi, kwa sababu yeye aliajiriwa pale *Airport* kama *Security Officer* katika eneo lile la *Airport*.

Mhe. Spika, sisi Waheshimiwa siku zote ndio tunaolalamika, kwamba pale watu wanapita ovyo, vitu vinapitishwa ovyo na kuna wengine wanapita *VIP* na wala hawahusiki. Kwa hivyo, huyu kijana wetu alijitahidi sana na kipindi wakati alipofika yeye aliona ile mizigo pale watu vijana wanabeba mizigo bila ya utaratibu, yaani wananyang'anyiana mpaka wakati mwengine abiria kwenye tax wananyang'anyiana.

Kutokana na hali hiyo, aliamua kupeleka maombi kwa kutumia ile *experience* yake, kwa sababu huyu mtu alikuwa ni Askari Jeshi tena alikuwa katika Idara ya Usalama, yaani anao utaalamu mwingi wa kuangalia mambo ya *explosion* na mambo mengi na kama kitu kibaya itapita pale *Airport*, basi anaweza kukigundua.

Mhe. Spika, kwa bahati mbaya alipopeleka maombi ya kampuni yake, kwa kweli yalimgeukia, lakini alipata mashirikiano mazuri na kuambiwa kwanza akatayarishe maandiko yako ya kampuni, akaambiwa basi anza kutafuta wafanyakazi tengeneza *uniform* na kila kitu. Kwa bahati mbaya sana Mhe. Spika, kwa sababu yeye ndiye aliyeandaa ule mradi, lakini matokeo yake ule mradi wakaja kuuchukua watu wengine.

Sasa Mhe. Spika, kitu cha kushangaza kwamba mradi ule yeye alikuwa pale ni mfanyakazi na alitumia ule uzoefu wake wa jeshini pamoja na utaalamu wake wa usalama, kuhakikisha kuwa ile kampuni atakayoiweka pale itakuwa na maslahi kwa Wazanzibari, kwa sababu watakuwa sio kubeba mizigo tu, pia watasaidia masuala ya *security* katika lile eneo.

Lakini Mhe. Spika, *documents* nimekuja nazo hizi hapa tatu, zote hizi ni kuhusu maombi yake pamoja na mambo mengine. Kwa hivyo, matokeo yake kazi ile hakupewa yeye. Sasa kazi ile wale aliokuwa akiwapelekea barua ndio wameichukua wao na hapa utawala bora haupo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pamoja na kwamba kampuni imeshakuwa *establish*, lakini naomba suala hili tuliangalie tena upya na wala sitaki niseme kwamba tuunde tume kwa

ajili ya kwenda kuchunguza. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho aje anipe jawabu nzuri sana. Sasa ikiwa hakunipa jawabu nzuri basi Mhe. Spika, nitakuomba uunde Tume ya Baraza kwa ajili ya kwenda kuangalia upya uhalali wa kampuni ile na huyu ambaye aliyeanzisha. *(Makofi)*

Kwa kweli alipoonekana huyu anaanza kufuata watu sana pamoja na kuhoji watu sana, basi amehamishwa na hivi sasa yupo mlangoni UUB analinda. Mhe. Spika, mtu amefikia karibu Cheo cha Canal na leo unampeleka pale UUB, sasa pale kunapita mzigo gani au kuna unga ama bomu litakalopitishwa pale UUB. Mhe. Spika, tunafika pahala kwa kweli tunawadhalilisha.

Lakini isitoshe Mhe. Spika, kwa sababu hii kampuni alishirikiana na mkewe, basi matokeo yake huyu mkewe alipoonekana mbona anataka kuingilia mambo mengine ya watu, basi na yeye amekuwa akipigwa danedane, kwa sababu huyu alikuwa *Office Supervisor (OS)* pale *Airport*.

Mhe. Spika, baada ya kuona mazonge mengi basi hata kazi akawa hapangiwi, aliamua kwenda kusoma na amejitahidi na kwenda hapo Chuo cha Utumishi Serikalini amesoma masuala ya *Accountant* amekwenda mara ya kwanza, mara ya pili. Sasa baada ya kurudi mtu ambaye amesomea *Accountant* unampeleka Afisa wa Mazingira *Airport*.

Mhe. Spika, nilisikiliza sana wakati Mhe. Waziri anatembelea vitendo vyake, aliwasisitiza sana wafanyakazi wake wasome na alisema kwamba kila atakayesoma basi atajitahidi kuhakikisha kuwa anamsimamia, ili ile taaluma yake ifanyakazi.

Kwa hivyo, mtu amesomea *Accountant* amekuwa Afisa wa Mazingira *Airport*, hivi kweli tunawatendea haki watu wetu na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora yupo hapa. Mhe. Spika, nadhani haya masuala tujaribu kuyaangalia vizuri sana. *(Makofi)*

Kwa kweli hivi sasa tunasema tunayo Serikali ya Umoja wa Kitaifa na wala tusijisifu tu kwa maneno, hebu tufanyeni kazi halafu wananchi waseme kweli Serikali ya Umoja wa Kitaifa inafanyakazi. Mhe. Spika, suala hili naomba tuliangalie kwa uzuri sana na ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anipe jawabu nzuri, vyenginevyo Mhe. Spika nitakuja kuomba tuunde Tume ya Baraza kwa ajili ya kwenda kuchunguza na kuangalia suala hili, kwa sababu Mhe. Spika tunapofika pahala watu wetu wanafanyakazi.

Kwa mfano, huyu mwanamama hivi sasa ameomba tena kwenda kusoma, kwa sababu amepewa Afisa wa Mazingira pale hata gari hana. Kwa kweli Afisa wa Mazingira anatakiwa aangalie mbwa, wagonjwa wa akili wanaoingia *Airport* wala hana gari, sasa atafanya nini afisa yule, yaani amekaa ofisini bila ya shughuli yoyote. Mhe. Spika, sitaki kumdhalilisha huyu mama, lakini hata sura yake imegeuka kama yangu, yaani sura yake kama ya mwanamme hivi sasa kwa mawazo. Kwa hivyo, tusiwadhalilishe wafanyakazi wetu kiasi hicho. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa maana hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anipe maelezo ya kina, ili yaweze kunisaidia kuhusiana na kadhia hii.

Mhe. Spika, kuna suala moja na Mhe. Naibu Waziri ameninong'oneza lakini haya naliacha.

Sasa niende kwenye ukurasa wa 12 kuhusu Sekta ya Usafiri wa Nchi Kavu. Lakini hili suala nililoliacha namuomba sana Mhe. Naibu Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, alishughulikie. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakuja Sekta ya Usafiri, yaani Idara ya Usafiri na Utunzaji Barabara. Kwa kweli idara hii kwa mwaka huu kuna barabara hii ya Amani – Mtoni na mimi kwanza nataka niwashukuru sana kwa ujenzi ule wa barabara. *(Makofi)*

Vile vile nataka nishukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete. Pamoja na Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Benjamin William Mkapa pia naye tunamshukuru, kwa sababu alitoa ahadi ya kujenga barabara ya Amani – Mtoni ile ya awamu ya pili. Kwa hivyo, tunashukuru ahadi ile Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaitekeleza hivi sasa na ile barabara iko upande wa pili. (*Makofi*)

Lakini hapa kidogo namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, aje anipe maelezo ya kutosha. Kwa kweli pale mradi ule hivi sasa kimeshaanza kuweka kifusi na bado ule mrdi unaendelea. Sasa kimsingi hoja yangu ipo hapa, ili kazi na mimi nakuja kwenye kifusi, kwa sababu kifusi tunajua Kibele tunalo eneo letu la serikali na kule kwa Mhe. Mohammed Seif Khatib kule Uzini liko eneo letu ya UUB.

Kwa hivyo, kwa nini tukanunue kifusi kwa mtu binafsi na hapa ndipo ninapopata mashaka na tukiangalia Mhe. Spika wizara hii katika wizara ambayo yenye miradi mingi mikubwa ni wizara hii na tunapitisha miradi mingi, hivyo fedha nyingi sana tunaidhinisha. Sasa haya mambo madogo madogo

kama sisi Wawakilishi inakuwa kidogo yanaanza kututia wasi wasi hata ile miradi mikubwa basi tunaweza kuwa na wasi wasi mkubwa zaidi.

Mhe. Spika, nataka kuuliza kwamba hapa sijui kuna kampuni au mwekezaji bwana Khalifa, ambapo kifusi kimenunuliwa na Idara ya UUB kutoka kwake yeye. Kwa hivyo, nauliza lile eneo la Kibele linafanyakazi gani? Mhe. Spika, serikali imenunua mitambo mingi kama vile *graders*, *bulldozers*, ili kufanyakazi za kwetu.

Mhe. Spika, hapa naweza kuja kuzuia kifungu cha mapato, kwa sababu hapa inaonesha kwamba kazi ile kama ingelifanya UUB, inamaana fedha zile zingelirudi serikalini. Lakini fedha hizi za kifusi zinakwenda kwa mwekezaji binafsi.

Sasa huyu mwekezaji tumeanza kuwa na mashaka naye, kwa sababu huyu bwana Khalifa sijui kama ndio kampuni, ndiye huyu Waheshimiwa Wajumbe jana waliokuwa wanalalamikia kwa kuvamia eneo la Maruhubi Chuo cha Maendeleo ya Utalii na mwekezaji huyu Mhe. Spika, amefukia bahari bila ya ruhusa ya serikali. Mhe. Spika, nitatafuta eneo la kuja kuunda tume ya Baraza kwa ajili ya kwenda kuangalia, kwa sababu huyu ndugu Khalifa ameuziwa eneo kule Dunga ameuziwa na serikali.

Kwa hivyo, kwanza tunataka taratibu za mauzo ya anayeuziwa na hili tunajua pengine halihusiani moja kwa moja na Mhe. Waziri, lakini miradi ya wafadhili inayokuja inakuja kwa niaba ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na tunajua yale mashimo wakati wanapoondoka yanarudi chini ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Pili kwa nini tukanunua kifusi kwa mtu binafsi wakati serikali inalo eneo pamoja na vifaa ambavyo vimenunuliwa maalum kwa ajili ya mradi huu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna hivi vifaa vya UUB. Kwa mfano, kuna *bulldozer* lilitoka Pemba moja kwa moja likatua Mangapwani kwa sababu kuna Mradi wa Chelezo. Mimi juzi wameniletea nakala ambayo Mhe. Makame Mshimba Mbarouk nakala hii inaonesha hakuisoma lakini kapelekewa yeye. Nilishangaa sana alipokuwa anasifu sana leo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano wakati kuna nakala ya barua ya ZIPA ambayo inakanusha kwamba Mradi wa Chelezo wa Mangapwani hawakuupa kibali.

Sasa Mhe. Spika, mimi nashangaa sana leo rafiki yangu kidogo labda inaonesha ile document hakuiona, lakini yeye ndio aliyepelekewa kama Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, mimi Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi wa Serikali nimeletewa nakala. Leo mradi huu wa Chelezo wa Mangapwani vifaa vilivyotumika ni vya UUB. Mhe.

Spika, tutapata maswali mengi kwa nini mradi ule binafsi ukatumia vifaa vya serikali, inawezekana pengine wanakodisha lakini sasa tujiridhishe kwa sababu baadhi ya gari ambazo zilifanya kazi kule zimerudishwa mbovu ziko pale UUB Saateni.

Sasa Mhe. Spika, huyo aliyekodishwa hakuwekewa masharti ya kutengeneza hizi gari. Mhe. Spika, nitakuja kuwa mgumu sana, nitaanza katika makusanyo kwa sababu ina maana kama tunakodisha vifaa vyetu tunakusanya fedha, hizi fedha tunazitumia vipi, kwa nini magari yarudi mabovu.

Lakini jengine Mhe. Spika, vifaa vya UUB kuna gari hapa la kubebea lami linaitwa *BOMARK*, gari hili zima limetolewa maringi akachukua Kampuni ya *MECCO* aliyoisifu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Mhe. Spika, mimi ninavyojua kampuni zote zinazojenga miradi zinafunga mikataba ya serikali, kampuni inalipwa *advance* na wanalipwa baadae.

Kwa nini waje wakongoe vifaa vyetu vya UUB, hili gari la lami hapa kama limetolewa mipira litatembea vipi. Sisi tunalalamika barabara zetu hazitengenezwi, *graders* yanakodishwa, magari yanatolewa maringi. Mhe. Spika, nataka maelezo ya kutosha ili niweze kupitisha bajeti hii ya Mhe. Waziri Magufuli. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakuja hapo hapo kwenye Idara ya Utunzaji wa Barabara.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, bado dakika mbili.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, pale Mtoni kulikuwa kuna vifaa vya UUB vimewekwa pale na hivi sasa wameambiwa waviondoe na wavirejeshe Idarani UUB na eneo lile tunasikia ameuziwa mwekezaji. Mhe. Spika, ardhi tunauza kama njugu, kwa sababu eneo lile pale vifaa vimewekwa, tena vimehifadhika pamoja kustirika tunaambiwa eneo kwamba limeuzwa na UUB wanaambiwa watoe vifaa vyao na tayari wameshaanza kuondoa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa hivi kwenye bajeti hii nitakuja kuunda Tume ya Baraza kwa ajili ya kuchunguza mambo yote na itabidi Mhe. Spika, kama hukuniruhusu nitakuwa sichangii tena Barazani na itakuwa nakaa Kwamtipura nasikiliza kwenye redio na kuja kuchukua posho, kwa sababu kazi nitakuwa siifanyi. *(Makofi)*

Vile vile hapa wanapohamishwa hawa UUB kulikuwa na *bulldozer* ambalo lilikuwepo na Kampuni ya *MECCO* waliruhusiwa kwenda kutoa *spare*, wakati *bulldozer* hii UUB wenyewe walikuwa wanalitengeneza na ilikuwa linakaribia kuanza kazi. Sasa Kampuni ya *MECCO* kwa kuhurusiwa imekwenda kutoa

spare. Kwa hivyo, hii Kampuni ya *MECCO* nauliza ni ya serikali au binafsi? Kwa nini watoe *spare* katika maeneo ya kwetu kwa ajili ya kwenda kuimarisha kazi zake. Mhe. Spika, naomba maelezo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia kulikuwa na majanareta hapa UUB. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, aje aniambie majanareta haya yako wapi, kwa sababu tuliambiwa yameazimwa na Shirika la Meli na yametiwa kwenye meli gani. Kwa hivyo, Mhe. Spika, tunataka kujua majanareta haya yako wapi na itabidi hiyo kamati utakayoiunda iende ikayaangalie na kuyaona majanareta haya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kweli naheshimu sana muda wako, lakini nilikuwa na *points* nyingi za kuzungumza. Lakini jambo la msingi ambalo nataka nizungumzie ni kwamba tunahitaji mawaziri wetu, wawasimamie watendaji wetu, ili wafanyakazi kweli.

Kwa hivyo, mambo ya kuja tu hapa na kusema Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kwa kweli wenzetu kule Bara Mhe. Spika, ili watu wasikuseme sana basi wewe msifu Nyerere tu, yaani wewe kaa pale na kusema Mwalimu Nyerere na wewe tafuna fedha zote huku kusema Mwalimu Nyerere. Sasa na sisi tusitumie mwanvuli wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa tukayafumbia macho haya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namuamini sana Mhe. Waziri kwa haya niliyoyasema, basi naamini atanijibu kwa ufasaha kabisa.

Lakini la mwisho kabisa Mhe. Spika, kuna Kampuni ya *ZAT*. Sasa na huku kwenye Kampuni hii ya *ZAT* kumeanza kuwa na wasi wasi kwamba hii kampuni inataka kunyang'anywa kazi na huu ni wasi wasi tu na wala sina ushahidi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri amelezo yake ndiyo yatakayonipa ushahidi, kwa sababu ni wasi wasi wangu asije akageuzwa kama hii kampuni iliyoandaa mradi na halafu mradi ule wakaja kuuchukua wakubwa na kuufanya wao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa sababu Mhe. Waziri kwenye kitabu chake hakueleza safari za nje. Kwa hivyo, tunataka Mhe. Waziri atueleza pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wote wanapokuja watueleze safari za nje, kwa sababu *they use public money*, yaani wanatumia fedha za umma. Mhe. Spika, nilikuwa nataka nije nipae maelezo kwa safari ya Mhe. Waziri.

Mhe. Spika: Mheshimiwa malizia *points* zako muda uliobaki ni mdogo sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, Mhe. Waziri na hii Kampuni ya Sea Sport kwa nina wasi wasi wale ambao sasa hivi wako Dar es Salaam pengine kuna mpango kwa sababu na hizi fununu tunazizungumza ili kama zipo kama watakuja basi waje kwa umakini, wasije katika njia za mlango wa nyuma.

Mimi sina uhakika lakini Mhe. Waziri akija akinieleza nitapata uhakika, alikwenda Uswiss nafikiri na Mkurugenzi wa Anga na *Security Officer,* hebu atwambie kule kulikuwa kuna kitu gani labda tukipata maelezo nadhani Mhe. Waziri ataweza kutusaidia kidogo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ndio maana nikasema mawaziri wasisubiri tuwasifu sisi wajisifu wenyewe kwenye vitabu, safari hizi za nje zisitutie mashaka. Mhe. Waziri kama angelieleza nimekwenda wapi, nimefanya nini, nimefanya mazungumzo na kampuni gani na kampuni gani tungeliridhika na wala tusingeliuliza masuala yoyote.

Mhe. Spika, mengine nitakuja kuyazungumza katika eneo jengine lakini pamoja na hayo yote, nataka nijue huyu aliyefukia bahari na hili ingawa sio la wizara yake lakini natanguliza kabisa Wizara ya Fedha siku yake, kuhusu uwekezaji *ZIPA* barua yao hii hapa hawakumruhusu amefukia bahari hakufuata masharti ya mazingira. Mhe. Spika, baada ya hayo machache mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura wameniambia nisiseme hata asilimia mpaka watakapewa kauli katika ujenzi wa barabara yao na mambo mengine. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe muda uliobaki ni mchache mno hautaweza kumtosha Mhe. Farida isipokuwa nimuombe tu kwamba jioni Mwenyezi Mungu akipenda awe ni mtu wa kwanza kuchangia. Na wengine watakaofuata ni Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Asaa Othman Hamad pamoja na wengine kwa hiyo niwaomba hawa niliowataja waje mapema ili kuweza kuendelea kuchangia.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa
hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Farida Amour Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia mtu wa mwanzo jioni hii ya leo, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae ameniwezesha kufika hapa katika baraza hili tukufu nikiwa na Afya njema, pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa dhati kabisa yeye pamoja na watendaji wake jinsi walivyoichambua bajeti hii kwa umakini, bajeti yenye kuleta matumaini kwa Wazanzibari.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo naomba niende moja kwa moja kwenye mchangio wangu na nitaanzia katika bandari ya Wete, bandari ya Wete ni eneo muhimu sana kwa wasafiri wa Pemba na Zanzibar kwa jumla na hasa Mkoa wa Kaskazini Pemba, katika kitabu hiki nimezunguruka sana lakini sikuona eneo ambalokuwa lina matengenezo ya bandari hii ya Wete. Sasa kipindi cha nyuma sana ilifanyiwa ukarabati mdogo sana ambao kuwa haukidhi haja, sasa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atuambie ni lini atakuwa na mpango wa kuendeleza ile bandari ya Wete angalau kuongeza mita ishirini ili vile vyombo vipate kufunga gati vizuri pale katika bandari ya Wete.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kama usafiri wa Pemba Tanga pia ni mgumu kupindukia na asilimia kubwa ya wananchi wanaoishi katika kisiwa cha Pemba hasa Kaskazini Pemba shughuli zao za kutafutia maisha ni biashara, biashara hiyo matumaini yao makubwa wanamochukua bidhaa hizo ni Tanga na Mombasa. Sasa Mhe. Waziri naomba afanye jitihada zake zote pale hapana usafiri wa uhakika kutoka Pemba Tanga ambao watu wanaosafiri kwenda katika maeneo hayo wanaweka rehani roho zao Mhe. Spika, kwa sababu vyombo vidogo vidogo ni hatari Pemba na Tanga ukipaangalia unaona ni masafa mafupi sana, lakini kwa bahari haina udogo, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri atumie jitihada zake zote ili tupate usafiri wa uhakika katika kisiwa cha Pemba na Tanga.

Mhe. Spika, pia naomba niendelee katika shirika la meli katika usafiri wa jumla wa Pemba bado hatuna usafiri, usafiri kutoka Unguja Pemba pia ni matatizo Mhe. Spika, tunapata tabu na watu ni wengi sana wanaosafiri tokea iuzwe meli ya MV Mapinduzi Mhe. Spika, tunapata tatizo kubwa wananchi wa visiwa viwili hivi. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupe maneno mazuri na madhubutu yatakayoturidhisha Wazanzibari kujua badala ya MV Mapinduzi atatupa usafiri gani wa uhakika ili tuepukane na matatizo ya usafiri watu wa visiwa hivi.

Mhe. Spika, vyombo vya usafiri vya binafsi namuomba Mhe. Waziri vifanyiwe ukarabati, vichunguzwe kwa makini kwa sababu vile vyombo baadhi yao vinaonekana ni chakavu sana havina umadhubuti na baadae watu wanaoingizwa katika vyombo hivyo pia waangaliwe, sio kama watu waingizwe tu katika vyombo vile bila ya mpangilio maalum, vyombo vile ni vidogo lakini vinachukua abiria kupita ule uwezo wa ile meli matokeo yake vinaweza kuleta matatizo na athari kubwa kwa nchi nzima.

Mhe. Spika, Shirika la Meli ni muhimu kwa wasafiri na abiria kutoka Unguja kwenda Pemba na ni muhimu kiuchumi, sasa kwa vile wafanyabiashara wa Unguja na Pemba hasa katika kipindi hiki tunachokielekea cha ramadhani wanasafirisha bidhaa nyingi sana kutoka Pemba kuzileta Unguja kwa

kuwasaidia wenzetu waliopo Unguja kwa ajili ya futari za ramadhani, mihogo, ndizi, mafenesi sasa pakikosekana usafiri mzuri wa uhakika wale wa Pemba wanaosafirisha vitu vile kuleta huku Unguja kwa ajili na wao kupata maslahi yao kidogo ya kujiendesha maisha na watoto wao wanakosa. Na wale watu wa Unguja nao wanaopokea bidhaa zile kwa ajili ya kuendesha maisha yao pia wanakosa.

Mhe. Spika, hili ni jambo muhimu sana na namuomba Mhe. Waziri aliangalie kwa makini san asana, ningelia hapa kidogo lakini mtu mzima kulia ni vibaya hivi sisi watu wa Pemba kwa nini hatupati usafiri wa uhakika, hakuna uwezekano sisi wa kutafutiwa meli moja kubwa ya kazi ambayo kuwa inaweza kwenda vizuri inayohimili maji yaliyopo kutoka Kisiwa cha Pemba na Unguja tukapata usafiri wa uhakika. Nina imani kwa umakini aliokuwa nao Mhe. Waziri na jinsi anavyowapenda wananchi wa Zanzibar basi hili atalitekeleza na namuomba alitekeleze kwa ufumbuzi huo tutakuwa tumeshapata nafuu Wazanzibari.

Mhe. Spika, naomba niwapongeze watu wa mashirika ya simu, pongezi zangu ziende kwa watu wa *ZANTEL* kwa kazi kubwa wanayoifanya, lakini kuna mambo mawili muhimu itabidi watusaidie watu wa *ZANTEL* kuna kipindi huwa wanatoa ofa sana, lakino ofa zao zinaleta matatizo wanaweza kuleta ofa lakini ofa hiyo ikishaletwa katika kipindi hicho unaweza kupiga simu za muhimu kuna mambo muhimu unataka kuzungumza lakini simu hiyo mtu hapa na hapo unaambiwa hapatikani, simu imefanya hivi na hivi. Kwa hivyo wajipange vizuri katika kutoa ofa zao hizo na pia waige kutoka *TIGO*, *TIGO* wanatoa ofa nyingi tu tena wakitoa ofa hata kama ya muda mrefu au muda mfupi basi wao hawana matatizo, kwa hivyo na wenzetu wa *ZANTEL* wana mambo mengi wanayoyafanya lakini naomba pia walitizame vizuri hili wanapotoa ofa wasiwape usumbufu wateja wao, kwa sababu *ZANTEL* tumewaunga mkono asilimia kubwa Wazanzibari kwa hivyo naomba walielewe hilo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kidogo nataka niende kwenye barabara lakini huku sitaki niseme sana nataka niseme mambo mawili au matatu, kwanza nataka niipongeze serikali kupitia Wizara yako kwa kuwa na nia ya kutengeneza barabara tatu kubwa za mijini na vijijini katika kisiwa cha Pemba. Mhe. Waziri nataka alielewe hilo kama Wazanzibari wa Kisiwa cha Pemba kwa muda mrefu kilio chao ni barabara, sasa kwa miradi hii au kwa imani hizi zilizotolewa watakuwa tayari kututengenezea barabara za Pemba naomba nimwambie Mhe. Waziri neno moja muhimu.

Mhe. Waziri ukumbuke kama unatumia pesa nyingi za serikali pamoja na washirika na wafadhili kutoka nchi mbali mbali kwa ajili ya kutengenezea

barabara, nakuomba Mhe. Waziri unapotengeneza barabara hizi barabara ziwe nzuri na ziwe na kiwango ili kuondosha yale malalamiko na kila siku ikawa tunatengeneza kitu kile kwa kile, tukitengeneza barabara mwaka huu ikiwa nzuri miaka mingine tutatafuta mipango mingine ya kutengeneza kiwanda ili mradi na sisi nchi yetu ionekane inang'ara.

Mhe. Waziri kwa kumalizia naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu katika bajeti hii ya Wizara hii ambayo ni muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu, kwanza naomba nitangulie kwa kumpongeza Mhe. Waziri, nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na Naibu wake kwa kuteuliwa kuziongoza Wizara hii, hii ni wizara muhimu sana na wizara ambayo ndio msingi wa ujenzi wa uchumi wa nchi yetu, naamini kwamba Mhe. Rais kafanya hivyo baada ya kuona na kutambua uwezo na uzoefu aliokuwa nao Mhe. Hamad Masoud pamoja na msaidizi wake naamini kwamba watafanya kazi ambayo Wazanzibari wote tunaitegemea ndani ya kipindi hiki cha miaka mitano na Mwenyezi Mungu naomba awawezeshe katika hilo.

Mhe. Spika, utangulizi naomba niseme kitu kimoja, baraza lako sasa hivi liko katika wakati wa kupitisha bajeti na baada ya bajeti wizara zitakwenda kufanya maatumizi na baada ya kutumia kazi itakayofuatia ni kukagua matumizi, kazi hiyo inafanywa na mdhibiti na mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali. Lakini baada ya kazi hiyo ya kutumia ripoti mdhibiti ataleta mbele ya baraza lako na kamati ya PAC itakabidhiwa kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, naomba katika hilo uniruhusu nifanye nukuu ya kanuni ya Baraza kifungu cha 115 kifungu cha pili c.

Kifungu cha 115 (2) C kinasema.	"*Kamati ya Kuchunguza na kudhibiti hesabu za serikali moja kati ya jukumu lake ni kuchunguza kwa njia yoyote inayofaa mambo yote yanayohusu hesabu za serikali asasi zake"*
Kifungu cha 115 (3) Kinasema.	" *Kamati ya PAC katika kufanya kazi zake itakuwa na wajibu wa kuchunguza kama fedha*

zilizoonyeshwa katika Makadirio ya Matumizi ya Serikali na Mashirika yake zimetumika kama ilivyokubaliwa, na matumizi yalikuwa chini ya mamlaka iliyo husika na matumizi yalifanywa na kuzingatia thamani halisi ya fedha"

Kwa hivyo naomba niwakumbushe mawaziri kwamba Kamati ya *PAC* inafanya kazi katika Wizara zao ingawa inavyoonekana kila waziri anayekuja hapa asahau kwamba ni moja kati ya kamati inayofanya kazi katika Wizara zao, na inafanya kazi kubwa kwa sababu hiki tunachokiidhinisha ni jukumu la Kamati ya *PAC* kufuatilia matumizi yake, sasa huu ni ukumbusho tu kwamba mawaziri watambue baada ya kuwaidhinishia fedha mwisho wa siku kamati itapita na kuchunguza mahisabu kufuatia ripoti za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa hesabu za Serikali.

Kwa maana hiyo naomba Mawaziri nao niwakumbushe kwamba moja kati ya kamati yao ni kamati ya Kuchunguza hesabu za serikali na mashirika ya Umma, inanipa tabu kuona kwamba mawaziri wanaokuja wote wanazungumzia tu kamati zao za kisekta, wanasahau kwamba kuna kamati inayowashauri vizuri na kuwapa miongozo juu ya matumizi ya fedha za umma tunazoziidhinisha katika baraza hili. Ni mategemeo yangu kwamba mawaziri watakapokuja wengine watatambua hilo na watatambua kazi kubwa inayofanywa na kamati ya *PAC* katika kuwashauri juu ya matumizi ya fedha tunazoziidhinisha hapa.

Sasa baada ya ukumbusho huo Mhe. Spika, naomba niende kwenye hoja na naomba nianze na Idara ya usafiri na Leseni, kwa kweli bado tuna tatizo la matumizi mabaya ya fedha za umma na moja kati ya kipengele kinasababisha matumizi mabaya sana ni matengenezo ya magari ya serikali, serikali kupitia matengenezo ya magari ya serikali kupteza fedha nyingi sana kwa kutengeneza magari katika gereji za vichochoroni. Nakumbuka katika kipindi cha nyuma serikali ilikuwa na utaratibu mzuri wa kuitumia hii karakana kuu utaratibu ambao tumeuacha na hiyo hupelekea kila idara na kila taasisi kutafuta gereji hata chini ya misheli sheli.

Kitendo cha serikali kutumia kutengeneza magari kwa magereji yasiyofahamika Mhe. Spika, ni tatizo kubwa sana na ni moja kati ya chaka la ufisadi tulilonalo hapa, naishauri serikali kwanza naishauri wizara iimarishe karakana kuu, lakini hili sio suala tu la Wizara ni suala la serikali kuu

kulifikiria hilo na kuona umuhimu wa kuimarisha karakana hii ili magari yote na vyombo vyote vya serikali Mhe. Spika, tuwe na sehemu maalum ambayo vyombo hivi vinaweza kwenda kupata huduma ya matengenezo ili kuokoa fedha nyingi za serikali, ambazo huwa zinateketea kupitia sehemu ya matengenezo ya magari.

Mhe. Spika, sasa naomba nigeukie Shirika la Bandari kwanza niupongeze uongozi wa Shirika la Bandari kwa kazi kubwa na nzuri wanayoendelea kufanya, lakini baada ya pongezi hizo nataka nitambue kwamba serikali iliamua kujenga bandari ya Wesha/Chake Chake nisifu kwa hatua hiyo ya serikali nisifu kwa sababu Chake Chake katika kisiwa chetu cha Pemba ni ukweli kwamba sasa hivi ni mji unaokua kwa kasi na kijografia Chake Chake ndio mji ulio kati kati unaounganisha kusini na Kaskazini. Chake Chake ni mji wa kibiashara kwa hivyo maamuzi ya serikali kujenga bandari pale ni kuendeleza kwa sababu bandari ya Chake Chake ilikuwepo kwa muda mwingi sana haizuru ilikufa lakini nashukuru na napongeza serikali kwa kuona umuhimu wa kufufua bandari ile ya Wesha.

Sasa pale kilichotumika ni fedha nyingi za serikali lakini hatutegemei kwamba serikali iweke fedha nyingi halafu baadae yale malengo yaliyokusudiwa yasifanikiwe, ninachokusudia kusema sasa hivi matumizi ya gati ya Wesha yanaonekana kama kupoteza maana Mhe. Spika, na katika hili basi kwa sababu nilikuwa nikifuatilia hili na kuchukua takwimu kwa sababu bandari kuwepo kwake maana yake vyombo vifike pale lakini inavyoonekana vyombo vingi tulivyokuwa tunategemea havifiki katika bandari ya Wesha, maslan katika mwezi wa Mei kwa mujibu wa taarifa nilizokuwa nazo ni mashua mbili tu ndio zilizoegesha katika bandari ya Wesha. Sasa ikiwa mwezi mzima wa Mei ni mashua mbili na mwezi wa Jun ni mashua tatu pamoja na meli moja ya saruji, ni dhahiri kuona kwamba kuwepo kwa bandari ile kunapoteza ile maana hasa ya kuwa na bandari.

Kwa sababu serikali imewekeza fedha nyingi kwa maana maalum sasa tatizo nini, tatizo kubwa lililojitokeza ni kutokana na udogo wa bandari au ni kutokana na udogo au ufupi wa lile tuta la bandari, kwa sababu wenye vyombo wengi hucheleya kupeleka vyombo vyao pale na kupwewa. Sasa kama alivyosema Mhe. Farida hapa kuhusu bandari ya Wete ndio tatizo lililopo katika bandari ya Wesha, kuna tatizo la ufupi wa nandari na nilifuatilia wakanambia bandari ile kama ingeliongezwa kama mita ishirini ikafika kwenye mto basi hapana shaka vyombo wakati wote vingelifunga na kuondoka wakati wowote wanaotaka.
Sasa naishauri serikali ili isionekane kwamba imepoteza fedha za umma bure ndio hilo suali tunalolizungumzia naomba ifanye jitihadakwa hii sehemu iliyobaki, haidhuru tugharamike zaidi lakini uwepo wa bandari ile ionekane na

maana naishauri serikali, naishauri Wizara ifanye kadiri inavyowezekana imalizie hatua ya kuongeza mita kama ishirini ili bandari ile itumike na wafanya biashara wa Chake Chake wasipate tabu ya kuteremsha mizigo yao ama bandari ya Mkoani au Bandari ya Wete.

Mhe. Spika, sasa naomba niende kwenye ujenzi wa barabara idara hii inafanya kazi kubwa na nzuri, lakini tatizo lililoko katika idara ya *U.U.B* ni tatizo la ukosefu wa zana nzito unenzi wa barabara unahitaji kuwepo kwa zana nzito na bila ya kuwepo zana nzito haiwezekani, haidhuru mara hii tumekuwa na teknolojia mpya ya kujenga kwa kutumia mikono. Lakini mimi binafsi siamini kama ni ujenzi ambao unaweza kuleta maana sana, bado naamini kwamba kwa nchi yetu ilivyo nchi ya milima zana pekee ambayo inaweza kutujengea barabara ni kutumia dhana nzito kwa ajili ya kukata milima na kutengeneza barabara.

Mheshimiwa tumekuwa na tatizo kubwa la kutokuwepo kwa zana nzito sijui sijafuatilia sana lakini hasa Chake Chake au Pemba kwa ujumla wizara imekuwa na tatizo kubwa la zana nzito, katika bajeti hii nilifuatilia sana lakini sikuona pahala kwamba kutakuwa na program ya ununuzi wa zana nzito, leo ukienda pale Mawasiliano utaambiwa kuna *grader* moja Pemba nzima huazimwa kama kitabu cha maulidi na *grader* hilo mipira mara mibovu, injini mara mbovu mara hivi. Sasa imekuwa ni tatizo hatuwezi kujenga njia bila ya zana nzito, pamoja na kwamba sasa hivi tunajikita kwa wafadhili na wafadhili moja kati ya masharti ni kuleta zana zao, lakini wakati mwingi wafadhili nao au makampuni tunayoyatumia haya huchukua au hutaka kutoa zana kutoka kwa serikali tayari tumeshaliona hilo katika kampuni yia *PHIL* na kampuni nyengine.

Sasa Mhe. Spika, nimuuliza Mhe. Waziri atakapokuja atwambie ana mpango gani wa kuomba, maana yake wakati mwengine kuomba ndio kwingi ana mpango gani wa kwenda kuomba katika safari zake hizi angalau tukapata ma-*grader* angalau matatu kule Pemba na mengine tukapata hapa Unguja, tunazungumza hivi kwa sababu Mhe. Spika, wawakilishi wako wakati mwengine tumekuwa tukisaidiana na serikali katika kutengeneza njia zetu, maana ake sio kwamba kila kitu tunawaachia serikali. Lakini mara nyengine na wakati mwengine wawakilishi ama wabunge hushirikiana na wananchi na hushirikiana na serikali katika kutatua kero ndogo ndogo tunazoziweza, sasa hapa inakuwa ni tatizo tunapokwenda Mawasiliano mimi nimshukuru sana Afsa Mdhamini kwa kweli tuna mashirikiano mazuri sana ya kutusaidia tunapokwenda na matatizo yetu, lakini katika hili na yeye pia linamuwia vigumu unaweza kuengeji angalau wewe muwakilishi utoe mafuta, umwambie niazime gari mimi nitaweka mafuta hana.

Sasa katika hili Mhe. Waziri tunaomba uwe na utaratibu maalum kwa wale wawakilishi ambao watafika katika afisi yako kukuomba msaada kama huu hata kwa kuchangia mafuta basi kusiwe na vipingamizi, kwa sababu sote tunafanya kazi moja kazi ya kutumikia wananchi, serikali inafanya kazi ya kuwatumikia wananchi na sisi tunafanya kazi ya kuwatumikia wananchi. Wakati mwengine huwa tuko tayari kuchangia mafuta wizara itoe gari sisi tutoe mafuta lakini hilo pia linashindikana, tunamuomba Mhe. Waziri kwanza awe na utaratibu maalum wa kuhakikisha kwamba pindipo itatokezea hali kama hiyo basi kusiwe na vikwazo vingine, lakini hapo ninachomuomba zaidi anielezee kuhusiana na vipi wizara imejipanga kuleta zana nzito katika kisiwa cha Pemba na katika kisiwa cha Unaguja.

Mhe. Spika, nimuulize Mhe. Waziri tulikuwa na ile teknolojia *row mix* tulilizungumza mwaka juzi na mwaka jana na kwa kweli ilionekana baadhi ya barabara serikali iliamua kuzitengeneza kwa juhudi hizi, lakini katika bajeti ya mwaka huu kwa kweli sikusikia hadithi yoyote inayohusiana na *row mix* ile program iliishia je, ni vyema Mhe. Waziri akatuarifu kwa sababu tulikuwa tulikuwa tunafahamu barabara ya Kiwani ile Mhe. Hija aliyosema imetengenezewa kwa *supe clue*, barabara yangu ya Birikau, Barabara ya Kirwa *road* Wete na barabara alizozungumza Mhe. Hamza Hassan Juma zote zilipangwa kutengenezwa kwa tenkonojia hii. Je ile teknolojia imemalizi malizia vipi haikufanikiwa katika nchi yetu, kwa sababu serikali ilitwambia wenzetu wa Afrika ya Kusini walinufaika sana na baadhi ya nchi za kiafrika na sisi tulijaribu tukatumia fedha nyingi sana za umma.

Lakini matokeo yake hatukuona matokeo na tunaona *row mix* inayayuka kimya kimya tu, sasa tulikuwa tunahitaji kupata kauli ya serikali ile teknolojia iko je sambamba na hilo basi niulizie barabara yangu ile ya Birikau imefikia katika hatua gani kwa sababu ilijengwa kwa *row mix* katika kiwango cha kiliomita moja na nusu teknolojia ile ikaharibika na wizara ikaamuza kujenga kwa njia nyengine. Lakini mara hii sikusikia hadithi katika kitabu hiki barabara ya Birikau, Barabara ya Kichungwani na barabara ya Msingini ambayo mfuko wa barabara iliahidi kunijengea. Sasa sijasikia hadithi yoyote namuomba Mhe. Waziri atakapokuja aje atueleze hatima ya barabara zangu hizi.

Mhe. Spika, tatizo langu jengine ni daraja la Tinga Tinga hili sina maelezo sana isipokuwa nasubiri maelezo kwa sababu kilio cha wananchi hasa wa ukanda wa Magharibi wa jimbo langu kilio changu ni daraja la Tingatinga, jibu nililolipata kwa Mhe. Naibu Waziri ni kwamba daraja la Tingatinga halina maana mimi hili leo silihitaji, wananchi wanahitaji na mimi muwakilishi nahitaji kwa maana hiyo naiuliza serikali. Watafanya utaratibu

gani wa kuhakikisha japo lile lile daraja la mbao kulijenga tena ili kuepusha maisha ya wananchi.

Mhe. Spika, naomba nizungumzia suala la Karume *Air Port* na suala la taa, hiki ni kilio kikubwa sana kwa kipindi cha miaka nenda miaka rudi tunazungumzia tatizo la taa katika uwanja wa ndege wa Karume, hili sio suala la kuambiwa kwamba tusubiri wafadhili au tusubiri kitu chengine. Kwa umuhimu wa uwanja wa ndege kwa kisiwa cha Pemba ilikuwa serikali ifanye kadiri inavyowezekana iweke taa, Pemba hatuna *ICU* mgonjwa wakati wowote anatakiwa kuwahishwa Unguja ikiwa uwanja wa ndege hauna taa hali itakuwaje. Tusisahau kipindi kilichotokea matatizo ya Marehemu DK. Omar Ali Juma na matatizo ya taifa yaliyojitokeza pale katika Uwanja wa Ndege, kwa hivyo sasa tunataka tupate jawabu. Namna serikali ilivyojipanga kwa kuweka taa katika Uwanja wa Ndege wa Pemba.

Mhe. Spika, mwisho kabisa kwa kuthamini muda wako naomba nizungumzie suala la ujenzi wa ofisi, wenzangu wameshazungumza Mhe. Mbarouk Mussa Wadi kazungumza lakini na mimi vile vile nataka nijue kwa sababu wizara ilikuja hapa tukaiidhinishia fedha na fedha zikatolewa na baraza lako hili, ndio yale niliyosema kwamba kazi ya *PAC* ni kufuatilia matumizi yaliyotumika. Sasa ikiwa leo kamati yangu ilifuatilia pale na tukaambiwa kwamba ujenzi ule sasa umeshaondoka Mtoni na unakwenda Mazizini tulitaka tujue kulikoni, katika hili badi kwa sababu katika serikali sasa hivi kuna kitu kinanipa tabu. Jina la Rais kutumika vibaya uhaulishaji mwingi wa mali za serikali sasa hivi utasikia jina la rais linatajwa sijui kama kweli rais anaingiza mkono wake, lakini mimi binafsi nina hofu kwamba watu wanatumia jina la rais kufanya uhaulishaji na katika kuuza mali za serikali.

Naomba nimtanabahishe waziri mapema atakapokuja hapa kamati ilikwenda ikauliza na ikaambiwa kwamba kiwanja amepewa mfanya biashara na mfanya biashara kaahidi kujenga mazizini, lakini kamati ilihoji kupewa mkataba kamati haikuona mkataba uliotolewa. Sasa nahofia hili Mhe. waziri kuja kusema mkataba upo likija likitokea hilo itakuwa ama wizara imeidanganya kamati au waziri anataka kulidanganya baraza, naomba nimtanabahishe hili katika majibu yake ili tusije tukafika pahala tukampigia buti. Kwa sababu tunaona kaanza na mwendo mzuri amalizie na mwendo mzuri.

Mhe. Spika, baada ya hapo nakushukuru sana ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia kukutana jioni hii ya leo tukiwa wazima wa afya, pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa

nafasi na mimi ya kusema machache ndani ya hotuba ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasilino.

Mhe. Spika, naomba nianze na suala la usafiri wan chi kavu, Mhe. Spika, tunamfuko huu wa barabara. Miongoni mwa kazi zake ni kutunza na kuzifanyia matengenezo, barabara za mijini na vijijini ili ziweze kupitika.

Mhe. Spika, miaka mitano iliyopita nilikuwa naiyomba sana serikali ili kutunza jina la Marehemu kiongozi wetu, mzee wetu, Rashid Bin Abdalla Mamba. Mzee huyu alikuwa mahiri sana kwa kuzijenga njia kwa uwezo aliyokuwa nao yeye. Mhe. Mamba alitujengea barabara kutoka Mtemani, ikapita Jadida, ikapita Bugujiko, Kipangani na kuibukia viwanja vya mpira Mnazi Mmoja Wete. Siku hizo mji wa Wete labda ilikuwa na wakaazi laki moja na kidogo.

Mhe. Spika, barabara ile naomba sana serikali kupitia waziri ambaye sifa zake umezisikia mwenyewe. Sasa hivi ina umuhimu mkubwa zaidi kuna mji, kuna wakaazi wengi, kuna mashamba makubwa ya mikarafuu, kuna mashamba ya mifugo, katika ile dhana ya mapinduzi ya kilimo tunakotegemea asilimia karibu 90 ni moja ya miundombinu mizuri. Wakulima waweze kutumia barabara hizi kusafirisha mazao yao.

Namuomba sana Mhe. Waziri barabara hii ilipata msaada, nashukuru sana msaada wa mfuko huu. Unapoiwacha miaka mitano mengine unakuja kuanza hesabu mpya. Ingefaa angalau pale panapoharibika parudiwe kutengenezwa, tuwe na barabara kwa kiasi hichi hichi cha kifusi lakini iweze kutumika ipasavyo.
Mhe. Spika, pili kuna barabara maarufu inayotoka barabara kuu Wete/Chake inapita Mtemani, Kipangani cha Juu, Kipangani Bondeni mpaka mjini na hii inaungana kupita Darajani na barabara hii ninayoizungumza mwanzo. Barabara hii leo laitani wenzetu wangeiyona na wakaipa hayo matengenezo na kuzifanyia ukarabati ingepunguza kwa kiasi kikubwa msongamano wa barabara hizo.

Mhe. Spika, barabara kuu leo kunapotokezea matengenezo madogo inakuwa ni bughudha kubwa kwa sababu ni barabara moja tu ndani ya Mji wa Wete. Barabara hii ina umuhimu wa aina yake. Namuomba Mhe. Waziri akisikie kilio cha watu wa Wete, barabara yao tokea mkoloni, kuna haja ya mbadala. Ndani ya serikali ya awamu ya saba inayoongozwa na Dokta Shein chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, nadhani jina libaki na sifa zake.

Mhe. Spika, nije kwenye Mamlaka ya Viwanja vya Denge. Wamesema waliosema lakini miongoni mwa shughuli za Mamlaka hii ni kusimamia viwanja vya ndege Zanzibar kimaendeleo. Zanzibar ni pamoja na Unguja na

Pemba, tumepiga makelele mengi na mwenzangu aliyekaa punde bado kapiga makelele juu ya kiwanja cha Ndege Pemba. Hivi Mhe. Spika, mpaka tuone ajali ndio tuone umuhimu. Viwanja hivi havina taa ya kuongoza ndege. Kiwanja hiki hakina uzio, siku ya kutokea ajali nani alaumiwe. Ndege inatua na ng'ombe kaingia jamani tutasema nini, ni wenyewe wenyewe tutafunikana. Kama siku ile mlango uliyofunguka, lakini siku nyengine tunakuwa na wageni wetu pengine ndio hao tunaowatarajia kutusaidia maendeleo yetu, ni aibu.

Mhe. Spika, kitabu hichi baada ya kutaja ujumla viwanda vya Ndege vya Zanzibar lakini hakikutajwa Kiwanja cha Ndege Pemba. Mhe. Waziri tunakuomba angalau uje utupe sababu zilizokufanya kwa nini ndani ya kitabu hiki kiwanja cha Ndege Pemba hakimo. Kwenye kitabu kumeandikwa Pemba wamepokea ndege 450 mwaka uliopita, kiwanja cha Unguja elfu thalathini mia tisa thamanini na tatu (30,983) ni sababu zipi zilizofanya kiwanja hichi kipokee ndege 450. Ni hii dharau iliyoota mizizi ndio iliyofanya idadi hii. Kwa sababu uwezekano mkubwa upo. Wafanyabiashara Pemba wapo, wenye uwezo wapo, wasafiri wa ndege wapo. Lakini dharau imezidi mipaka, mimi natumia neno hilo hilo. Hakuna sababu ya msingi, mimi nasema haipo ya kuwa kiwanje kile hadi leo hakina taa za kurukia ndege.

Mhe. Spika, tuna Mamlaka ya Usafiri baharini, kwa sababu tunaishi ndani ya visiwa tutaogelea humu humu baharini. Mamlaka hii iliundwa kwa Sheria ya *Zanzibar, Maritime Authority Act No. 3 2009* tuliipitisha sisi wajumbe wako na kuipa kazi moja ni

- Kudhibiti safari za baharini,
- Uchunguzi wa ajali baharini,
- Maslahi ya mabaharia,
- Kutoa leseni kwa Manahodha kwa vyombo vyetu vidogo vidogo.

Mhe. Spika, kazi inayofanywa na Mamlaka hii ni kinyume na haya yaliyokusudiwa. Meli zinazopewa leseni ni mbovu. Meli zote zinazokwenda Pemba zinachukua abiria ni mbovu. Tiketi zinazouzwa na mashirika au Kampuni za meli hii, hizi kila kampuni ina bei yake. Lakini zinakwenda Pemba eti Wapemba wakisafiri tiketi moja ina watu watano, saba. Kwa hiyo inakwenda Pemba iwache iyende iyendavyo.

Mhe. Spika, kupitia kwa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano hii Mamlaka ina dhamana na dhamana ipo kwa serikali, keshakata tiketi mtu anafika bandarini huwezi kumwambia tena usiingie meli imejaa, anachotaka ni safari. Wapemba tukisafiri tunasafiri na ndundu zetu. Mhe. Spika, zile ndundu mtu hana pa kuziweka, akaziweka ndani ya ile meli ndio anaondoka nayo. Sasa

ukimwambia usiondoke meli imejaa hapo haelewi. Sasa ni juu ya Mamlaka kufanya kazi iliyopewa.

Mhe. Spika, juzi kuna meli moja linaitwa sijui Nura, Pemba imeondoka saa 7 ya usiku, Unguja haipo Pemba haijulikani. Kumbe ipo chini Tanga huko ina abiria zaidi ya elfu moja mia tano, mseba mseba mpaka inafika hapa watu wote taabani. Vitoto vyengine vipo Mnazi Mmoja mpaka hivi sasa. Mhe. Waziri hii si hali kwa nini serikali ya Mapinduzi yenye dhamana na watu wake hadi leo imeshindwa kuweka chombo cha uhakika baina ya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika hapo hapo penye Mamlaka tunawashukuru sana wenzetu, Wazalendo wa ndani wamewekeza usafiri wana tusaidia. Mzalendo anapowekeza kwao huyu anadhima hii nchi ni yake pia, anapaswa na yeye kutoa mchango wake. Tunashukuru sana usafiri wa Unguja Dar-es-Salaam lakini bado usafiri wa Pemba-Unguja ni mgumu mno. Ni mgumu kuliko maelezo ninavyoyasema miye hapa.

Mhe. Spika, pamoja na usafiri kwamba tunabebe ndundu, ndundu tunabeba kwenye meli kubwa, hizi Speed Boti hatubebi ndundu tunaziheshimu kwa sababu ni Speed Boti vile vitanda vyetu vya kamba hatubebi mle. Tunachukua kwenye hizi jitihada na Serengeti. Speed Boti sasa inayokwenda ni hii Azam Marine, nyengine zote zimekatisha. Kuna lugha ambayo nimeisikia kwa sikio langu mwenyewe anaambiwa huyu mratibu, usipeleke meli Pemba wataiharibu huo. Lakini ilinibidi nimezee, tunaharibu kivipi, sikumuuliza yule bwana kwa sababu tusingeelewana.

Jengine ni kuwatunza Mabaharia kuna kampuni ya meli zetu hapa. Mabaharia wamepewa barua kwamba kampuni haina uwezo wa kuwalipa mishahara. Sasa wao wanataka ajira kwa kujulikana na umasikini huu tulionao. Umasikini unatupeleka sipo na wenzetu wapo wanaoutumia umasikini wetu kutudhalilisha. Anaambiwa baharia kama utafanya kazi ufanye kwa kujitolea lakini hugaiwa pesa ya sabuni. Anachotaka mwenye kampuni asiwape mikataba hawa mabaharia.

Mhe. Waziri hii Mamlaka yako kama inasimamia na hawa mabaharia miye ndio nakupa hiyo habari. Mabaharia wamepewa barua za kujitolea ndani ya ile meli ya MV. SIGAL, hiyo barua ukiitaka utaniona kwa wakati wako. Tunakaribisha wawekezaji lakini hatuwakaribishi kuja kutudhalilisha, tunajitosheleza kabisa na huo umasikini tulionao. Mbinu za kujitatua tutatafuta wenyewe, lakini hatungependa Mhe. Waziri hali ya namna hii.

Mhe. Spika, mamlaka hii mimi ningemuuliza Mhe. Waziri hivi mamlaka na vyombo vipi, au chombo kipi kinachofuatilia meli zinazoingia ndani ya bahari

yetu. Mbona bahari hii imefanywa shamba la bibi atakae aingie kwa wakati wake na kutoka apendavyo. Mamlaka ipo, mamlaka ya wapi hii. Umeziorodhesha kazi za mamlaka mbona hatuoni kufanywa kazi hizi. Kama wanakudanganya wanakudanganya Mhe. Waziri, lakini kuna madhambi kadhaa na yanatuathiri sisi Wazanzibari.

Mhe. Spika, nije katika kwenye Shirika la Bandari, niungane na wenzangu kumpongeza sana Mkurugenzi huyu kwa kazi nzuri. Lakini nimefika mahali nasema mkurugenzi tunamfanyisha kazi *under capacity* na kutathmini uwezo wake mkubwa aliyonao. Bandari tulizonazo bado ni chache mno kwake. Bandari ya Malindi haijafanya kazi inavyostahiki, bandari ya Mkoani Mhe. Waziri kwenye kitabu anasema anakwenda kuirekebisha, sijui anakwenda kuiendeleza, wapi ilipodidimia pale katikati.

Mhe. Waziri hapa hujatwambia kitu. Bandari ya Mkoani tunaambiwa ni ya Kimataifa. Wafanyabiashara wa Kisiwani Pemba na kwengineko ingekuwa kweli una nia thabiti ya kuifanya iwe ni Bandari ya Kimataifa ili meli zingekuja Mkoani. Kama kweli serikali ina nia ya kuwapunguzia ule umasikini uliostadi kule Pemba bandari ile isingekuwa na hali ile hadi leo. Leo mnavyotambia tuwashawishi wafanyabiashara wa Kipemba walete bidhaa zao Pemba. Wazilete washushie wapi. Hivi kweli karine hii unamtegemea Asaa akapinde mgongo ashushe gunia pale Mkoani au ashushe Hamadi na Kombo. Jamani Bandari Waheshimiwa mnasafiri mnaziona. Msitujengee bandari ya *Rotterdam* lakini kwa hali ya Kizanzibari bandari mmezizarau zile.

Mhe. Spika, bandari za Pemba zimedharauliwa, umasikini unalazimishwa uendelee. Wapemba wanapoondoka Pemba kuja Unguja ni kuja kuhangaikia wapate maisha yao, uwezo wa kujituma wanao, lakini sasa wafanye nini. Ni juu ya serikali yao kuzikuza bandari.

Mhe. Spika, nasema hivi ni visiwa, maisha yetu tunategemea bahari yetu ndio mgodi wetu. Mungu katujaalia tuna bandari Wete, tuna bandari Chake, tuna bandari Mkoani, leo naona hapa pakizungumzwa panatajwa Forodha Mchanga. Forodha Mchanga ni *extension* ya Bandari ya Malindi, Mpiga Duri ni *extension* ya Malindi tunataka Zanzibar kuitangaza ni eneo la biashara Zanzibar yote hii ndio zana tuliyonayo sisi. Zanzibar iwe ni eneo huru la biashara ni pamoja na Mkoani ni pamoja na Wete ni pamoja na Chake. Leo ukinambia Forodha Mchanga lakini unashindwa kuitaja Mkumbuu ambapo ni eneo tukijenga tutakuwa na uwezo mkubwa wa kuwaajiri vijana wote. Mhe. Waziri nataka uje unambie hata Mkumbuu unashindwa kuitaja ndani ya kitabu hichi. Kwa nini?

Hivi kweli kuna sifa Forodha Mchanga kuliko Mkumbuu. Mwenzangu mmoja alinambia pana mwamba kuingia pale ndani. Kwa karne ya leo ukitaja

mwamba pale mtoni ni mto wakokota, mimi tokea navua pale na babu yangu naujua, hakuna kepteni hata mmoja wa meli hawa tuliokuwa tunao hapa atakae kwama kwa mwamba ule. Mwamba ule tukiamua kujenga bandari utakaa kama hapa tunapopita. Mhe. Spika, peupe, si mwamba wa kuzuia meli, meli haizuiliki.

Mhe. Spika, kwa ujenzi wa bandari kama hizi tunazozungumza naamini uwezo wa serikali haupo. Lakini kama nia ipo tutajenga bandari Mkumbuu. Huu ndio uchumi wetu, hapa ndio uhai wetu, hapa ndio ajira ya vijana wetu. Lakini Mhe. Spika, leo tugharamike Forodha Mchanga, kesho tunataka *extansion* ya Malindi tunaanza kazi upya, hesabu hizi hazitufai sasa. Hetu tuende na *vision* ya miaka mia moja mbele, tunakuwa, tunaongezeka kwa idadi kubwa. Tunataka waje wajukuu warithi mambo mazuri tuliyowawekea sisi.

Mhe. Spika, Shirika la Meli, naita ni mradi wa watu miaka yote tunasema hili Shirika linafanya kazi kwa hasara. Wenyewe wanatwambia wanahitaji msaada mkubwa wa serikali waweze kukopa, wakopesheke ili walete meli zitakazofanya kazi. Shirika la Meli si lazima kuwa na Wakala tu. Uwakala unasema na meli zote za serikali, kumbe ni meli mbili tu. Tena panawekwa na jina meli zote, kuna Ukombozi, ikowapi, hiyo Maendeleo siku moja inatembea miezi sita haipo. Mhe. Waziri tunafanya nini?

Mhe. Spika, hii si sifa bwana, Shirika la Meli lina meli mbili, tena serikali ya Mapinduzi! Inawezekana tukawa na shirika bila ya kuwa na meli hata moja na likafanya kazi kwa ufanisi mkubwa ni suala la kukaa tukajipanga. Mhe. Waziri una sifa zako usitie mchanga katika mambo kama haya.

Mhe. Spika, kwa kuheshimu sana muda wako kuna suala la mnara wa Komasha. Mnara huu ni wa Kimataifa asubuhi unawaka usiku hauonekani. Mhe. Waziri hebu twambie kuna nini hasa? Wavuvi wetu wanasafiri kuna mameli ya nje yanategemea mnara huu, huu mnara una *record* kubwa, au kuna matatizo? Hebu twambie lipi lililosibu hapa.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa nimepatwa na mshangao. Tuna eneo hapa Mtoni la UUB wenzetu hawa wanaweka vifaa vyao pale kwa kuendeleza hizi barabara tunazozisema. Leo wanaambiwa wahamishe vyombo vyao waondoke. Mhe. Waziri hebu njoo utueleze keshapewa nani tenaaaa (*Makofi*)

Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake kwa kunipa fursa hii ya kuchangia. Nataka nitumie dakika chache ili nithamini wakati.

Mhe. Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri wa Miundo Mbinu, kwa kitabu chake hiki kizuri sana ambacho kinaeleza maendeleo yetu ya Wazanzibari kwa jumla. Pia nawapongeza wafanyakazi wote wa wizara hii kwa juhudi zao kwa kutuletea maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nataka kueleza katika mradi wa barabara kuu Zanzibar. Katika barabara Zanzibar na mimi ninayo kule Matemwe barabara ya Kijini lakini katika kitabu sikukiona na kama Mhe. Waziri ameniwekea mpango maalum wakuja kunijengea barabara atakuja kunikumbusha lini nimngoje na siku gani tumsubiri atufanikishie hii barabara yetu. Japokuwa ndani ya kitabu haimo lakini naamini Mhe. Waziri atanifanyia.

Mhe. Spika, nakwenda katika barabara za vijijini na mimi kule Matemwe ninazo. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri ndani ya kitabu hiki hamna barabara ya vijijini katika Kaskazini. Mimi namuomba Matemwe ninazo barabara mbili za vijijini, barabara hizi zipo tokea mwaka wa 2005 wakati Mhe. Waziri wa Miundombinu mstaafu Adamu Mwakanjuki barabara hizi zipo. Wananchi barabara hizi ndizo wanazozitumia lakini zipo vibaya sana na hazijapata ufadhili wa kujengwa. Mpaka barabara hizi amazikuta mstaafu tena aliyekuwa Waziri wa Miundombinu, Mhe. Machano.

Namuomba Mhe. Waziri wa Miundombinu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoendeshwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa azione barabara hizi na zipe baraka. Namuomba barabara hizi baada ya kumaliza mkutano wetu wa bajeti nimchukue nikamtembeze azione barabara hizi kwa macho yake.

Nikiondoka katika mpango wa barabara mimi nakuja mradi wa bandari. Mhe. Spika, Zanzibar hivi sasa imekuwa ni nchi kubwa sana na imeshakuwa na watu wengi, hususan upandwa wa Kaskazini, hivi sasa tumekuwa ni watu wengi sana, wengi wetu kula Kaskazini hatuna ajira. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wa Miundombinu aiangalie bandari yetu ya Mkokotoni. Bandari ya Mkokotoni ipo haja hivi sasa ya kuwa Bandari ya Kimataifa. Bandari hii sasa hivi inachukua watu wengi hususani watu wa Kaskazini ‘A’. Ndugu zangu wa Pemba wenye asili ya Kimatemwe wengi wakati wanapotoka Pemba wanataka washuke pale waje zao kwao.

Mhe. Waziri bandari hii kama ataihudumia nina hakikisha italeta uchumi, itaondolesha matatizo ndugu zetu wa Kaskazini ‘A’ na itaondosha matatizo hata ndugu zetu wa Pemba. Namuomba Mhe. Waziri bandari hii imetajwa hata na Mhe. Raisi. Bandari ya Mkokotoni ifanye kazi. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri Bandari ya Mkokotoni aitie katika ilani mwaka wa 2011/2012 kwa sababu mara hii hapa haimo lakini naiyombea hivyo.

Mhe. Spika, nakwenda katika kitabu chake hiki hakina mpango wa ajira, sikuuwona humu kwamba wananchi wataajiriwa, hakuna. Ajira ni tatizo kubwa kwetu sisi, hii Wizara ya Miundombinu ndio wizara kubwa. Ikiwa haitochukua wananchi kuwaajiri, sijui itakuwa vipi. Naiyomba Wizara ya Miundombinu ifanye mpango wa kuwaajiri vijana. Vijana tunao hawana kazi, wameshasoma, wengine mainjinia, Matemwe sisi tunao mainjinia kule wa magari, tuna ma-*engineer* wa kila aina basi namuomba Mhe. Waziri atuajiri na sisi ndani ya miundombinu.

Mhe. Spika, mimi kama nilivyosema kwamba sitochukua muda mkubwa na waheshimiwa wengi wameshazungumza maendeleo yetu, wameshazungumza uwanja wa ndege, wameshazungumza mashirika. Kwa hivyo, na mimi tena haina haja ya kupoteza wakati ila nasisitiza kwamba barabara ya Kijini pamoja na barabara za ndani za Matemwe hizi nasisitiza sana Mhe. Waziri azione. Kwa hivyo, mimi naunga mkono hoja hii kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Matemwe naunga mkono mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya jioni hii kusimama hapa kuja kutoa mawazo yangu juu ya Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano. Pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na hatimae nimshukuru Mhe. Waziri kwa hotuba yake.

Mhe. Spika, mawaziri wetu wote waliopita ni mawaziri wazuri kila mmoja amekisoma Kiswahili kuliko mwenzake, kwa hivyo ni watu wazuri kwa lugha ya Kiswahili katika maelezo yao. Mhe. Spika, baada ya kumshukuru waziri pia nawashukuru na watendaji wake katika wizara yake hii kwa wanavyomsaidia kutengeneza kitabu hiki cha bajeti ya wizara yake.

Mhe. Spika, mimi nianze moja kwa moja kwa barabara zilizomo katika Jimbo langu la Mtambile, nianze na hii barabara ya Mtambile-Mwambe ambayo imepita katika jimbo langu la Kengeja. Katika hotuba yake hii Mhe. Waziri amesema kwamba barabara hii ya Mtambile-Mwambe na Mtambile-Kangani zimekamilika. Lakini Mhe. Spika, hii ya Mtambile-Mwambe bado inamapungufu tena makubwa. Mimi nataka nimwambie Mhe. Waziri kuburuta kitanda si dawa ya nyumba ivujayo, viraka unavyotia bado havikidhi kwa barabara hii kwani hii ni mbovu haifai kabisa pamoja na sifa zote ulizoipa barabara hii, hii ni barabara mbovu tena sana.

Mhe. Spika, barabara haisizimwi, pamoja na kutwambia kwa teknolojia mpya sawa, lakini namwambia kuwa barabara hasizimwi watu wanatia lami kwa mkono juu ya fusi. Mhe. Spika, kwa kweli popote pesa tutakapoipata kama ni ya SMZ moja kwa moja, kama ni ya mkopo, kama ni ya kusaidiwa bado ni

pesa ya serikali na ingefaa itumike vyema, ama pale pesa ya umma imepotezwa bure. Kwa sababu barabara haina kiwango hata kidogo.

Mhe. Spika, bado kanzu iko kwa fundi charahani lakini inatiwa viraka, barabara bado haijakabidhiwa kwa serikali inafanyiwa marekebisho tena makubwa. Kuna matuta makubwa waliyotia mengine yameshang'olewa, kuna sehemu nyengine wameweka alama ya kuwa humu ni sehemu mbovu wanataka kurekebisha. Lakini Mhe. Waziri anasema kwamba barabara hii tayari imekamilika, sijui imekamilika vipi na bado kazi ya ujenzi inaendelea.
Mhe. Spika, hapa kwenye barabara hii kwa kweli pesa yetu imetumika sivyo. Kampuni hii sijui ni kampuni gani ambayo kokoto za Mwambe, Vitongoji na Micheweni hazifai eti mpaka zitoke Kenya. Mhe. Spika, ujenzi wote tangu enzi na enzi hatujaagizia kokoto leo Mhe. Waziri anatwambia kokoto za Mwambe hazifai mpaka ziagiziwe kutoka Kenya. Mhe. Spika, mimi nataka kujua pana nini hapa barabara zote zimejengwa kwa kokoto za Mwambe na Vitongoji lakini kwa barabara hii za Mwambe hazifai tena. Nadhani hawa mafundi waliojenga barabara hii kampuni yake labda inatoka Kenya kwa hivyo watuzidi kete wakatuonesha kokoto za kwao ndio bora ili wapate kuuza zile kokoto zao.

Mhe. Spika, mimi barabara hii inanitia uchungu sana pamoja na sifa nyingi Mhe. Waziri aliyokwishaipa na ataendelea kuipa lakini mimi nasema ni mbovu barabara hii. Kwa hivyo, sasa hivi niache barabara hiyo nije katika barabara ambayo imetajwa kutoka Ole-Kengeja.

Mhe. Spika, barabara hii kaitaja Mhe. Waziri kuwa itafadhiliwa na nchi zinazozalisha mafuta kwa wingi duniani OPEC, lakini hajaitaja itaanza lini. Ningemuomba Mhe. Waziri atwambie hii barabara itaanza lini kwa sababu hapa ameitaja tu hajataja lini itaanza na itaanza wapi? Kwa hivyo, ningemuomba akija atwambie barabara hii itakapoanza.

Mhe. Spika, vile vile ameitaja barabara ya Mkanyageni-Kangani kuwa itaanza barabara hii pale itakapomalizika barabara ya Mgagadu-Kiwani. Je, hiyo barabara ya Mgagadu-Kiwani itamalizika lini ili na hii ya Mkanyageni-Kangani nayo ianze? Halafu Mhe. Spika, katika jimbo langu hili mna barabara nyingi ndogo ndogo ambazo katika mpango huu wa barabara za vijijini niseme kuwa hazikutaja, lakini ningemuomba Mhe. Waziri zimo nyingi moja wapo ni barabara inayotoka Mahudusi kwenda katika kijiji kimoja kidogo cha Sipwese ambacho ndipo ninapoishi mimi, ningemuomba barabara hii aisaidie kwa kututulia kifusi tu wala sitaki lami.

Vile vile kuna barabara inayotoka Mgagadu kwenda Mtadoda, kuna barabara inatoka Mtambile kwenda Jaani, kuna barabara inatoka Kangani kwendea Kuukuu ambayo kipindi fulani Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi barabara hii

aliitaja na Mhe. Waziri alimuahidi kuwa zimalizapo tu mvua za Masika barabara hii ataimwagia fusi. Lakini hadi nasimama hapa bado fusi hilo halijatiwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atekeleze ahadi aliyomuahidi Mhe. Mwanajuma, kwani wanawake ukiwapa ahadi inatakiwa uwatekelezee.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, sasa nije katika bandari yetu ya Mkoani, taehe 28/01/2011 wakati Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mhe. Salim Abdalla Hamad alisema kuwa bandari ile ya Mkoani imezama kidogo kwa sababu yale mawe yaliyopangwa ile nafasi ndogo ilipo baina ya jiwe na jiwe ndio iliyozama kidogo ndio maana ile bandari ikenda chini kidogo. Mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri kwani wakati wa ujenzi huu serikali huwa haina mtu anayeshughulikia hizi kampuni za ujenzi huwa wanaachiwa peke yao hadi itokee namna hiyo.

Pia Mhe. Asaa ameitaja kuwa imefanyia matengenezo lakini mimi sijui imefanyiwa lini, hili sipingi wala sikatai, lakini bado ile bandari ni muhimu na inahitaji ifanyiwe matengenezo makubwa. Hapa Mhe. Raya amesema asubuhi kwamba ule ni mtitio tu na maji yakiendelea kutuama pale juu ikija ikididimia basi watu watazama na watu wakizama huenda wakapoteza maisha yao. Kwa hivyo, tuthamini maisha ya watu wetu.

Mhe. Spika, kuhusu vyombo vya usafiri wa baharini kwa kweli sisi tunaotoka Pemba kuja Unguja tumo katika mtihani mzito juu ya hivi vyombo vya usafiri. Mhe. Spika, usafiri wowote ni *risking* hata chombo kiwe kizima na kipya seuze meli mbovu. Mhe. Spika, meli zetu tunazopanda kutoka Pemba kuja Unguja na kinyume chake Unguja kwenda Pemba Mhe. Spika, kama ingelikuwa tunawajali raia wetu basi meli zile tungelizizuia. Mhe. Spika, mara moja nilifurahi sana Mhe. Waziri alipoipiga marufuku MV Maendeleo kuchukua abiria, lakini siku mbili tatu tunasikia MV Maendeleo inatembea kama kawaida. Mhe. Spika, ilizuiliwa kwa kitu gani na baada ya muda mfupi ikaruhusiwa kwa kitu gani?

Mhe. Spika, kwa kweli bado tuna tatizo kubwa tena sana la usafiri baina ya visiwa vyetu hivi viwili. Mhe. Asaa amesema tuna ndundu zetu Wapema, “ndundu” Waheshimiwa ni mizigo mizito ndio ndundu tunazopakia katika vyombo hivi. Mhe. Spika, Wapemba tukija Unguja tuna mizigo na tukiondoka Unguja tuna mizigo, lakini leo hatuna pahala mizigo hii pakuitia. Mhe. Waziri tufanyie maarifa utupatie meli ya uhakika Wapemba kwa ajili ya kupakia mizigo yetu tukenda Pemba na kurudi Unguja.

Mhe. Spika, kwenye Karakana Kuu ya Serikali Mhe. Omar Ali Shehe amesema takriban magari yote hivi sasa yanatengenenzwa kwenye gereji za watu binafsi na kuacha hii ya serikali. Hapa kwa njia yote ile kuna biashara maalum

inayofanyika baina ya serikali na hizi gereji ambazo tunavipeleka vyombo kwa matengenezo. Mhe. Waziri ningekuomba uimarishe hii ya serikali ili vyombo vyote vya serikali viende katika matengenezo kwenye Karakana Kuu ya Serikali ili kuisaidia serikali kuongeza mapato yake.

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ina jukumu kuubwa la kuhakikisha kuwa Wazanzibari popote wanapokwenda katika kusafiri ama angani, baharini au nchi kavu wanakuwa salama katika safari zao. Mhe. Spika, vyombo hivi vya baharini vinachukua abiria wengi kupita uwezo wake, vinachukua mizigo mingi kupita uwezo wake mara nyengine ile *water table* ya chombo inazama, lakini na sisi wasafiri kwa sababu mtu anaposafiri hajali chochote.

Mhe. Spika, kwa sababu kwenye mashirika yenye usafiri na wao wanataka pesa basi hawajali maisha ya watu, lakini mimi nasema serikali ipo je hao wenye vyombo ndio hawajali je, hata serikali haijali raia wake? Mhe. Spika, mimi sidhani kama haijali lakini pengine imesahau kwa hiyo tunaikumbusha kuwa ihakikishe vyombo vyote vinachukua abiria kulingana na uwezo wao. Mhe. Spika, lile suala la kuwa mtu amechukua tiketi akaambiwa meli imejaa anasema vipi ijae na mimi tiketi yangu ninayo mkononi.

Mhe. Spika, sitaki nipoteze muda zaidi lakini pia katika Wilaya yangu ya Mkoani iko barabara inayotoka Kenya kwenda Chambani, lakini barabara hii matengenezo yake yanamalizia pahala ambapo panaitwa kwa Mtora. Mhe. Spika, kwa Mtora bado hujafika Chambani kuna upande mmoja unaelekea Ukutini na upande mwengine unaelekea upande wa Tumbini ambapo huko ndiko Chambani hasa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri asijesema kuwa katengeneza njia ya Chambani pale kwa Mtora bado ni njia tu yakwenda Chambani huko Chambani hasa barabara bado ni mbovu. Kwa hivyo, ningekuomba Mhe. Waziri usimalizie pale uingie ndani kuelekea Tumbini na uingie ndani kuelekea Ukutini ili watu wa Chambani hiyo barabara walioambiwa kuwa watatengenezewa iwe imetengenezwa kweli.

Mhe. Spika, baada ya machache hayo niseme naunga mkono hoja hii, ahsante sana.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuchaguliwa kushika wizara hii, na pia nimpongeze Naibu Waziri wake na yeye kwa kuchaguliwa kushika nafasi hii.

Mhe. Spika, nikianza na kitabu hiki mimi nitaanza na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Mhe. Spika, niipongeze Wizara ya Mawasiliano kupitia Mamlaka ya

Viwanja vya Ndege kwa kujipangia malengo yakuimarisha viwanja vyetu vya ndege hasa Kiwanja cha Abeid Amani Karume. Mhe. Spika, nitaanza na ujenzi wa *terminal building*, niipongeze serikali kupitia wizara hii na pia niishukuru Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kupitia Benki ya Exim kwa msaada wao huu. Jambo kubwa mimi nilikuwa nawaomba wananchi wa Zanzibar pamoja na wafanyakazi wa *air port* kwa ujumla baada ya ukamilifu wa ujenzi wa jengo hili mimi nawaomba walitunze ili liweze kudumu.

Mhe. Spika, nikiendelea pia naiomba Mamlaka ya Viwanja vya Ndege tusisahau kwamba *old is gold*, pamoja na kwamba *terminal* mpya inakuja pia nilikuwa nawaomba waikuze ile *terminal* ya zamani ambayo inatumika hivi sasa kwani kiwanja hiki chetu cha ndege tunakiita Kiwanja cha *Abeid Amani Karume International Air Port*.

Mhe. Spika, mimi nasema kuna kasoro ndogo ndogo ukiachia hizo kubwa ambazo watu wengine wamezizungumza, kuna kasoro ndogo ndogo. Mhe. Spika, mimi nimesafiri lakini sijapatapo duniani kuona inakosa maji, mheshimiwa hili ni tatizo naiomba wizara hayo makuwa wakipata uwezo wayafanye, lakini haya mambo madogo wangeondosha kero hizi ndogo ndogo. Lakini pia Mhe. Spika, ile ni International Air Port wakati wa ku- *board* International Air Port hatu-*expect* mtu kusimama kule akasema abiria wanao-*board* na Ethiopia tayari ndege inaondoka. Mhe. Spika, hata vipaza sauti kama hiki cha kutangaza jamani ndege fulani sasa hivi ina *board*. Hilo ningeomba pia wizara iliangalie kwa makini zaidi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo sasa naingia katika Shirika la Bandari. Mhe. Spika, mimi tangu kuingia katiba Baraza hili nimeshahudhuria kama vikao vitatu vya *briefing*. Mhe. Spika, Wajumbe wa Baraza hili wanalalamika sana kuhusu *V.I.P Lounge* bandarini. Na mimi naungana na maneno ya Mhe. Asha Bakar kwamba kama serikali inaona ugumu wa kujenga *V.I.P Lounge* pale kwa nini hatumpi huyu mzalendo mwenzetu akatujengea, iweje ajenge kule kwa wenzetu aje ashindwe kutujengea sisi hapa. Kwa hivyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri labda aje atueleze kama kuna ugumu wowote katika hili.

Mhe. Spika, pia nilikuwa namuomba Mhe. Waziri atufafanulie kwamba kwa nini siku hizi *car carrier ship* haifiki Zanzibar inafika Dar es Salaam inashusha gari, gari zinapakiwa kwenye Buraq na Aziza ndio zinakuja hapa Zanzibar. Mhe. Spika, gari hizi zinapotolewa kwenye zile meli na kuingizwa kwenye Buraku kunahitilafu hitilafu ndogo ndogo zinatokea ambazo zinatutia hasara sisi na badala yake hujui hata umshike nani ambaye ni *responsible for damage*. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nilikuwa nataka Mhe. Waziri atufafanulie kwa nini *car carrier ship* sikuhizi haifiki Zanzibar inaishia Dar es Salaam. Lakini pia Mhe. Waziri ningemuomba atufafanulie ni shilingi ngapi serikali kuwa

inaingiza wakati meli hii ilipokuwa ina *dock* hapa na sasa hivi shilingi ngapi inapoteza ambapo meli hii haifungi gati hapa tena inafunga kule kwa wenzetu Dar es Salaam.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nilikuwa nataka niingie kidogo kwenye sekta ya mawasiliano kuhusu Zantel. Mhe. Spika, naomba niishukuru Zantel sana kwa kuisaidia serikali na jukumu la ajira, vijana wengi wamepata ajira kupitia kampuni hii. Lakini nilikuwa naiomba hii Kampuni ya Zantel isitupatie zile ajira za upota tu, tunaenda huku tunahangaika huku na zile *high post* pia watupe. Mhe. Spika, nawajua Wazanzibari wachache ambao wapo wanafanya kazi katika kampuni hii na wapo katika *high post* lakini wale wengi wao ni wale wanaopeleka vocha huku, wanaokaa vibandani kutwa nzima. Kwa hivyo, Mhe. Spika, na hili nalo pia waliangalie zile *white colour job* wasichukue wao na sisi pia watupatie.

Mhe. Spika, baada ya hapo nilikuwa nataka niingie kidogo kwenye Mamlaka ya Usafiri Baharini. Mhe. Spika, hapa nilikuwa nataka Mhe. Waziri atupatie maelezo kwamba kuna nini Mamlaka ya Usafiri Baharini hakuna vyombo vya kutizama hali ya hewa au vipi. Mhe. Spika, maana naona siku nyengine hasa kwa vyombo vinavyokwenda Pemba abiria wana-*board* kama kawaida lakini wakifika Nungwi wanarejeshwa wanaambiwa hali ya hewa mbaya Pemba hakwendeki na hivyo kuwapatia usumbufu wananchi. Mhe. Spika, hili pia nilikuwa namuomba Mhe. Waziri akija hapa atupatie ufafanuzi. Mhe. Spika, baada ya hayo kwa niaba ya vijana wote wa Zanzibar na pia kwa niaba ya wanawake wote wa Mkoa wa Mkoa wa Kusini Unguja naunga mkono hoja.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak: Mhe. Spika, ahsante sana kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia jioni hii kuwa na uzima pamoja afya na kuweza kutekeleza majukumu yetu. Pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nitoe maelezo yangu machache katika hotuba hii. M

Mhe. Spika, katika miaka mitano niliyokaa katika Baraza la Wawakilishi vitabu vingi vya hotuba vya bajeti huviona vinaanza na alhamdulilahi, lakini hotuba hii ya Mhe. Waziri imeanza kwa bismilahi kwa huu unaonesha ni ufanisi mkubwa wa Mhe. Waziri ana utaalamu wa engeneer, lakini katika miongoni mwa maulamaa na yeye ni mmoja wao. Kwa hivyo, kwa maana kwa kuanza kwa jina la Mwenyezi Mungu hapa basi na mimi nimpongeze Mhe. Waziri kwa hili kwani kuanza jina la bismilahi inaonesha manufaa mazuri, na utekelezaji mzuri wa mipango yote ambayo aliyoiandaa katika bajeti yake. Kwa hivyo, inshallah Mwenyezi Mungu kwa kuanza jina hili Mungu atamsaidia.

Mhe. Spika, mimi nianze katika hili Shirika la Meli. Mhe. Spika, kusema ukweli kitu ambacho hakinunuliwi ni roho ya mwanadamu kwa kweli meli zote

ni mbovu, kwa hivyo basi mimi ningeliomba kama serikali haiwezi kununua meli basi ushauri wangu ningemuomba Mhe. Waziri hili shirika bora livunjwe. Mimi nadhani hii itakuwa ni bora zaidi.

Nikiondoka hapo nije katika suala zima la ujenzi wa barabara. Mhe. Spika, kwanza nimshukuru waziri kwa kuona hivi sasa barabara nyingi zinafanyiwa matengenezo, lakini ningelimuomba Mhe. Waziri awe na umuhimu mzuri wa kuona zile barabara za *feder road* nazo zina umuhimu mkubwa. Kwa mfano, hivi sasa kuna matengenezo ya barabara ya Mwanakwerekwe, tukiacha hayo matengenezo yaliyopo mvua za karibuni tu zilizokuwa nyingi Mwanakwerekwe palijaa mengi.

Kwa hivyo, njia ya Mwanakwerekwe ilikuwa haipitiki na kuna barabara ambayo inatoka Nyumba Mbili inatokezea Kwa Mchina gari nyingi zilikuwa zinapita njia hivyo na nyengine nyingi zilipita njia ya Makaburini na kutokea Ijitimai ya zamani. Ukitizama leo barabara kubwa haipitiki lakini hizi *feder road* ndizo zilizokuwa zikatumika, lakini katika utumikaji wake je nazo ziko katika hali nzuri? Madereva wanapata tabu ya kutosha ndio maana nilipomuomba Mhe. Waziri awe na umuhimu wa kuzitizama hizi *feder road* nazo zina umuhimu wa pekee. Ningelimuomba Mhe. Waziri kila penye njia hizo basi apape kipaumbele.

Hivi sasa kuna ujenzi wa barabara ya Mwanakwerekwe ikifika saa tatu barabara imeshafungwa, msongamano wa magari yote yale yanapita katika njia hizo za *feder road*. Hivi sasa Mwenyezi Mungu katujaalia kuna jua kali kwa hivyo njia zile zinapitika, ingelikuwa mvua ingekuwa hatari sijui gari zingepita wapi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri suala la *feder road* kila penye kichocho ambapo tunajua hizi njia zinatumika basi Mhe. Waziri azipe kipaumbele. Ukitizama kwa wenzetu kila penye njia za ndani basi zimejengwa, sasa na hizi ni njia ambazo zina maana yake mjini na mashamba.

Kuna njia moja Mhe. Waziri katika eneo la Koani Kibonde Maji naomba uwatizame wananchi hawa ni njia ambayo iko mbali na barabara kubwa, wananchi wakilima wanapata tabu kutoa mazao yao, hivyo njia hizi tuzione Mhe. Waziri.

Jengine Mhe. Spika, nije katika Idara ya Usafiri na Leseni. Mhe. Spika, niliwahi kuzungumza katika Wizara ya Makamo wa Kwanza wa Rais, nilimuomba Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais wizara yake ikae na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuona haya manyanyaso wanayoyapata walemavu katika daladala. Mhe. Spika, na leo nasisitiza tena kwa Mhe. Waziri wa Miundombinu nakuomba mzungumze na madereva wa daladala jinsi wanavyowanyanyasa wenzetu wenye ulemavu.

Nikiacha hapo pia na wanafunzi wanapata matatizo makubwa ndani ya magari. Tukitizama daladala madereva wetu nao wanabeba roho zetu, lakini Mhe. Spika, jinsi waendesha daladala wanavyo fujo naweza kuthubutu kusema sisi wanawake hatuna uso humo barabarani. Kwa sababu yale mambo ya kiajabu wanayosema madereva mimi naweza kusema wanawakashifu mama zao, unasikia maneno ya ajabu tu na hatajwi baba anatajwa mama ndiye anayekashifiwa pale. Kwa hivyo, ningeomba hizi leseni zinapotolewa zitizamwe sio mtu kaja kasokota nywele anapewa, mle wanabeba roho nazo hazina duka la kukunua.

Mhe. Spika, unaikuta daladala inafukuzana na daladala nyengine anataka kuigonga hali ya kuwa ndani ana abiria kapakia. Alisema mchangiaji mmoja hapa, akasema hawa polisi nao wanakula rushwa sana, kweli hakuna chochote kinachofanyika. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri muda mrefu tangu Baraza lililopita madereva wanapigiwa kelele, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanapiga kele kuwa tuwe na utaratibu mzuri ili tuone kuwa kuna usalama wa roho zetu.

Mhe. Spika, jengine kuna suala moja lina manung'uniko yanatokea na manung'uniko haya hutokea kwa wananchi baada ya kutengenezwa barabara. Tulikuwa tuna matengenezo ya barabara ya Tunguu/Kinyasini *Alhamdulillah* namshukuru Mwenyezi Mungu, tuna barabara nzuri, gari zote sasa hivi zimehamia Tunguu hadi Kinyasini ni barabara ambayo magari mazuri mazuri yanapita kule sasa hivi. Lakini kuna manung'uniko baada ya kumalizika ujenzi ule, kuna vijana waliajiriwa kuchimba mitaro ya maji katika barabara zile, lakini hadi leo hawajapewa kile kisaidizi chao. Kwa hivyo, sijui Mhe. Waziri suala hili liko katika ofisi yako unalielewa, na kuna utaratibu gani vijana hao ambao mpaka leo wana manung'uniko na suala hili. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri hili uje unipe jibu wajisikie vijana wale na wao au wajue njia gani wapite ili wapatiwe hiki kifuta jasho chao walichokitumia wakati ule wa ujenzi wa barabara na bara bara ile ni ya muda mrefu sasa.

Jengine Mhe. Spika, watu wa Tunduni, Mchangani. Kuna manung'uniko kwamba kuna baadhi ya wananchi walioharibiwa vipando vyao bado hawajapatiwa malipo yao. Hili nalo namuomba Mhe. Waziri aje anipatie jibu, kwa sababu umeshakuwa muda mrefu haupungui miaka minne au mitatu kama sijakosea tangu kumalizika barabara ile wanaona kimya juu ya hali hiyo kupatiwa mafao yao.

Basi Mhe. Spika, mengine niyaache siwezi kurejea rejea. Kwa hivyo, nakushukuru na naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia Hotuba ya Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano nashukuru sana. Mhe. Spika, kwanza kabisa niende moja kwa moja katika Mradi wa Barabara Vijijini Kaskazini Pemba.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Marekani kwa kupitia Mfuko wa Changamoto ya Milenia ya *MCC*, kwamba Kojani ni moja wapo iliyofaidika.

Mhe. Spika, tuna matumaini makubwa sana kwamba watu walioathirika na kuvunjiwa nyumba zao pamoja na vibanda vyao tayari wameshalipwa. Lakini pamoja na matumaini hayo, wako wengine hawajalipwa. Namuomba Mhe. Waziri kama hilo lina ukweli ndani yake atapokuja hapa anieleze.

Vile vile Mhe. Spika, tumepata faraja kubwa kwa kusikia jambo hili ambalo litawasaidia wananchi wa Jimbo la Kojani, ambapo watu wengi wa Jimbo la Kojani huenda kisiwani Koojani kufanya biashara zao ndogo ndogo watapata urahisi wa kufanya shughuli zao za maendeleo. Tunashukuru sana.

Pamoja na faraja hiyo, lakini bado ndani ya Jimbo la Kojani kuna barabara ambazo ni *feder road* hazipitiki. Naomba nizitaje barabara hizo. Mhe. Spika, barabara ya Kiongoni kupitia Kimango ina hali mbaya, tunaomba Mhe. Waziri aiangalie kwa kina. Vile vile barabara ya Mtijuu kupitia Maziwani/Shengejuu, tunaomba na hii itizamwe pamoja na barabara ya Kitambuu/Kiwani. Mhe. Waziri barabara hii wananchi tayari wameshatupa nguvu zao wameshaisafisha bado kumwagwa kifusi tu. Namuomba Mhe. Waziri atusaidie kwa fusi tu ili njia ile ipitike vizuri kwa sababu kuna wazalishaji wengi wa kipando cha mwani, watapata faraja kutumia njia hiyo.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niende moja kwa moja katika Shirika la Bandari kwenye ukurasa wa 31. Mhe. Spika, nichukue tena fursa hii kulipongeza Shirika la Bandari kwa utendaji mzuri wa kazi zake pamoja na kuifanyia matengenezo Meli ya Jitihada ambayo sasa hivi ukiiona ni mpya kabisa inaleta matumaini mazuri.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu ni mjumbe mmoja wapo wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi niliwahi kuipanda meli hii na *engineer* wake mzuri na imerudi katiak upya, pamoja na watu kutaja pesa nyingi zilizotumika kuwa zimetumika vipi, lakini zimetumika kihalali. Tunawapongeza sana.

Pamoja na hayo Mhe. Spika, lakini bandari ina changamoto kubwa sana ambazo ni vitendea kazi. Ukiangalia vitendea kazi hawana kwani bandari nzima tagi ni moja tu na sisi tunategemea meli za nje zinazoshusha makontena,

meli zile kunapokuwa na upepo tagi moja ikiharibika basi shughuli zote za bandarini zimekwama. Mhe. Spika, tunamuomba waziri aiangalie kupitia bajeti hii. Kwa sababu tagi moja ina thamani ya shilingi 16 bilioni ile tunayoiona pale, lakini siku ikizimika je, kwa sababu tagi inasaidia kufunga gati mbili hasa wakati wa upepo.

Mhe. Spika, pamoja na hayo kuna ufinyu wa bandari. Makontena yanayoingia pale ni mengi sana bandari yetu haitoshi. Tunaomba Mhe. Spika, kupitia waziri wetu au wizara hii yale malengo ya kujenga bandari mpya Mpigaduri basi yaendelezwe kwa sababu bandari haikidhi haja.

Vile vile ndani ya bandari hii kwa upande wa chelezo na majahazi pamoja na wavuvi wanaoingia pale ni sehemu finyu ambayo inaleta mgongano wavuvi wanaporudi baharini wanapata kadhia hawaegeshi vyombo vyao kwa usalama na kuuza samaki wao kwa usalama. Pale hutokea matokeo ya kugongana na kuharibiana mashine zao. Jambo hili liangaliwe kwa kina angalau kama kuna sehemu ya kuwapeleka watu wa majahazi wanaposhusha mizigo na kupakia na wavuvi wapate kuegesha vyombo vyao katika sehemu ile.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nije katika Sekta ya Usafiri wa Baharini. Katika sekta hii vile vile niipongeze sana, naipongeza kwa vyombo binafsi wanajitahidi kutoa huduma. Nilipokuwa katika Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi tulipokutana na wenye vyombo na kubadilishana mawazo na kwa kweli ushauri wetu waliusikiliza. Kwa sababu katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba tuna ubovu wa usafiri na hii ndio njia yetu kuu tunayotumia kama watu wa visiwa. Lakini kulingana na usafiri tulionao baso hauridhishi, unaweza kupanda meli kutoka Unguja kwenda Pemba kama umetoka safari ndefu sana kutokana na uchovu wa kwenye meli vyombo havina hadhi ya kubeba abiria, nathubutu kusema hivyo.

Mhe. Spika, mtu anapopanda meli hizi hata akifika anakuwa mgonjwa, wengine wanafika wiki hawajakuwa wazuri ni tatizo. Tunamuomba Mhe. Waziri aliangalie kwa kina, kweli tunapata huduma.

Juzi tu Jumapili meli zilizokwenda Pemba kwa siku moja usiku ni meli tatu naomba nizitaje, moja ni Meli ya Braki, Seagull na Noora, lakini zote ni mbovu. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri anayetoa vibali katika vyombo vyetu hivi atoe vibali kama zinakidhi haja kama wananchi wanasafiri bila ya matatizo.

Mhe. Spika, tulipokutana na wenye vyombo hawa walisema kwamba Pemba hatuwezi kupeleka vyombo kwa sababu wana mizigo mikubwa, lakini tumeshuhudia Unguja na Dar es Salaam nao wanabeba mizigo mikubwa,

yakiwemo mafriji na televisheni. Sasa kule mtu anabeba mkungu wa ndizi utamwambia kwamba ni mzigo mkubwa, anabeba kombe ni mzigo mkubwa, haiwezekani. Yeyote mwenye kubeba mzigo mkubwa basi atapanda meli ya Braki au Aziza, hizi ndizo meli za mizigo, lakini tunaomba *speed boat* zifanye safari zake Unguja na Pemba kama inavyofanya safari Unguja na Dar es Salaam, mwenye uwezo atakwenda kwenye *speed boat* na aliyekuwa hana uwezo atapanda meli aliyokuwa na uwezo nayo, lakini tuwe na mtandao huo.

Mhe. Spika, Shirika la Meli. Shirika hili limebakiwa na meli mbili , Meli ya MV. Ukombozi na Meli ya MV. Maendeleo, lakini meli ya MV. Maendeleo imezidi kuwa katika hali mbaya tutabakia na uwakala tu, lakini meli hatuna. Kwa hivyo, tunaliomba Shirika la Meli kutupatia meli mpya kwa kuzingatia kama sisi ni watu wa visiwa tena zenye hadhi ya kubeba abiria na mizigo. Mhe. Waziri atapokuja hapa tunamuomba atupe maelezo ya kina kuhusu kupatikana kwa meli.

Mhe. Spika, katika mambo ya usafiri wa baharini wenye kampuni zao hizi za usafiri bado wanaendelea na tiketi kuziuza kwa walanguzi, hili linaendelea kila siku hata jana nimeshuhudia. Unakwenda kukata tiketi unaambiwa hakuna, lakini anayekwambia hakuna anakwambia zipo mbili hizi au tatu unataka ngapi? Hili ni tatizo, tunaomba tuuziwe tiketi katika maofisi yao waliyoyajenga na kama zimemaliza tujue kwamba tumekosa safari kuwa tiketi zimemaliza, lakini suala hili hatulipendelei. Tena Mhe. Spika, ukiwakuta hao wanaouza tiketi wengi ni mateja, unakwenda pale mtu anakwambia hii, hili halisaidii Mheshimiwa, tunaomba tudhibiti kweli kweli. Tuna matumaini sana na Serikali ya Umoja wa Kitaifa kama itarekebisha mambo.

Kwa haya machache Mhe. Spika, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa dhati kwa kunipa nafasi hii jioni hii kuweza kuchangia Hotuba ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, mimi nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri, Naibu wake pamoja na watendaji wake wote kwa namna wanavyojitahidi kwa utekelezaji wa kazi zao za kila siku. Mhe. Spika, mimi naomba kuchangia kama mambo matatu au manne, lakini zaidi nitaanzia na suala la barabara.

Mhe. Spika, mimi kiswahili kidogo kinanipa tabu sana, katika kitabu hiki kimeelezea katika majukumu ya barabara ni utengenezaji na utunzaji. Mimi Mhe. Spika, ninapoambwia suala la utunzaji maana yake kitu chochote kilichotengenezwa ni kukitunza ili kiwe vizuri. Sasa mashaka ninayoyapata

katika Kiswahili kinachonipa tabu, mimi nafikiri kulikuwa na haja ya kuandika hasa, kwamba ni utengenezaji wa barabara na utunzaji wa baadhi ya barabara.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu zangu za msingi. Katika jimbo langu la Kwahani lote kwa kawaida limezungumzwa na barabara, barabara kubwa mbili lakini na barabara ndogo zisizopungua nane. Lakini kabla sijaendelea na chochote nimshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Mawasiliano aliyepita Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Machano katika kipindi chake alijitahidi kuzifanyia hiyo lugha ninayozungumza ya kutunza barabara, barabara nyingi zilifanyiwa marekebisho, zikaparwa na kuwekwa lami mpya, lakini kile Kiswahili cha kutunza baadhi ndio kinakuja hapa. Mhe. Spika, nina vibarabara vyangu viwili ambavyo havizidi mita 300 kwa kila barabara. Barabara ya kutoka Mwembevjugu/Mikunguni na barabara ya kutoka Kwajuma pweza/Kwalamsha *Bridge*, najiuliza sababu ya kuachwa Mheshimiwa, zote zimetengenezwa lakini hii imeachwa kwa sababu gani.

Mhe. Spika, barabara hii sina la kuielezea sana kwa sababu unaifahamu vya kutosha, sijui kama inafika siku tatu kama hujapita. Sio wewe tu, hata Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ndio njia yake kubwa. Mhe. Spika, hizi barabara zimeunganisha barabara kuu na zina umuhimu wake, lakini hazistahiki hata kuitwa barabara kwa mazingira ilizokuwanazo. Mimi nashangaa sana kwamba barabara ile imewekwa matuta unaweka matuta ya nini wakati barabara haipitiki, matuta yawekwe kwenye barabara iliyotengenezwa ambayo inapitika gari kwa kasi ili kupunguza mwendo wa kasi wa magari, lakini unakwenda kuweka matuta njia ambayo ina mashimo matupu, huku ni kupoteza fedha za serikali tu, unaweka matuta wakati barabara haipitiki.

Mhe. Spika, barabara hii ina umuhimu mkubwa sana, barabara hii ni kiunganishi na inapotokea matatizo basi magari yote yanakuwa yanapita katika njia hizi. Wakati wa sikukuu ndio barabara kubwa ambayo inatumika kwa ndugu zetu au watoto wetu wanaokwenda katika Viwanja vya Demokrasia. Mheshimiwa Uwanja wa Demokrasia hawishi kufanyika sherehe za kitaifa, magari mengi ya baadhi ya viongozi yanapita hapo kuondosha msongamano katika barabara kubwa, barabara hiyo unaelekea sokoni, barabara hiyo pana skuli kubwa ambayo Mhe. Spika, kila wakati unakuja kuleta watoto wako, nashangaa tatizo liko wapi.

Mhe. Spika, nimekiangalia kitabu hiki na Mhe. Waziri kajitahidi sana, kaelezea mpango wa mradi wa *World Bank* kutengeneza barabara lakini amezigusa nyingi mimi kanigusa pembeni tu kati kati kaniacha, imo barabara ya

Magomeni/Kariakoo, barabara ya Amani/Kariakoo. Mhe. Spika, naomba kwa dhati Mhe. Waziri pamoja na kwamba barabara hii haiko katika mpango wa serikali bado aipe umuhimu au kipaumbele kupitia eneo la Mfuko wa Barabara kuifanyia ukarabati.

Uwanja wa Demokrasia hufanyika mikutano kama nilivyoelezea na mikutano ni mikutano, wakati mwengine mikutano haimaliziki katika hali ya utulivu na pale wanapita viongozi wetu wa kitaifa. inapotokea dharura kiongozi anaweza akapita njia za ndani ili kutafuta njia nyengine na Mheshimiwa hili limeshatokezea tutakuja kuhatarisha usalama wa viongozi wetu. Kuna kipindi kiongozi alipita chini ya nyumba yangu *speed* kubwa wakati njia haipitiki, hii ni hatari, ni vizuri njia hizi tukaziboresha ili zipitike katika hali iliyokuwa inastahiki. Nina imani Mhe. Waziri atakuja kunieleza vizuri na nina imani kwamba atakuja kunisaidia kwa hili. Mimi hofu yangu kubwa ni katika hili, nafikiri sijuo kuna hofu ya nini.

Mhe. Spika, barabara hii Mhe. Naibu Waziri ndiko alikozaliwa, Mkurugenzi wa Bararabara ndiko alikozaliwa, sasa sijui tatizo liko wapi labda wana hofu wakitengeneza wataambiwa wanatengeneza barabara za majumbani kwao. Sasa hilo wasilitizame wawatizame wananchi wa lile eneo wanaotumia barabara.

Jengine nije katika suala hilo hilo la barabara, ningeomba tusaidiane na ndugu zangu wa mawasiliano. Pamoja na ukarabati wa barabara lakini bado barabara zetu zinakuwa na mapungufu makubwa sana, barabara zetu zimekuwa barabara za juakali lakini wakati wa mvua barabara hazipitiki hata safari zako ukitaka kwenda hufiki. Barabara zote zilizofanyiwa ukarabati bado zina matatizo makubwa ya *drainage*, barabara haziwekewi *drainage* pembeni, barabara ya Magomeni ikinya mvua haipitiki, Kariakoo ikinya mvua hakupitiki, Afisi Kuu ikinya mvua hakupiti, Miembeni hapapitiki, Mheshimiwa kuna haja ya barabara hizi kuangaliwa kwa umakini katika matengenezo yake.

Sio hilo tu, barabara zetu pia haziweki maeneo maalum ya kuvuka kwa walemavu. Mlemavu anapotaka kupita kuanzia Darajani mpaka Malindi inabidi atafute eneo maalum zinapokatishwa gari, lakini vyenginevyo katika maeneo ya kawaida basi hakuna maeneo ambayo yamewekwa kwa mlemavu kuweza kupita na kigari chake kwa urahisi. Hili nalo kuna haja ya kupewa kipaumbele, kila tunapotengeneza barabara basi tujue kama tuna wenzetu wanahitaji nao kuzitumia katika hali yao ambayo Mwenyezi Mungu amewajaalia.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije katika Shirika la Bandari. Kama tutakuwa tunakumbuka nchi yetu katika miaka ya karibuni ilipata janga la kitaifa kwa Meli ya MV. Fatih kuzama pale bandarini, kama sikosei natumai kwamba

paliwahi kuundwa tume ya kufuatilia chanzo cha ajali ile, lakini mpaka leo sijapata kusikia ripoti ya tume ile.

Ajali Mhe. Spika, ni ajali hatuwezi kujua ajali ile imesababishwa na nini, ili na sisi tuweze kuisaidia serikali kuweka miundombinu yakuweza kujakuepusha pindipo itakapotokezea ajali nyengine. Mhe. Waziri naomba hili nisaidiwe kuweza kupata hali halisi ya ile taarifa ya kamati iliyoundwa ili tuweze kujipanga vizuri katika masuala yetu ya kutumia bandari zetu. Kwa sababu Mhe. Spika, ile meli ilizama bandarini. Kwa hivyo, ni vyema tukajua ni nini tatizo ili tukaweza kujiweka sawa na matatizo kama hayo kujakutokezea siku nyengine.

Mhe. Spika, jengine wenzangu wengi wameongelea ni suala la kujengwa eneo la VIP bandarini, kujengwa eneo la kupumzika kwa wale wanaosafiri bandarini. Mhe. Spika, hili suala lina umuhimu wake kwa sababu tayari athari nyingi zinaonekana wakati wa kusafiri. Mhe. Spika, sasa hivi imekuwa tunapata usumbufu wa baadhi ya watu kutokusafiri kwa wakati kutokana na kadhia hii.

Sababu ya kusema hivyo Mhe. Spika, ni kwamba kuna baadhi ya wakati viongozi wetu wa kitaifa wanatumia boti hizi na kiongozi anakwenda kwa *time* yake. Inafika pahala Mhe. Spika, kwa sababu hakuna maeneo maalum ya kuwaweka watu sasa inabidi tucheleweshwe kupanda boti na kuondoka kutokana na kadhia hii. Lakini ukiacha hilo hata hilo jengo lenyewe la kusubiri basi mazingira yake hayastahiki. Eneo ambalo tuombe Mwenyezi Mungu wakati wa kusafiri isinyeshe mvua, lakini ikinyesha mvua basi inakuwa ni maudhi na balaa tupu. Kuna haja ya kutoa umuhimu wa kuweka jengo katika eneo la bandari yetu kwa wasafiri wanaosafiri pale.

Mhe. Spika, nije kwenye Shirika la Meli. Sisi wengine huwa tunajiuliza kulikoni Zanzibar. Mhe. Spika, huwa tunajiuliza hivi kwa sababu kila kilichoanzishwa Zanzibar basi hakina mwisho mwema. Tulianzisha Bizanje haikumalizia vizuri, tumeweka viwanda vidogo vidogo havikumalizia vizuri. Viongozi wetu walinunua mabasi hayakumalizikia vizuri, zimenunuliwa meli Mhe. Spika, hazikumalizikia vizuri. Lakini uzuri huu uko kwa wale waendeshaji meli tu. Viongozi wote wa Shirika la Meli wana majumba matatu matatu ya ghorofa, lakini meli hazieleweki. Suala hili linasikitisha.

Mhe. Spika, hiki ni kisiwa. Kisiwa ndio kisiwa Mwenyezi Mungu atuepushie mbali, lakini litakapotokezea tatizo hatuna njia za kukimbilia zaidi ya kuwa na meli au kutumia ndege. Mhe. Spika, hii ni nchi kamili, nchi hii haina meli zake za abiria, nchi hii haina ndege yake ya serikali. Mhe. Spika, naomba kwa dhati kabisa na niwaombe ndugu zangu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano

kuna haja ya kuhakikisha tunapata meli ya serikali ili kuondosha matatizo kwa abiria wetu.

Mhe. Spika, taasisi binafsi zina matatizo yake, kuna mambo yako wazi, ukiuliza sababu za msingi hupewi, leo tuna boti zetu ukitoka Dar es Salaam kuja Zanzibar Shs. 15,000/- lakini boti hiyo hiyo ukitoka Zanzibar kwenda Dar es Salaam Shs. 20,000/- tatizo liko wapi. Mhe. Spika, kuna haja ya kutafuta meli zetu wenyewe, naamini kwamba uwezo huu upo linalohitajika ni kujipanga vizuri tu.

Mhe. Spika, mimi asubuhi hapa nilikuwa namsikiliza kwa makini na nilimsikiliza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano. Mhe. Spika, leo nilikuwa najiuliza Mwenyekiti kulikoni, kila akikaa Magufuli Magufuli, haya sio Magufuli haya ni mafunguo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kilichonipa tabu baada ya kupata *paper* ambayo sitoizungumzia sana, ambayo yeye mwenyewe Mwenyekiti ametumiwa nakala, lakini pia hili halioni. Sitozungumza kwa sababu Mwenyekiti wangu na kwa sababu ndio kwenye kamati yetu na sisi, lakini ametumiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu, Mhe. Hamza Hassan Juma, ameshazungumza kwa upeo kabisa, kwa hivyo sitoizungumzia sana. Lakini kuna haja ya kuangalia hali halisi ya watu ambao wanataka kuanzisha miradi katika nchi yetu.

Mhe. Spika, hii *paper* ina masikitiko makubwa sana, kumuona mwekezaji pamoja na kuwa ni mzalendo hafuati taratibu, lakini vifaa vya serikali vinatumika na vifaa hivyo hivyo baada ya kutumika vinarudishwa katika mazingira ambayo sio mazuri, inapelekea serikali yetu kuitia hasara. Mhe. Spika, jambo hili silizungumzii sana, kama sikosei hata na wewe nakala unayo kama itakuwa imekufika kwa mujibu wa maandishi.

Mhe. Spika, nimalizie kuhusu uwanja wa ndege. Mhe. Spika, katika uwanja wa ndege kulikuwa na karakana, kwa Kiswahili wengine wanaita hanga. Kabla ya kitengo kile kuvunjwa serikalini au baada ya kuvunjwa kitengo kile kuondoshwa katika serikali, kuna fununu kwamba kilichukuliwa na mtu binafsi, baada ya kuchukuliwa sasa hivi inasemekana kwamba kimekodishwa katika eneo jengine. Katika kitabu hiki sijaona kwa sababu suala la kukodishwa au kuondoshwa katika eneo moja kwenda eneo jengine imani yangu kwamba pale pahala panaingizia mapato serikali. Sasa sijaona kitengo kile wapi kilipowekwa na ni mapato gani yanapatikana na nani kapewa na amepewa kwa kufuata utaratibu gani na amepewa kwa kufuata sheria gani. Mhe. Spika, naomba hili nipatiwe ufafanuzi wa kutosha.

Mhe. Spika, mimi naungana na Mhe. Mwenyekiti wangu, ambaye aliomba iundwe kamati hapa ya kufuatilia maeneo karibuni matano. Kampuni ya mizigo ya Zanzibar kunyang'anywa *tender* na mengine mengi. Mhe. Spika, katika kamati itakayoundwa na nina imani kwamba leo kamati hii itaundwa basi na suala hili la hanga ya uwanja wa ndege liongezewe katika kamati yako kulifuatilia ili kujua ukweli wa suala hili kwa manufaa ya Serikali ya Zanzibar na wananchi wake.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, mimi siungi mkono hoja ya hotuba hii mpaka nipate maelezo kamili ya Mhe. Waziri naomba kukaa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri kama walivyokwisha kuchangia wenzangu. Lakini na mimi sitokuwa na mchango mkubwa kwa vile wenzangu wengi wameyazungumza.

Vile vile nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii tena nadhani umeniona kwa sababu ya hii rangi ya kanzu yangu na yako wewe zimefanana. Naamini Mhe. Spika, kwa Mwenyezi Mungu hakuna kubwa, huwenda mwaka 2015 na mimi nikawa Spika.

Mhe. Spika, mimi naanza na wizara ya Mhe. Waziri kuhusu mawasiliano Pemba. Idara hii ya Mawasiliano ni muhimu sana katika sehemu ya idara zake Mhe. Waziri. Lakini cha kusikitisha idara hii imekosa muelekeo wa kufanya kazi. Kwa mfano idara hii inahusika moja kwa moja kufuatilia matukio ambayo yanatokea moja kwa moja katika barabara.

Vile vile cha kusikitisha zaidi idara hii haina vitendea kazi, zaidi ni gari la kufanyia kazi, ambapo gari hili Mhe. Spika, wakati inapotokea ajali huwa gari ni moja tu na siku nyengine gari hiyo huwa inatakiwa sehemu nyengine ambapo iweze kufanya kazi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ajitahidi katika Idara hii ya Mawasiliano Pemba aipatie gari ili waweze kufanya kazi zao vizuri na kufuatilia ajali za barabarani zinapotokea.

Mhe. Spika, nije kwenye Shirika la Bandari. Shirika hili lina matatizo makubwa sana na ni matatizo ambayo yanatuvunja moyo kwa wakati mwengine. Juzi Mhe. Spika, kulikuwa na meli inayotoka Pemba ilifika Zanzibar sio kwa muda wake ambao unatakiwa na wakati katika meli ile kuna watu wengine hawana uwezo wa kusimama, wengine ni walemavu na kuna wagonjwa. Kwa kweli huu ni usumbufu mkubwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ajitahidi kuziangalia hizi meli, aziangalie pale ambapo pana matatizo aweze kuyatatua, kwa sababu meli zetu ni mbovu na sasa hivi zinatutia wasi wasi hasa wakati wa kusafiri.

Mhe. Spika, nije katika barabara yangu ya Kangani. Mhe. Mohammed keshaieleza. Kwa hivyo, naamini Mhe. Waziri ameshasikia, naamini Mhe. Waziri atanitekelezea ombi langu hili, naamini ni kazi nyingi tu zimemzonga lakini kwa imani yake naamini atanisaidia katika barabara yangu ya Kangani kwenda Kukuu.

Vile vile Mhe. Spika, kuna barabara nyengine za ndani, kama barabara ya Mtadoda kutoka Mgagadu Mtadoda. Kuna barabara ya Tondooni Kangani au Tondooni Mjimbini. Kuna barabara ya Kikwete Kengeja. Mhe. Spika, naamini Mhe. Waziri barabara hizi zote hata kuzijua hazijui. Lakini simlaumu, kwa sababu anayejua mambo yote hayo ya ulimwengu ni Mwenyezi Mungu peke yake. Naamini na yeye wakati tumeshamueleza basi atazifuatilia ili kuzipatia ufumbuzi.

Mhe. Spika, nije kwenye Kampuni ya Zantel. Naipongeza kampuni hii ya simu za mikononi. Mhe. Spika, kampuni hii kwa ujumla ina kazi kubwa sana ya kutuunganisha Wazanzibari ndani na nje ya nchi yetu. Lakini kampuni hii bado haijawa na utaratibu zaidi wa kutuendeleza na zaidi vijijini. Kwa mfano katika Jimbo langu la Mtambile, Kangani Kukuu bado kuna matatizo ya kupata mawasiliano. Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri suala hili alipatie ufumbuzi zaidi.

Mhe. Spika, kwa vile sisi ni wajumbe na mwakilishi yeyote sio lazima kuona matatizo yanatoka kwake tu, lakini hata kama matatizo yanatoka kwengine, basi naamini Mhe. Waziri utaweza kuyatatua.

Kwa mfano kama Jimbo la Dimani la Mhe. Mwinyihaji. Jimbo hili pia lina matatizo ya kupatikana kwa mawasiliano ya simu. Sehemu za Maungani hata ukipigiwa simu basi hupatikani inakuwa ni matatizo. Hivyo, namuomba Mhe. Waziri afanye jitihada zaidi ya kutembelea sehemu hizi na kuona matatizo yake.

Mhe. Spika, vile vile nije kwenye Idara ya Leseni. Mhe. Spika, naipongeza idara hii kwa kuanzisha vyuo vya udereva na kutoa leseni kwa wahitimu. Pamoja na kutolewa leseni kwa wahitimu bado kuna ongezeko la ajali za barabarani na ajali hizi zinatutia unyonge sana. Kwa sababu kwanza madereva wetu hata akipewa ile leseni tayari yeye keshafurahia kuwa mimi tayari nimesha *top*. Lakini anapotoka pale tu basi zile sheria zote analizosomeshwa huwa hazifuati na ndio maana ikawa ajali nyingi za barabarani hutokea. Kama ingekuwa sheria anazozisoma pale basi ingekuwa ajali nyingi za barabarani hakuna.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri afanye jitihada ya makusudi ya kuweza kuwaelimisha madereva wetu, ili wajuwe kuwa barabara sio ya madereva peke yao, barabra ni ya watu wote, barabarani kuna jamii nyingi inatembea. Kuna wanyama, kuna viumbe walemavu, kuna watoto wadogo na kuna wengine vipofu Mhe. Spika. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aliangalie suala hili sana, kwa sababu ajali barabarani Zanzibar zimekuwa kubwa mno.

Mwisho Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kuniona. Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na wafanyakazi wake wote. Pia nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kumchagua Mhe. Naibu Waziri kutoka ndani ya Umoja wa Vijana.

Mhe. Spika, nakwenda kwenye sekta ya usafiri wa nchi kavu. Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Zanzibar katika kampeni zake aliahidi kuitengeneza barabara inayotoka Kiuyu Penjewani mpaka Mjini Kiuyu. Lakini kwenye bajeti hii sikuiona bajeti ambayo itatengeneza barabara hiyo inayotoka Kiuyu Penjewani mpaka Mjini Kiuyu. Barabara hii ya Mjini Kiuyu wa wanakijiji wa Mjini Kiuyu. Wanakijiji wa Mjini Kiuyu wanapoteza maisha yao sana wakina mama wajawazito wanapotakakujifungua.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kwenye majumuisho yake anieleze ni kwa nini barabara hii ya Mjini Kiuyu haikuingizwa katika bajeti hii.

Vile vile nichangie hizo hizo barabara zetu za Pemba Mhe Spika, ambapo nyingi ziko karibu na skuli, lakini barabara hizi hazina matuta. Tukianzia katika Wilaya ya Wete, katika Skuli ya Minungwini, Skuli ya Mzambarauni, Skuli ya Jadida na Skuli ya Utaani. Mhe. Spika, barabara hizi zote ziko karibu na skuli ambazo wanasoma wanafunzi.

Pia Mhe. Spika, katika Wilaya ya Mkoani na Wilaya ya Chake Chake. Mhe. Spika, katika Skuli ya Mbuzini zinatokea ajali mara kwa mara na wanaopata ajali pale Skuli ya Mbuzini ni wanafunzi. Je, Mhe. Waziri ataliangalia vipi suala hili, kwa sababu ni muhimu kujengwa matuta kwenye barabara hizo.

Mwisho Mhe. Spika, kwa niaba ya vijana wenzangu wote wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla na kina mama wa Mkoa wa Kaskazini Pemba naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano. Mhe. Spika, napenda kwanza nichukuwe nafasi hii kumpongeza Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake wote wa wizara hii.

Mhe. Spika, wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano imejikita zaidi juu ya kuendeleza miundombinu ya barabara kutoa huduma za aina zote za usafiri wa anga, usafiri wa nchi kavu pamoja na usafiri wa baharini. Jengine ambalo wizara hii imejikita ni katika mambo ya mawasiliano.

Mhe. Spika, katika mambo ambayo nimeyataja ni mambo muhimu ambayo wizara hii ina kazi kubwa ya kuyatekeleza. Nisetu tu kwamba waziri bado ni mpya katika suala hili na naibu wake vile vile ni mpya. Kwa hivyo, kwa jinsi kazi inavyoonesha ni kubwa sana na wamejitahidi vya kutosha kukiandaa kitabu chao vizuri kabisa na wanastahiki pongezi katika kasuala haya.

Mhe. Spika, barabara hizi zote ni nyingi sana na zimeanzia hapa Unguja na nyengine ziko Pemba. Kila sehemu ya barabara ya hapa Unguja wamejaribu kuziandika na wanazitekeleza. Katika barabara hizi ambazo ziko hapa ni miongoni mwa barabara nyengine ambazo zilikuwa zimesalia katika kipindi kile kilichopita zinaendelea. Kwenye miradi hii ya barabara ilioko Unguja na Pemba ni miradi ambayo inafadhiliwa na mataifa ya nje na barabara nyengine ni mchanganyiko baina ya wizara na wafadhili na kuna barabara nyengine zinafadhiliwa na wizara yenyewe. Mimi nasema kwamba waziri anajitahidi kweli kweli, ili kuhakikisha kwamba pamoja na zile zilizokuwa zimepita bado zinaendelea.

Mhe. Spika, napenda nimwambie Mhe. Waziri kwamba kazi aliyonayo ni kubwa sana, barabara hizi ni nyingi na fedha ambayo aliyoipata katika suala hili ni kidogo. Kwa hivyo, kwenda kwake zinakwenda kidogo kidogo kwa kujisuasua. Kama zile barabara zilizokuwa zimepita kwa mara ile zilikosa kwenda kwa wakati kwa sababu ya fedha ni kidogo. Kwa hivyo, nimwambie tu Mhe. Waziri kwamba pamoja na jitihada yake ya kuziangalia au miradi yote hii ambayo ameiandika katika kitabu chake ajitahidi katika miradi hii, ahakikishe mara hii kwamba barabara hizi zimekwenda vizuri. Vile vile tuhakikishe kwamba barabara hizi ziwe zina uangalizi mzuri ili kuona kuwa barabara hizi zimekuwa imara kabisa.

Mhe. Spika, baada ya hilo la miundombinu, sasa niingie katika suala zima la Msitu wa Hifadhi wa Kimataifa ambao ni msitu wa Ngezi. Mhe. Spika, katika kipindi kilichopita tuliwahi kuzungumza mara nyingi juu ya suala la barabara

mbayo inapita katika Msitu wa Ngezi. Barabara hii kwa muda mrefu tumeizungumza katika Baraza, lakini bado haijapatikana mafanikio.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba barabara hii ni barabara ya asili na iliyokuwa inalazimika katika Wizara ya Mawasiliano barabara hii waitengeneze, kwa sababu kuna usafiri wamagari unaotoka Konde moja kwa moja mpaka kupitia msitu ule mpaka Mnarani. Lakini kwa namna moja mpaka nyengine, kwa sababu ule ni msitu wa hifadhi, basi Wizara ya Kilimo na Maliasili haikuwa tayari kuitengeneza barabara ile katika kiwango cha lami. Hata kuitengeneza kwa kuitia kifusi vile vile hawakuwa tayari.

Mhe. Spika, tumejaribu kuizungumza mara kwa mara kwamba ile ni barabara ya asili na iko tokea zamani, kama barabara ile iko chini ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, basi ina haki barabara ile ya kutengenezwa. Lakini kwa bahati mbaya haikuwezekana. Mara hii baada ya makubaliano na waziri huyo mpya alioko tukakubaliana tuitengeneze ile barabara kwa kujaza kifusi katika maeneo ambayo yana mashimo. Kwa bahati kazi ile iliwahi kufanyika, lakini Wizara ya Kilimo na Maliasili ilikuja juu na ikachukua hatua ya kusema kwamba kama mtaendelea kuitengeneza barabara hiyo basi tutawashitaki. Kwa kweli hili suala na mimi nililipata na nilionana na waziri na wakurugenzi walikuja na wakaangalia ile kazi walisema wao wameharibiwa, lakini hakuna kilichoharibiwa ila wao hawataki barabara ile itengenezwe kwa hali yoyote iwachwe vile vile.

Mhe. Spika, mimi nilisema kwamba watu wa kilimo bora wajifunze, kwa sababu ikiwa suala la kwamba barabara ile isitengenezwe. Kuna barabara za Jozani imepita lami, kuna barabara ya Micheweni imepita lami wala hakuna msitu uliokuwa umeharibika. Mimi nasema wapatiwe safari hawa watu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili wapelekwe huko Bara wakaone ni jinsi gani barabara zilivyopita katika misitu ya hifadhi vile vile. Lakini kwa sababu huu ni msitu wa hifadhi wakakataa. Suala hili tumezungumza na waziri na akasema kwamba watazungumza na Waziri wa Kilimo na Maliasili kwamba watatafuta namna ya kuweza kuwafikishia barabara watu wa kutoka Konde mpaka Mnarani. Kwa hivyo, mimi suala langu linabakia pale pale kwamba nataka nimuulize Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwamba je, katika suala hili mmefikia wapi. Je, ndio basi itabakia vile vile au mmeshakubalia na waziri kwamba barabara ile muitengeneze.

Mhe. Spika, baada ya hilo nataka niendelee na barabara nyengine ambayo ni ya Konde Msuka, barabara hii Mhe. Spika, bado haijapata bahati ya kuweza kuwekwa lami, kwa sababu barabara hii sio katika *feeder road*, lakini ni katika barabara kuu inayoendelea kutoka Konde moja kwa moja mpaka Msuka. Nashukuru kwamba barabara hii baada ya kuzungumza na wakuu wa

mawasiliano wamekubali kuitengeneza barabara ile kidogo kidogo kwa kuweka *culvert* katika maeneo yote ambayo ni ya hatari wakati wa mvua. Wameniambia kwamba wataweza kuitengeneza ile barabara.

Sasa nilitaka vile vile baada ya hiyo kazi ndogo ambayo tayari barabara ile imefanyiwa. Naomba wizara hii kwamba tuweze kuitia kifusi, kwa sababu barabara hii ni muhimu na ni barabara ya kilomita kiasi tatu na kidogo. Kwa hivyo, ningemuomba tena Mhe. Waziri, lakini zaidi nimuombe Mhe. Waziri kwamba katika kipindi hiki chake cha bajeti basi aweze na mimi kunimegea fedha kidogo kwa kuwaza kukitia kifusi ile barabara.

Mhe. Spika, baada ya barabara hiyo kuna barabara nyengine ya Ungi Msuka. Barabara hii iliwahi kuombwa na wananchi wakati wa kipindi cha Rais Aman Abeid Karume na Rais alitoa ahadi mbele ya wananchi hao kwamba barabara ile atawatengenezea kwa kuwatilia kifusi. Kipindi kile barabara hii haikuwezekana. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri ile ahadi ya Rais bado haijaondoka iko pale pale. Hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri ajitahidi katika kufanikisha maamuzi ya Rais aliyepita.

Mhe. Spika, baada ya hilo ningelimuambia tu Mhe. Waziri kama kuna maneno yanazungumzwa kwenye mnara wa Kigomasha, kwamba mara nyingi mnara huu huwa hauwaki sawa sawa na ni mnara muhimu sana wa Kigomasha unatakiwa kuwaka, lakini mara nyingi unakuwa hauwaki. Lakini zaidi ambalo nalipata katika mnara huu ni kwamba kuna vifaa vya asili katika ule mnara, kwa sababu ule mnara ulikuwa unawaka kwa kutoa rangi mbali mbali kulikuwa na rangi nyekundu, rangi ya manjano, rangi za bluu sasa inaonyesha kwamba vifaa vyake vile havipo tena.

Sasa namuuliza Mhe. Waziri vile vifaa vyake pamoja na zana zake za zamani ule mnara wa asili vifaa vyake vimekwenda wapi, halafu kwa nini mnara ule ukawa unaleta matatizo mara kwa mara hauwaki. Hilo ningelimuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa aniletee taafira yake.

Jambo jengine ambalo nataka nilizungumze ni suala zima la mawasiliano tuko katika karne ya sayansi na teknolojia, ambapo mawasiliano ya habari na tekinolojia yana nafasi kubwa katika eneo la utafiti. Mhe. Spika, ukitizama wizara zetu zote tulizokuwa nazo kuna kitu tunaita sera mipango na utafiti sasa kila wizara inakuwa nayo hii, sasa huu mtandao wa mawasiliano wa *internet* ni muhimu sana katika kuimarisha tafiti zetu zote tulizonazo na katika kila wizara kila Mkurugenzi anapewa nafasi hiyo kwa maana yeye anakuwa ni mtafiti katika upande wake wa wizara, kushughulikia tafiti za upande wake katika Wizara yake au idara yake aliyopewa na aweze kuifanya kwa vizuri.

Saa mimi nataka nimshauri Mhe. Waziri kama itawezekana wakati anapokaa yeye pamoja na makatibu wakuu wa Wizara hili suala tungeliweka katika kikao likawa katika kikao cha mazungumzo, kwa kuwa mawizara haya wakurugenzi waliomo katika mawizara haya ni wakurugenzi wa suala zima la mambo ya utafiti. Ningeliomba mimi suala hili tukalifanya *one cowmen centre* yaani tukawa na pahala pamoja pa utafiti, ikawa hii ni idara kubwa ambayo inashughulika na tafiti zote za Mawizara haidhuru Waziri atakuwa katika Wizara yake, atakuwa na tafiti zake lakini tafiti zile kuwe na pahala ambapo wakurugenzi wale wawe wanapeleka tafiti zao pawe na Kiongozi au *director* au meneja na kifunguliwe kama kitu kipya, kuliko ninachoamini mimi hivi sasa kwamba Wakurugenzi wanapopewa nafasi hizi za kufanya tafiti katika wizara zao huwa hili suala halifanyiki wala hapafanywi kitu chochote ni jina tu utafiti lakini hapafanywi utafiti wa aina yoyote.

Kwa hivyo ili kuondosha hizi tuhuma za Wakurugenzi kwamba shughuli zao haziendi vizuri ningeshauri au ningemshauri Waziri aweze kukaa pamoja na Makatibu Wakuu wakati wanapokutana waweze kuzaa fikra hiyo ya kuweka kitu kimoja, wawe na *center* moja ya utafiti kwa sehemu zote. Na wao watakuwa wanatoa ripoti zao katika mawizara yao nafikri suala hilo baadae Mhe. Waziri baadae aweze kunieleza wakati wa majumuisho kwamba hilo suala linawezekana au haliwezekani.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka niseme kwa kuipa hongeza wizara hii jambo ambalo la kufurahisha kwenye ukusanyaji wa mapato, Mhe. Spika, napenda nitoe pongezi kwa wizara hii kwa hatua nzuri juu ya ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe inaonekana tumetosheka na mjadala lakini muda umebakia kidogo tu tumalize ili kesho tufanye majumuisho, kwa hivyo Mhe. Suleiman na wewe chukua muda mchache sana kuna mjumbe ameniomba dakika tano.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, nitoe pongezi kwa wizara hii kwa hatua nzuri na za kufurahisha juu ya ukusanyaji wa mapato kwa sekta mbali mbali za wizara, kwa mfano katika mamlaka ya kiwanja cha ndege, mamlaka ya usafiri wa baharini, shirika la bandari na shirika la meli. Niseme tu Wizara imetekeleza majukumu yake kwa sekta zote hizo na mapato yamekusanywa vizuri, kwa hivyo katika kukusanya mapato bila ya shaka yanasaidia kukamilisha uchumi wetu au kukuza uchumi wetu pia inachangia bajeti ya serikali katika mgao ambao uko katika *selling.*

Namuomba Mhe. Waziri katika suala hili ajitahidi sana kwenye ukusanyaji wa mapato jambo ambalo ni muhimu sana, jambo ambalo kila siku linapigiwa

kelele kwamba makusanyo haya hayakusanywi vizuri lakini nashukuru katika sekta zake linakwenda vizuri.

Jambo jengine ningelimuomba Mhe. Waziri katika suala zima la madeni ambalo yeye kuna sekta anazidai, kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri madeni haya ambayo unazidai kekta nyengine ufanye jitihada uweze kuzikusanya.

Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Waziri kutokana na jitihada za kuweka jengo ambalo linategemewa la Uwanja wa ndege wa kimataifa, kwa hivyo nampongeza Mhe. Waziri vile vile kwenye suala hilo muhimu ambalo litaleta changamoto ya uchumi katika nchi yetu ya kuongeza mapato.

Kwa haya machache nasema naunga mkono hoja hii mia kwa mia pamoja na watendaji wako wote *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kuniona kwa jicho la huruma pengine hata dakika tano zisifike Mhe. Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mhe. Rais kwa uteuzi wake aliofanya mahiri kabisa kwa vijana wetu hawa wawili Mhe. Hamad Masoud na Mhe. Issa Gavu kutoka Mkoa wa Kusini, niwapongeze kwa dhati kabisa kwa utendaji wao mahiri bila ya kumsahau Katibu Mkuu *doctor* Lilla hii ni wizara ya mfano peke yake kuigwa kwa utendaji.

Mhe. Spika, nitakuwa sio mwingi wa fadhila kama sikumshukuru Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari Mhe. Mustafa Aboud Jumbe, pamoja na hayo Mhe. Waziri hakukaa ofisini tu hutoka mpaka *field* akangalia mwenyewe kazi zinafanywa vipi kutokana na umahiri wake ni mchapa kazi wa kweli kweli sio masihara, hapa Mhe. Rais amegusa ndipo.

Vile vile nimshukuru Mhe. Mustafa Aboud Jumbe kutokana na utendaji wake wa kazi maana yake ata sijui saa ngapi anaingia kazini na sijui saa ngapi anatoka kazini, saa moja ukenda kazini yupo na saa tisa ukenda kazini yupo, magharibi yupo kazini vile vile. Pamoja na nafasi ya bandari kuwa finyu meli moja ikifunga nafasi hamna tena tusubiri siku ya pili, kafanya kazi katika kipindi kizito na kigumu, cha kushangaza hivi sasa bandari ina mtihani mkubwa kuhusu taa za bandarini, muwangaza wake hautoshi, vibaka wamekuwa wengi ndani imejengwa bandari lakini bila ya kuzingatia ramani ya taa ndani hazikidhi kabisa. Tatizo lile lile la wimbo wa taifa maji hayapatikani katika bandari yetu ni mtihani mkubwa ulioje.

J engine Mhe. Spika, bandari yetu finyu na haikidhi mahitajio hapo mwanzo wafanyakazi na wafanya biashara walikuwa wakiruhusu kushusha viazi vyao

wakati wa usiku, lakini kwa ghafla na kwa masikitiko makubwa wamezuiwa sasa hivi kushusha mizigo usiku sijui ni sababu zipi zimepelekea tatizo hilo na tunajua ufinyu wa bandari ni mdogo ukilinganisha wakati wa asubuhi magari yanakuwa mengi, msukumano ndani ya bandari umekuwa mkubwa nafasi haikidhi sijui kinachosababisha ni kitu gani.

Nije katika suala la barabara kwa masikitiko makubwa sijui sababu gani zinazosababisha barabara ya Malindi kuja zake Forodhani kufungwa, sijui tuangalie hasara gani tunayoipata pale na faida gani tunayoipata pale kufunga barabara ile, ikiwa kisingizio ni Mji Mkongwe mimi sikumbuki kujengwa barabara mimi barabara zote ni wizara ya miundombinu. Pale serikali inakosa mapato chungu nzima kwa baraza la manispaa kuhusu paki, juzi juzi kumetoka matukio ya kijambazi kuhusu barabara ile kufungwa wamekamatwa na bastola. Sasa hili Mhe.Waziri nataka maelezo sababu gani barabara hizi kufungwa.

Kuhusu Shirika la Meli tumeambiwa wamekusanya pesa nyingi sana lakini sijui inajua kwamba inadaiwa na kampuni ya Mkunazini karibu dola 230 na sijui ina mpango gani wa kulipa pesa hizo na muda mrefu na hii ni amri ya Mahakama. Hili nalo nitahitaji maelezo Mhe. Waziri.

Kuna ununuzi wa kifaa hiki cha *GMDSS* nafikri karibu miezi sita mpaka minane tokea kufika hapa sijui kinafungwa lini kama huyo aliyetumiwa tiketi hajafika au anakuja kwa miguu, ni kifaa muhimu sana leo utakuta simu hazifanyi kazi karibu wiki moja mpaka mbili sijui watu wanawasiliana vipi na kituo muhimu kabisa hiki cha kuingiza meli na kutoa meli. Aliuliza Mhe. Hija Hassan Hija hapa akaambiwa nadhani lakini sisemi nadhani nazungumza kwa uhakika imeshafika mpaka wiki moja au wiki mbili simu hazifanyi kazi mule. Hili nalo Mhe. Waziri tunahitaji maelezo kutoka kwako.

Kwa vile sadaka inaanza nyumbani Mhe. Issa Gavu yuko jirani yangu hapa itabidi niwe nyuma yake tu. Mhe. Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ni kweli ametumia dakika tano hakuzidisha. Mhe. Subeit nakuhurumia sana sasa kuna dakika saba tu sijui utafanyaje, kama unaweza kuweka *point* zako mbili tatu basi tumia dakika hizo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii lakini kwa kweli naona muda uliobakia labda niwashukuru tu, mimi nawashukuru sana Wizara ya Mawasiliano nawashukuru sana watendaji wote wa Wizara ya mawasiliano kwa ujasiri wao na mimi naamini kama ni muda mchache tu tangu kuingia Mhe.Hamad Masoud kushika wadhifa huu. Naamini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tumpe subira ishaala tutafaidi.

Mhe. Spika, nakushukuru sana Ahsante.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe wajumbe ambao waliomba wachangie jumla yao walikuwa ni 38 tumemudu kuita kiasi 25 tu na kesho asubuhi hoja hii inabidi tufanye majumuisho, sijamuita waziri hata mmoja ambao wapo wawili watatu walioomba ili wamsaidie Mhe. Waziri kabla ya yeye hajafanya majumuisho. Hivyo niwaombe radhi waheshimiwa wajumbe wote wale ambao hawakupata nafasi ya kuchangia, ningependa sana wote wangeweza kuchangia ili kumsaidia sana Mhe. Waziri lakini muda ulikuwa hautoshi kufanya hivyo.

Sasa waheshimiwa Mawaziri ambao watakuja kuchangia keso asubuhi kabla ya kumwita Mhe. Waziri ni pamoja na Mhe. Naibu Waziri wa Bishara Viwanda na Masoko, Mhe. Waziri asiyekuwa na Wizara maalum Mhe. Machano Othman Said pamoja na Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na mawasiliano.

Baada ya hapo nitawaomba waheshimiwa wajumbe wakubali kumsikiliza Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, baada ya hapo nitawaomba waheshimiwa wajumbe mukubali Mhe. Waziri afanye majumuisho kwa angalau yale mawili matatu ambayo mmemuuliza na kutaka atoe kauli ili hatimae tumalize shughuli hii kesho asubuhi.

(Saa 1.40 Usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 14/7/2011 Saa 3.00 asubuhi)